

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini - Tarehe 30 Juni, 2010

(Mkutano ulanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anna S.Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA :

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA, MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE. GRACE S. KIWELU, MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:-

Taarifa ya Msemadi wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 141

Barabara ya Nyakagomba- Katoro

MHE.ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA) aliuliza:-

Barabara ya Nyakagomba – Katoro kupitia Inyala inahudumia Kata zilizo katika Tarafa ya Butundwe kusafirisha mazao na bidhaa za biashara, lakini barabara hii haipitiki katika majira yote na kuwafanya wananchi wa maeneo husika kushindwa kufanya shughuli za maendeleo, na kwa sababu Halmashauri husika imeshindwa kulitatua tatizo hilo kutokana na Bajeti finyu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipandisha hadhi barabara hiyo iwe ya Mkoa ili iweze kuhudumiwa kimko na kumaliza tatizo hilo kabisa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nyakagomba- Katoro kupitia Inyala ina hudunia Kata zilizoko katika Tarafa ya Butundwe. Barabara hii kwa sasa inapitika kwa shida na inahitaji matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina jumla ya urefu wa kilomita 14 ambazo wastani wa kilomita 1.5 ni eneo la mbuga linalohitaji kuinuliwa tuta na kuweka karavati za kutosha kupitisha maji. Urefu uliobakia unahitaji ukarabati. Katika Bajeti ya fedha ya mwaka 2009/2010, barabara hii ilitengewa shilingi milioni kumi.

Aidha Bajeti ya mwaka 2010/2011, barabara ya Nyakagomba-Katoro imetengewa kiasi cha shilingi milioni 23. Kiasi hiki kinatosha kuifanya barabara hii ipitike wakati fedha ya kufanyo matengenezo makubwa inaendelea kutafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hupandishwa daraja iwapo tu inakidhi vigezo vya daraja inaloombewa kulingana na kanuni za sheria ya barabara. Kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, taratibu za kupandisha hadhi ya barabara huanzia katika vikao vya Halmashauri husika baadaye mapendekozo hupelekwa kwenye Kikao cha Bodi ya Barabara cha Mkoa, ambacho pia kikirithika na maombi hayo, hupeleka mapendekozo kwa Waziri mwenye dhamana yaani Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita inashauriwa kufuata utaratibu huo ili kuweza kuipandisha daraja barabara iwapo itaonekana inastahili.

MHE.ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuluru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuulizamaswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa mwaka huu wa Bajeti ametenga milioni 23 za barabara hii amekiri kabisa kwamba inapitika kwa shida:-

- (1) Je, hii milioni 23 inaweza kutosheleza?
- (2) Kwa kuwa barabara iliyotajwa katika swali la msingi linafanana kabisa na matatizo ya barabara ya Kamanga kwenda Sengerema na kwenda Geita. Je, Serikali haioni sasa umuhimu kwa kuwa tumetengeneza lami kuitia Usagara na hii barabara ikapewa umuhimu kuwekewa lami kuitika vizuri?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi milioni 23 ni kweli hazitoshi na sisi hapa tumesema kwamba hazitoshi, hizi ndio hela ambazo tumeziingiza katika bajeti hii ambayo tumepitisha hapa. Ndizo hizo zilizopitishwa kwa maanake kulikuwa kuna vigezo vilivyoleta. Bajeti hii wakati inaletwa hapa ilianzia kule kijijini ikaenda kwenye Halmashauri, ilipotoka kwenye Halmashauri ikaenda Mkoani, ilipopita Mkoani , Mkuu wa Mkoa akaenda akai-*defend* pale Dar es Salaam baada ya hapo Waziri Mkuu akaipokea ndio hiyo tukaja nayo hapa na bahati nzuri mmeshaipitisha.

Sasa tunachoweza kusaidia katika hilo eneo, ni kwamba sasa twende tukakae kule na wataalamu tuandike sasa kitu kinachoitwa andiko, tutengeneze sasa kitu ambacho kinaweza kikasaidia tukimpata mhisani atusaidie kutengeneza hiyo barabara lakini as far as this Budget is concerned, out. Habari imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii barabara nyingine, naielewa *concern* ya ndugu yangu Mheshimiwa Nyawazwa najua kabisa kwamba kuna hilo tatizo sasa tuje kule tushirikiane wote kwa pamoja, hata kitu kinachoitwa *special request* siku hizi, Serikali huwa haisikilizi tena kwa sababu tuna *cash budget*. Ukishasema ni shilingi elfu kumi, ni elfu kumi kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la barabara nyingine ambayo ameitamka hapa Mheshimiwa Nyawazwa na kwamba inapanda kwa kiwango cha lami, sisi wote hapa tumemsikia Waziri wa Miundombinu akituambia kwamba kilomita 1 ya lami inafikia karibu shilingi milioni 800 inakwenda karibu shilingi bilioni 1. nikiitikia hapa mtajua kabisa tunae Naibu Waziri kituko, kwa sababu hili nalionna, nalijua kwamba ni jambo muhimu, tuje tukae wote kwa pamoja tuiangalie halafu baadae tutafakari kwa pamoja kwamba ni nini kifanyike ili tuweze kuweka barabara ya lami pale.

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa tunapeleka pesa nyingi katika barabara za Halmashauri zetu, tukishazitengeneza mvua zinakuja ule udongo wote unaondoka, Bajeti ijayo tunapeleka pesa nyingi. Sasa kweli hizi pesa zinapotea nyingi sana. Kwa nini Serikali isiweke utaratibu sasa wa kuweka lami nyepesi katika maeneo yetu ambayo at least itachukua miaka mitano mpaka kuja kuitengeneza upya.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana nae kabisa kwamba wakati mvua zinaponyesha wakati mwagine zinasomba hizi *moramu* zinaondoka. Sasa kinachofanyika katika ujenzi ni kuangalia kama mkiona sasa ni wakati wa mvua mniamwambia mkandarasi ambaye mmekabidhi kazi ile aache mnganje kwanza mvua zipite.

Lakini la pili analolizungumza hapa, anazungumzia hii ya kuweka lami nyepesi nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Wizara tunao mradi ambao unafanya *pilot study* katika Wilaya fulani fulani katika nchi yetu ambao utaangalia uwezekano wa kuweka hiyo lami nyepesi katika maeneo yale ambayo ni korofi ili tuondokane na hili tatizo. Kwa hiyo, tunakubaliana kabisa na ushauri ambao anautoa Mheshimiwa Mbunge.

MHE. CASTOR R. LIGALAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Wilaya yangu ya Kilombero kuna madaraja mawili ya Mto Mfaji na Mto Luipa ambayo kwa Bajeti ya Halmashuri kwa vyovyyote vile hawataweza kujenga madaraja hayo:-

Je, Serikali inaweza kuoanisha hadhi ya madaraja tu na barabra ikabaki Halmashauri?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachofahamu hapa tunachofanya ni kupandisha hadhi ya barabara sasa kama ndani yake kuna haya madaraja yanayozungumzwa hapa *then* na Mheshimiwa Kawambwa yupo nyuma hapo ananisikiliza ntakwenda kumwiliza vizuri, halafu nitakuja kumjibu vizuri.

Lakini ninachojuwa kinachopandishwa hadhi huwa kwa kweli sio madaraja kinachopandishwa hadhi ni barabara ndizo zinapandishwa hadhi na yeze ndio huwa anafanya hivyo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongeza katika majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba changamoto katika barabara zetu Tanzania nzima tunazifahamu na kuna barabara hizi ambazo ni za Wilaya hazihudumiwi na *TANROAD*.

Baadhi yake zina changamoto kubwa hasa katika maeneo ya madaraja na nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwa maeneo yale ambayo ameyataja yenye matatizo makubwa ya ujenzi wa madaraja kwamba uwezo wa Halmashauri ni mdogo awasilishe Wizarani ili Serikali iangalie namna ya kusaidia kama ambavyo tumefanya katika maeneo mengine.

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa Ligalama angeuliza hivi, TAMISEMI kweli lakini haina fedha ya kufanya baadhi ya vitu vingine ikiwemo madaraja, hilo swalilinge kuwa la kisera, lakini ukimwibia eneo *specific* kweli Waziri unamtakia magumu sana.

Na. 142

Zoezi la Ujenzi wa Ofisi za Wtendaji Kata Nchini

MHE. ANIA S. CHAUREMBO aliuliza:-

Halmashauri nyingi nchini zipo katika mchakato wa ujenzi wa Ofisi za Watendaji Kata na katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna baadhi ya maeneo ya Kata hayana nafasi ya viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hizo:-

- (a) Je, hali ya ujenzi wa Ofisi za Watendaji Kata nchini ukoje?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzisa idia Halmashauri zenyne shida ya kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hizo za Watendaji Kata?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swalilige kuwa la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri nyingi nchini zipo katika mchakato wa ujenzi wa Ofisi za Kata ambapo ujenzi huu umekuwa ukifanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Ofisi za Kata nchini unaendelea vizuri na jumla ya Ofisi za Kata 2500 sawa na asilimia 53% ujenzi wake upo katika hatua mbalimbali. Aidha, jumla ya Ofisi za Kata 1000 zinatarajiwa kujengwa na Halmashauri nchini kote na fedha zimekuwa zikitengwa katika Bajeti ili kuhakikisha upatikana ji wa

Ofisi hizo. Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (*CDG*) imekuwa ikisaidia katika ujenzi wa Ofisi pamoja na Halmashauri zenyewe kuchangia kwa kutumia mapato yao ya ndani na kwa kushirikisha na wananchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mara kwa mara inatoa miongozo na maelekezo kwa Halmashauri kuhakikisha kuwa wanatenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kijamii ikiwemo ujenzi wa Ofisi za Kata.

Kwa kuzingatia maelekezo hayo, Halmashauri zinaendelea kufanya jitihada za kununua maeneo kwa sehemu ambazo upatikanaji wa ardhi umekuwa mgumu kama vile Kata za Kariakoo, Jangwani na Kisutu kwa ajili ya shughuli za huduma za kijamii ukiwemo ujenzi wa Ofisi za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo napenda kuchukua nafasi kusisitiza Halmashuri nchini kutimiza wajibu wao wa kutenga maeneo kwa ajili ya huduma za kijamii ikiwepo Ofisi za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam katika Manispaa ya Ilala, Kinondoni na Temeke ni mionganoni mwa Halmashauri zenyete tatizo la kupata ardhi.

Hata hivyo, Manispaa hizo zimeweka mikakati ya kununua majengo ili kupata Ofisi za Kata. Kwa mfano Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ina jumla ya Kata 26 na zenyete Ofisi ni 19. Kwa mwaka 2010/2011 Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imepanga kujenga Ofisi 4 za Kata na eneo limepatikana kwa ajili ya kazi hiyo.

Aidha, Kata za Kariakoo, Jangwani na Kisutu lipo katika tatizo la kupata ardhi. Hivyo, Halmashauri inafanya jitihada za kununua majengo. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ina Kata 5 ambazo hazina Ofisi na juhudhi zinaendelea ili kupata viwanja vyta kujenga ofisi hizo. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ipo Kata moja ambayo haina Ofisi na katika mwaka 2010/2011 Ofisi itajengwa kwa sababu hakuna tatizo la ardhi.

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Waziri na ufanuzi mkubwa aliota katika hata sehemu zile ambazo haziwezekani kupata ardhi kwa ajili ya kujenga Kata, sasa kuna mpango wa kununua maeneo au nyumba za kusaidia Kata hizo. Sasa ni swali moja la nyongeza:-

Hivi karibuni tumekuwa tukisikia katika taarifa kwamba kuna baadhi ya Watendaji Kata ambao wanakuwa hawana nidhamu hata kupelekea wengine kusimamishwa kazi na wengine kufukuzwa kazi na wengine kufukuzwa kazi. Sasa mimi ningependa kujua sasa. (*Makofî*)

Waziri atueleze hali hii iko kwa kiwango gani hapa nchini kuhusu maafisa Watendaji wa Kata na vile vile isitoshe aeleze kwamba ni lini sasa au Serikali itakuwa tayari sasa kutoa mafunzo sasa ya ziada kwa watendaji hawa, maafisa wa Kata ili kuelewa zaidi kazi yao ya kiutendaji kusitokee tena hali hii iliyojitekeza hivi karibuni? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, natamani kama ningejua kwamba ningeuliza pia suala la nidhamu na matatizo ambayo yamewatokea watendaji ningekuwa nimekuwa na takwimu zote zinazohitajika kujua kwamba ni wangapi.

Ni kweli kwamba tumekuwa na watendaji ambao wamekuwa na matatizo kwa maana ya watendaji wetu wa Kata na Vijiji na wengine wa namna hiyo kwa matatizo mbalimbali ambayo sintaweza kueleza hapa kwa sababu umenitaka nieleze kwa kifupi sana, lakini kama atahitaji naweza nikaenda nikapitia mara moja halafu baadae nitamjabidhi ili kuweza kumfanya aelewe kwamba hali ikoje katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili la elimu ambalo analizungumza hapa, hilo liko katika utaratibu.

Sasa hivi tuko katika maboresho namba mbili. Kwa hiyo, watendaji wetu wote tunajaribu kuwapa mafunzo na kuwapa elimu na wakati huo huo tumeanzisha kile chuo cha Hombolo amabcho Wabunge waliondoka hapa tukaenda nao kule kwa kweli tunategemea sasa watakuwa wanaenda kule pamoja na Madiwani na watu wengine wote wanaohusika ili tuweze kuwasaidia kuinua kiwango chao cha uelewa. (*Makofii*)

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Kwa kuwa moja ya maeneo muhimu sana ya kutoa huduma kwa wananchi ni Ofisi hizi ma-WEO hasa katika maeneo mbalimbali na kwa kuwa katika maeneo ambayo yaliyosemwa Dar es Salaam tunatofautiana sana na huko katika Wilaya, kwa mfano Iramba Magharibi ambako tuna ardhi ya kutosha lakini hakuna Ofisi za ma-WEO na kwa kuwa Ofisi za ma-WEO zinajumuisha ile Wakuu wa Idara mbalimbali katika zile Kata ili kwenda kutatua yale matatizo lakini hazipo hizo Ofisi.

Je, nataka kuuliza ni nani anayehusika na ujenzi wa Ofisi hizi na katika bajeti ipi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, wanaohusika na ujenzi wa hizo Ofisi ni Halmashauri zenyewe zinazohusika. Ameuliza hapa ni Bajeti gani inayotumika. Hela zinazotumika kwa ajili ya kazi hii ni hela zinazotokana na *Capital Development Grant* pamoja na michango ya wananchi, pamoja na mapato ya ndani ya Halmashauri.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa nafasi hizi za Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji ni nafasi muhimu sana katika maendeleo vijiji. Vijiji vingi havina kabisa Watendaji hao, Serikali inasema nini kuhusu ajira za Watendaji ili vijiji vyetu viweze kupata maendeleo yanayotarajiwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, tatizo hili limetokana na ukweli kwamba katika programu yetu hapa tumekuwa na Watendaji ambao kwa kweli hawaendi kwa kiwango kile tulichokuwa tunataka. Kwa hiyo, tukaingia na hawa Watendaji kwa kipindi cha miaka mitatu. Tukakubaliana kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitatu wahakikishe kwamba wanakwenda shule, wanasoma mpaka kiwango cha *Form Four* bila kujali kama wamefaulu au hawakufaulu lakini walao wafike mpaka *Form Four*. Kwa hiyo, tunapozungumza sasa hivi tunategemea kwamba wale ambao hawatakuwa wamefanya hivyo tutakuwa tumewa-*phase out*.

Lakini kutoka sasa tumeshasema kabisa kwamba utaratibu wa kuwachukua hawa ma-WEO na ma-VEO utakuwa ni kwamba lazima awe anakidhi hiyo hali tunayozungumza ya uelewa na kiwango hicho cha elimu ambacho kinahitajika.

Kwa hiyo, hapa katikati tumekuwa na hilo tatizo kwa sababu wale wanajitokeza kwa kweli wengine unakuta kwamba hawana hicho kiwango kinachohitajika na hatuwezi kuendelea kuwazalisha tena, tuwazalishe wa namna hiyo ndicho kikasababisha hivyo.

Lakini nataka nikuthibitishie kwamba kazi inafanyika sasa hivi kuhakikisha kwamba eneo hili linafanyiwa kazi ndiyo maana tunasikia kuna malalamiko hata hela hazitumiki vizuri ni kwa sababu watu walioko kule wengine uwezo wao bado unakuwa ni mdogo. Lakini matumaini yangu ni kwamba programu hii ikiisha tutakuwa na watu wenye sifa zinazotakiwa.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Watendaji wa Kata ni viongozi muhimu sana katika Kata na wanafanya kazi za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu na kwa kuwa watendaji hawa wanafanyakazi katika mazingira magumu.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba iko haja sasa kutenga kwa ajili ya kujenga Ofisi za Watendaji wa Kata?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapa Bajeti hii lazima itokane na Halmashauri yenye inayohusika.

Nimeeleza mafungu haya yanatoka katika maeneo gani katika *Capital Development Grant*, yanatoka katika mchango wa wananchi wao wenyewe na kama sasa Mheshimiwa Lubeleje anafikiri kwamba kuna haja sasa ya kuweka katika Bajeti kwa maana kabisa uandike pale Ofisi ya Mtendaji wa Kata kiasi hiki ikae pale. Mimi sioni *problem* na hilo, kwa sababu si itakuja tu katika utaratibu wa kawaida na kama ikionekana kwamba inazidi hivyo tunavyosema basi itakuwa imeondolewa pale.

Lakini kama wanafikiri kwamba kule kwao ni kipaumbele kwamba Ofisi ya Mtendaji wa Kata au Ofisi za Watendaji wa Kata ziwekwe pale, wanaweka tu pale kwamba kutengeneza Ofisi kiasi hiki. Wanaleta sisi tunapeleka moja kwa moja.

Na. 143

**Mkakati wa kupambana na tatizo la ajira kwa
Wahitimu wa Vyuo Vikuu**

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Serikali ya Uganda ilitangaza mkakati wa kupambana na tatizo la ajira kwa wahitimu wote wa vyuo vikuu watakaokosa nafasi kwenye soko la ajira nchini Uganda na kuwapatia mikopo ya mitaji ili waanzishe biashara zao, tatizo ambalo pia lipo Tanzania tena kwa kiasi kikubwa:-

- (a) Je, Serikali inasemaje juu ya kuiga mkakati huo mzuri wa Serikali ya Uganda?
- (b) Je, Serikali inaweza kupeleka wataalam Uganda au nchi nyingine kujifunza juu ya mkakati huo ili kuondoa tatizo hilo?
- (c) Je, Serikali haioni kwamba kuwaacha wahitimu kujihangaikia ajira wenyewe kunasababisha wakimbilie nchi nyingine (*brain drain*)?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA
aliibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania iko tayari kuiga mkakati wowote mzuri wa kukuza ajira katika nchi yoyote duniani ikiwemo Uganda. Hata hivyo ni vyema kutambua kwamba, kama nchi na sisi tunazo sera, mikakati na programu za kupambana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini ikiwemo ajira kwa wahitimu kutoka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imechukua hatua mahususi za ki-sera, ki-mkakati na mipango ambayo kwa pamoja imelenga kupunguza kero hii.

Hatua hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008, mpango wa Taifa wa kukuza ajira nchini, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana (*Natural Youth Action Plan*) ambazo zinatoa dira ya kuwawezesha wananchi kujajiri/kuajiriwa.

Aidha, Serikali imekuwa inatekeleza programu mbalimbali za kuwawezesha wananchi ikiwa ni pamoja na vijana wahitimu vyuoni kuwa wajasiriamali na kujajiri ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali kwa kushirikiana na Benki na Asasi za Fedha nchini. Mikopo hii hupitia mifuko ya vijana, wanawake, *SELF* na Mpango wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi yaani Mfuko wa JK.

(ii) Kuratibu utoaji mafunzo ya kuandaa mawazo ya miradi (*business ideas*) na jinsi ya kuanzisha miradi ya uzalishaji bidhaa na kujajiri yanayoendeshwa na *SIDO*, Taasisi ya Tanzania *Private Sector Foundation*, pamoja na Taasisi nyingine binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeanzisha Wakala wa huduma za ajira yaani (*TAESA*) mwaka 2008 na Sekretarieti ya Ajira mwezi Machi, 2010 kwa madhumuni ya kuwawezesha mchakato wa kuunganisha wa kutafuta na waajiri ikiwa ni pamoja na wahitimu wa vyuo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kupeleka wataalam wake kujifunza nchini Uganda au nchi nyingine yoyote yenye mikakati mizuri ya kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira mionganoni mwa wahitimu wa vyuo vikuu. Hii itawezekana baada ya kupata taarifa sahihi zinazohusiana na ubora wa mikakati ya kukuza ajira ya nchi hizo na namna mikakati hiyo inavyoshabihiana na sera, sheria na mikakati yetu ya kukuza ajira nchini.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza hapo juu, Serikali ina sera, mipango na mikakati ya kuwawezesha vijana na wahitimu wa vyuo vikuu kujajiri au

kuajiriwa na si nia ya Serikai kuona wahitimu wa vyuo vikuu wakihangaika bila ajira na mwishowe kukimbilia nchi za nje.

Katika kuendelea kubuni mikakati zaidi kwenye eneo hili, Serikali kupitia Muswada wa Sheria ya Taifa ya Ajira unaokusudiwa kuwasilishwa Bungeni na makakati wa Taifa wa kukuza ajira vinalenga kuanzishwa kwa vituo vya kuwasaidia Watanzania kupata ajira nchi za nje yaani (*Cross Border Placement Units*) na vile vile kuwawezesha Watanzania walioajiriwa nchi za nje kurejesha mapato nchini (*remittances*) na/au kurudi na kujaza nafasi za utaalamu adimu hapa nchini.

MHE. JOHN P. LWANJI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ni kwamba masharti haya ya mikopo kwa wajasiriamali bado inaonyesha kwamba ni migumu na hata urejeshaji wenyewe unaonyesha. Halafu kuna kipindi cha mpito kati ya kumaliza masomo na kupata ajira kwa hao wanafunzi, wakati huo hawana chochote.

Je, Serikali haioni vema kwamba hili kundi maalum lingeweza kufikiriwa kupata mitaji maalum yenyewe masharti nafuu zaidi mpaka hapo watakapo jajiri au kupata kazi?

La pili ni kwamba katika kuwashughulikia hawa wanafunzi imeonekana kwamba

NAIBU SPIKA: Naomba uulize kwa kifupi, watu wote wanakusubiri. Uliza kwa kifupi swalii lako.

MHE. JOHN P. LWANJI: Ndiyo, kutowapatia ajira kwa wakati kwa wanafunzi hawa haionyeshi kwamba Serikali inaidhalilisha elimu na taaluma yenyewe hasa kwa ajili ya wanafunzi, inavyoonekana kwamba wanafunzi hawa ni kama vile wamepoteza wakati wao bure kwenda kusoma, maana kuna *gape* kati ya waliokwenda shule na ambao hawakwenda shule wametajirika lakini hawajakwenda shule. Sasa haioni kwamba inafanya kana kwamba waone wamepoteza muda wao mwangi bila sababu yoyote?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba mikopo inayotolewa kwamba ina masharti magumu, nieleze tu kwamba mifuko hii ambayo nimeelezea kwa kweli jitihada za Serikali katika kuanzisha mifuko hiyo niliyoisema ni kwamba inayo unafuu kuliko mabenki ya kawaida. Hapa kwa kweli Serikali imejitahidi kufanya hivyo ili wapate mikopo nafuu.

Lakini mimi nakubali kwamba kama kuna utaratibu mwengine ambao tunaweza tukapata mikopo nafuu zaidi kuliko mifuko hii ninayo isema, basi Serikali itakuwa tayari kuangalia. Nimesikia nadhani ni jambo zuri kwamba wajasiriamali na hasa vijana wanafikiria kuanzisha benki ya ujasiriamali, Serikali inaweza ikasaidia katika hilo ili

tufike mahali basi tupate mifuko ambayo inaweza kutoa mikopo nafuu zaidi ya hii ambayo inazungumzwa.

Kuhusu kwamba Serikali inachelewa kuwapa ajira wahitimu wa vyuo vikuu. Mimi niseme kwamba mipango ya Serikali ya kutoa ajira iko pale pale. Lakini nafasi za kuajiriwa wahitimu wetu bado hazitoshelezi na ndiyo maana tunasema pamoja na hawa vijana walioko mitaani hata vijana wanaomaliza vyuo vikuu wafikirie kwamba sasa kuna umuhimu na wenyewe kujiajiri bila kutegemea tu kwamba wakimaliza vyuo wataajiriwa. Lazima wabadilike kutoka *job seekers* kwenda *job creators* waweze kujiajiri wenyewe. Hii itasaidia sana pamoja na juhudi za Serikali za kuwaajiri wengine.

MHE. MARTHA M. MLATA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kwa wasomi wetu kupata ajira Serikalini ni kutokana na ufinyu wa nafasi za kazi na wasomi hawa walio wengi wanakuwa wamepata mikopo kutoka kwenye Bodi ya Mikopo wanatakiwa warudishe.

Je, Waziri anaweza kuungana na mimi kwamba Wizara itumie Baraza la Uwezeshaji ambalo lilanzishwa mwaka 2005 ili kuwasaidia hawa vijana waweze kujiajiri? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, wazo lake ni zuri tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpango ulio Uganda ni sawa na ule ulio *Egypt*, (Misri) na kwa kuwa swali la msingi linahusu wanafunzi wanaomaliza Vyuo Vikuu na Waziri amethibitisha hapa kwamba juhudi zimeanza kutekelezeka.

Sasa tunataka atuambie. Je, mpaka sasa tangu mpango huu anaoueleza umeanza ni wanafunzi wangapi wa vyuo vikuu waliosaidiwa kujiajiri na ni katika sekta zipi?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa swali lake linahitaji takwimu, tutamwandalia ili tumpe. Lakini nina hakika takwimu hizo zipo na wameshapatikana watu ambao wameajiriwa kwa mpango huo niliousema.

Na. 144

Fedha za Mikopo kwa Wajasiriamali

MHE. MARIA I. HEWA (K.n.y. JAMES P. MUSALIKA) aliuliza:-

Kwa kipindi cha miaka minne sasa Serikali imekuwa ikiahidi kuwakopesha kutoka Mfuko wa Rais wajasiriamali wa Jimbo la Nyang'hwale ambao hawakupata mkopo huo kwa awamu zote mbili.

Je, Serikali inawaambia nini wajasiriamali hao katika kipindi hiki kifupi kilichobaki?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA
aliibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa James Philipo Musalika kwa namna anavyofuatilia mambo yanayohusu maendeleo ya wananchi katika jimbo lake, ikiwa ni pamoja na kuuliza maswali ya mara kwa mara yanayohusu mikopo kwa wajasiriamali wa Nyang'hwale. Wananchi wa Nyang'hwale kwa kweli lazima wamshukuru Mbunge wao. Katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge wakati nikijibu swali lake Na. 45 nilitoa ufanuzi juu ya utaratibu unaotumika wa kutoa mikopo kwa wananchi, maarufu kama mabiloni ya J.K. Mwongozo wa utoaji wa mikopo kwa wananchi ulielekeza fedha zilizobaki kutolewa katika Wilaya 21 zilizokosa kabisa mikopo na zile ambazo zilipata mikopo chini ya kiwango katika awamu ya kwanza. Utaratibu haukuwa kutoa mikopo kwa Majimbo ya Uchaguzi, bali kwa Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kigezo hicho Wilaya ya Geita haikustahili kupata fedha awamu ya pili, kwani kama Wilaya, Geita ilipata zaidi ya Shs. 200,000,000/= katika awamu ya kwanza. Kwa sasa njia iliyobaki kwa wajasiriamali au *SACCOS* zilizokosa zilizokoa awamu ya kwanza na ya pili ni kusubiri waliokopa awali wakirudisha mikopo yao, hawa waliokosa watapata fursa ya kukopeshwa na asasi hizo za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ya jibu langu la awali niliezea kuwa Benki Kuu walifanya mchakato wa kupata Benki/Asasi zinazoweza kuendelea kutoa mikopo katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya Asasi hizo Benki ya *CRDB* ilikubali kuendelea kutoa mikopo hii katika Wilaya mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Geita.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Nyang'hwale kuwa mpango huu ni endelevu, hivyo vikundi au *SACCOS* waliotimiza masharti lakini hawakufanikiwa katika awamu ya kwanza na ya pili kuwa *CRDB* Wilayani Geita watakuwa na fursa nzuri kuwafikia waombaji wengi zaidi baada ya wale waliopata awali kurejesha mikopo yao.

MHE. MARIA I. HEWA: Namshukuru sana Waziri kwa majibu aliyyoatoa na kwa kumpongeza Mheshimiwa huyo na Wananyang'hwale wamesikia. Nina swali dogo tu la nyongeza. Je, kwa vile sasa umesema wanapata hizi pesa kwa awamu. Je, unaahidi sasa kwamba na Nyang'hwale inaweza ikawemo kwa sababu umesema zinatoka kwa Wilaya na Nyang'hwale sasa ni Wilaya. (*Makofi*)

Je, unaahidi sasa kwamba kwa kigezo hicho Nyang'hwale itakuwemo?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:
Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu hizi mbili zilizopita mpango ni huo nilioueleza kwamba Wananyang'hwale wasubiri labda fedha zilizokopeshwa. Fedha hizo zikirudi *CRDB* basi na *SACCOS* zijiandaye vizuri ziweze kukopeshwa.

Lakini kama kutakuwa na awamu nyingine na hii sasa imekuwa Wilaya, kama Mheshimiwa Rais wetu atakuwa na nia nyingine ya kutoa fedha nyingine za JK katika kipindi kijacho, basi Nyang'hwale kama Wilaya itakuwa nafasi sasa mzuri zaidi.

MHE. ESTHERINA J. KILASI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa mpango huu wa pesa maarufu kwa jina la mabilioni ya JK kwa Wilaya ambazo zimeanza kupewa hiyo mikopo imeona haifakii walengwa hasa kwa kupitia *SACCOS* na kwa kupitia *NMB*.

Je, kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi na kwa Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiomba mara nyingi kwamba chombo pekee au muhimu sana ambacho kingeweza kusaidia wananchi ni aidha kupitia *SIDO* au kupitia mfuko huu *PTF* au *Presidential Trust Fund* ambao unawafikia hata wale walengwa wa chini. Kwa nini isitumie vyombo viwili ili wote tuweze kunufaika au wajasiriamali waweze kunufaika?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu utaratibu huu tuliutumia kwa kupitia Benki Kuu na taratibu za Benki Kuu ni lazima zipitie kwenye Asasi za kibenki ambazo zinaweza zikadhibitiwa vizuri na Benki Kuu kwa mujibu wa taratibu zao na sheria zao. Kwa hiyo, imekuwa vigumu kutoa kwenye taasisi zingine ambazo hazina ule mfumo wa kuweza kuwa *regulated* na Benki Kuu.

Lakini kwa sababu hiki kimekuwa ni kilio, Serikali katika awamu zingine kama itatokea basi mimi nadhani tunaweza tukafikiria kwa utaratibu tofauti. Lakini kwa kupitia Benki Kuu kwa kweli taratibu ndiyo hizo hizo zilizokuwepo katika awamu hii.

Mahitaji Ya Umeme - Mtwara

MHE. REYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa, utafiti wa matumizi ya gesi ya *Mnazi Bay – Mtwara*, unakaribia kukamilika kwa kuonesha kwamba kuna gesi yenye ujazo wa 2.6 trillioni *cu.ft (tcf)* inaweza kutumika kwa matumizi ya kawaida:-

(a) Je, Serikali inaona ugumu gani kutoa vibali ili miradi mikubwa kama ule wa kusambaza umeme katika Gridi ya Taifa, ili kutumia *MW 300* zinazoweza kusalishwa Mtwara na kuondoa kabisa matatizo ya umeme nchini na kuanzisha *Compressed Natural Gas?*

(b) Je, kwa kucheleweshwa matumizi hayo, Serikali haioni kuwa inadumaza maendeleo ya Uwanda wa Kusini?

(c) Je, ni lini kutakuwa na mpango maalum wa kuanzisha viwanda Mtwara, ili kutumia vyanzo vilivyopo vya nishati na Madini, yaliyopo kwa kutumia Bandari ya Mtwara?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini na kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Raynald Alphonse Mrope, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2008/2009, Wizara yangu ilifanya uchambuzi wa miradi mbalimbali inayoweza kutekelezwa kwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay*. Baada ya zoezi hilo miradi iliyopewa kipaumbele ilikuwa ni ule wa kiwanda cha mbolea, kiwanda cha saruji na umeme wa *Mega Watt 300*. Mradi wa kuuza gesi nje (*CNG*) ulipewa kipaumbele cha mwisho ikiwa na maana kwamba mradi huo utatekelezwa baada ya miradi nilioitaja awali ya kipaumbele kutekelezwa. Nia hasa ya kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba tunakidhi mahitaji ya Taifa kwanza. Miradi iliyopendekezwa ili iweze kutekelezwa inahitaji maandalizi; mchakato wa kuwapata wawekezaji katika kiwanda cha mbolea na saruji unaendelea. Wizara yangu imeunda Kamati ya wataalam kwa ajili ya kuandaa mradi wa kuzalisha umeme wa *MW 300*. Aidha, Wizara yangu imepokea mawasiliano ya wadau mbalimbali wenye nia ya kuendeleza mradi wa matumizi ya *CNG* kwa kutumia gesi ya asili ya Mtwara na gesi itokayo maeneo mengine. Baada ya kutoa maelezo hayo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni ugumu wowote kutoa vibali ili miradi mikubwa itekelezwe. Tatizo lililopo ni kwamba miradi mikubwa inahitaji taratibu nyingi za maandalizi inayochukua muda mrefu. Pia kwa upande wa Serikali, ni lazima kufanya tathmini za makini ili kubaini maslahi mapana ya Taifa. (*Makofî*)

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuchelewa kutekelezwa kwa miradi kunarudisha nyuma maendeleo, sio kwa mikoa ya Kusini tu bali, kwa Taifa zima. Kama nilivyosema hapo awali kuwa miradi mikubwa inapitia taratibu pana na za kina za tathmini, ili kujiridhisha kwa umakini kabla ya kuridhia miradi hii. Hata hivyo, ni lazima nikubali pia kwamba suala la kupitia na kuridhia miradi yote ni vyema ikatafutiwa taratibu zenye ufanisi zaidi ili kutokuchelewesha maendeleo ya miradi hiyo mikubwa na uwekezaji.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina jukumu la kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji, ili wawekezaji binafsi kutoka nje na ndani ya nchi waweze kutumia fursa zilizopo. Serikali pia inaratibu, inasimamia na kuhamasisha uwekezaji kutoka sekta binafsi kwa kupitia njia ya ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi, PPP. Kwa hiyo, Serikali imekuwa ikishiriki kwa asilimia chache kuwekeza pale ambapo imethibitika kuna uwezekano mkubwa wa uhakika wa kupata faida. Hivyo, Serikali imetoea wito kwa wawekezaji binafsi kutoka nje na ndani ya nchi yetu kutumia fursa zilizopo Mtwara, kama bandari, gesi na umeme, kuanzisha viwanda mbalimbali mkoani humo. Naomba niwahakikishie wote kwamba Wizara yangu itafanya jitihada ya makusudi ili kuboresha ufanisi na kiwango cha kutoa huduma na utekelezaji wa majukumu yetu katika kufanikisha miradi yote iliyo chini ya Wizara yangu ikiwemo miradi inayotarajia kuendelezwa Mtwara na maeneo yote ya Kusini.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

NAIBU SPIKA: Yawe mafupi eeh!

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha kwamba umeme upo wa masaa 24 pale Masasi; hongera sana *Boys To Men*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

(a)Waziri atueleze ni lini kazi ya kusambaza umeme katika vijiji vinavyoambaa na mradi huu itaanza? Na hasa katika vijiji vya Nkungu, Nkwera, Chipite, Nanganga, Mumburu, Nangoo, Lipitu mpaka Masasi?

(b)Je, Waziri anaweza kuthibitisha kwa kauli kwamba gharama za kuunganisha umeme katika maeneo haya, itakuwa ni shilingi 60,000/= mpaka 80,000/= na sio 475,000/= zinazotozwa na TANESCO hivi sasa hata kama wao hawatarudia kuiongoza Wizara ile hapo baadaye?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mzee Mrope kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa pongezi zilizotufikia. Huu mradi wa *Mtwara Energy Project*, (MEP), ambao ni mradi wa kuzalisha umeme unaotokana na gesi asilia, ya kupeleka umeme mikoa ya Lindi na Mtwara. Lengo lake ndio hilo la kufikisha umeme kwenye maeneo mengi; ukishatoka pale Mtwara Mjini, kwenda mpaka Masasi. Ndiyo maana juzi wakati tunajibu swalii la Mheshimiwa Mkapa, tulisema kwamba tunatarajia umeme ufile mpaka Mangaka. Ili kuondoa tatizo la umeme wa jenereta tunataka ufile mpaka Tunduru, ili maeneo yale yote yawe na ka-*mini grid* fulani kanakojitegemea. Uwezekano wa sasa hivi ni kwamba panazalishwa kama *Megawatt* 12 lakini nafasi imewekwa ili iweze kufika hata *Megawatt* 30, kwa mradi mdogo wa umeme wa Mtwara na Lindi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mzee Mrope, kwamba lengo ni kufikisha umeme kote huko, Mkungu, Mkwera, Nangoo mpaka Masasi. Kwa hiyo, naomba tuvumiliane ili utekelezaji wa mradi huu, kwa sasa tumeshafika Masasi, tunatarajia tupidie kwa awamu ya pili huku chini kwa kupitia Tandahimba, Newala mpaka kutokea tena Masasi, halafu twende mpaka Nachingwea na Mangaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la gharama ninaomba anipe muda nilifanyie utafiti zaidi. Kwa sababu ili kuwezesha upatikanaji wa umeme kwa gharama nafuu, pana kitu kinaitwa *Tariff Equalization Fund*, ambayo Serikali imewekeza mapesa mengi tu, nadhani ni karibu bilioni 14 na kwa mwaka huu wa Bajeti nadhani tunawekeza hela nyingine tena ili kuwezesha upatikanaji wa umeme na uunganishaji kwa gharama nafuu. Kwa hiyo, sasa tunajua kabisa kwamba mradi huu utatoka *TANESCO* utakwenda Umoja *Light* na makubaliano yaliyokuwepo hapo yanatarajia yawezeshe kuunganisha umeme kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara na wananchi wa Mtwara, waelewe kwamba tunalifanyia kazi suala hili ili kuunganisha umeme katika mfumo wa ki-*min grid* hicho uwe na gharama nafuu zaidi.

Na. 146

Taasisi Zinazoratibu Mchezo wa Ndondi

MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MHE. LUCY T. MAYENGA) aliuliza:-

Kwa kuwa, mchezo wa ndondi ni moja kati ya michezo yenyeye kuipa heshima nchi yetu na kuitangaza:-

Je, ni taasisi zipi zinazosimamia shughuli za kuratibu mchezo huo hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lucy Thomas Mayengaa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kufuatilia kwa karibu masuala ya michezo na hivyo kutaka kujua vyombo vinavyosimamia michezo mbalimbali hapa nchini. Zipo taasisi mbili zinazosimamia shughuli za kuratibu mchezo wa Ndondi ambazo ni Chama cha Ndondi za Ridhaa (*BFT*) na Shirikisho la Ngumi za Kulipwa (*PST*).

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu makubwa ya vyama hivi viwili ni kuratibu na kusimamia michezo na mashindano mbalimbali yanayopangwa kufanyika ndani na nje ya nchi. Aidha, Vyama hivi ambavyo pia vina jukumu la kuendeleza mchezo wa ndondi, husimamiwa na kupata ushauri kutoka Idara ya Maendeleo ya Michezo na Baraza la Michezo Nchini, (*BMT*).

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Shirikisho la Ngumi za Ridhaa Tanzania – *BFT*, lilifungiwa na Shirikisho la Kimataifa la Ndondi (*IFB*), baada ya baadhi ya Viongozi wake kukumbwa na kashfa ya madawa ya kulevy. Je, ni nini hatma ya *BFT* hadi sasa, hasa ikizingatiwa kwamba mchezo wa ndondi umekuwa ukiiletea sifa nchi yetu kwa kutupatia medali nyingi?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kumjibu Mheshimiwa Vita Kawawa, swalii lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, alichozungumza ni kweli na kwanza nimpongeze kwa kutambua kwamba mchezo wa ngumi nchini, umetuletea medali nyingi sana. Kama kihistoria utakumbuka wakati wa akina Taison Simba, akina Kinyogoli, katika Olimpiki tulikuwa tunapata medali nyingi. Lakini kama alivyosema hivi karibuni, kumetokea tatizo, viongozi wa mchezo huu wakati wanakwenda Mauritius walikumbwa na madawa yakulevy na wakashikwa na hivi ninavyozungumza bado wako ndani na *Interpol* inafanya shughuli na kesi hiyo inaendelea. Lakini sisi kwa kuona kwamba mchezo huo ni muhimu sana Serikali imejitahidi, kwa sababu kesi iko Mahakamani, kuomba chama cha ngumi cha dunia kuturudishia uanachama Tanzania. Chama cha Ngumi Duniani kimekubali, sasa hivi tumesharudishiwa uanachama. Tayari Serikali ina timu ya ngumi na imeajiri makocha kutoka Cuba, tayari kwa maandalizi ya Olimpiki yatakayofanyika kule India na Mashindano ya Jumuiya ya Madola yatakayofanyika Uingereza. Sasa hivi timu yetu na chama hiki kimerudishiwa heshima yake; kesi inaendelea na sisi huku tunaendelea kuuendeleza mchezo huu. (*Makofi*)

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mchezo wa ndondi huchezwa na rika zote kwa wanaume na wanawake. Na kwa kuwa, nchi zilizoendelea na michezo huu, mfano Cuba ambako nimesomea mimi michezo, mchezo huu huchezwa na wakubwa tu na sio watoto. Na kwa kuwa, hapa Tanzania katika maeneo niliyozunguka, kuna maeneo ambayo mchezo huu hufundishwa watoto, ambapo mimi naona ni kinyume cha sheria kwa sababu, mchezo huu ni wa hatari. Je, Mheshimiwa Waziri, anasemaje? Hii ni sheria katika michezo yetu au ni maamuzi tu ya watu kuwafundisha watoto bila kujua kwamba mchezo huu una athari gani? (*Makofi*).

NAIBU WAZIRIWA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kumjibu mwanamichezo mwenzangu, Ndugu yangu Mheshimiwa Mwanawetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikipongeze Chama cha Ndondi Tanzania kwa kuwa na Rais mwanamke, ambaye anaitwa Joan Ninja. Ni chama pekee ambacho Mwenyekiti au Rais wa Chama cha Ndondi Tanzania ni mwanamke na anafanya kazi nzuri sana. Lakini kimsingi alichosema ni kwamba kiutaratibu ndondi au mchezo wa aina yoyote unafundishwa katika ngazi ya utoto.

Hata siku moja huwezi ukamfundisha mtu aliyekomaa mchezo, kwa sababu ataumia tu. Kwa hiyo, kiutaalam unaanza katika ngazi ya utoro na mashindano haya yako katika umri mdogo pia na ndio maana kuna *weight* mbalimbali. Kwa hiyo utalaam unasema tuanze kufundishana michezo katika umri mdogo. Na ndio sheria na ndio utaratibu na ndio kitu ambacho kinahitajika. (*Makofit*).

Na. 147

Hitaji la Kituo cha Polisi Katika Tarafa ya Bashnet

MHE. DAMAS P. NAKEI aliuliza:-

Kwa kuwa, Ukanda wote wa tarafa ya Bashnet kwa muda mrefu hauna kituo cha Polisi, ikizingatiwa Bashnet na Dareda ni miji inayoibuka kwa kasi kubwa:-

Je, ni lini Serikali itaipatia tarafa ya Bashnet Kituo cha Polisi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Paschal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejiwekea mpango wa kujenga Vituo Vya Polisi katika Kata zote hapa nchini ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Mpango huu unatekelezwa kwa awamu kulingana na mafungu yanayotengwa na Serikali kwenye Bajeti ya Jeshi la Polisi. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika mpango huo Serikali imepanga kujenga Kituo Cha Polisi katika Tarafa ya Bashnet katika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kwa kuwa, muda tutakaopata hicho Kituo cha Polisi Bashnet ni mrefu, takribani miaka miwili na kwamba; kwa kuwa, suala la ulinzi wa amani na uhalifu hausubiri muda wote huo. Je, Serikali ipo tayari kufungua Kituo Kidogo cha Polisi, pale Bashnet, kwa kutumia majengo ya Ofisi ya Katibu Tarafa? Tuna Kituo cha Polisi Galapo, lakini askari pale Galapo, huondoka kwenye kituo hicho saa za jioni na kurudi Babati Mjini na kuacha Kituo wazi. Je, huo ni utaratibu gani wa kuacha kituo wazi halafu kesho yake asubuhi ndipo warudi kwenye eneo la kazi na usiku wote unakuwa umeachwa kwa watu wengine ambao ni wahalifu wanaoweza kutumia nafasi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nakei, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, analolisema kuhusu suala la kwanza kwamba Serikali imeamua kuweka kituo lakini itakuwa ni baada ya miaka miwili; hili ni suala ambalo tumekuwa tunalizungumzia mara kwa mara. Mheshimiwa Waziri, amelizungumzia katika Bajeti yake, nimelijibu mara nyingi hapa Bungeni, nikisema kwamba Serikali azma yake ni kuweka vituo pote nchini na kuhakikisha kwamba usalama wa raia na mali zao viko sawasawa. Nikasema na tumekuwa tunasema, azma hiyo inaendana na uwezo wa Serikali. Sasa itakuwa ni vibaya sana tukimwambia kwamba hiki kituo kinaweza kikafanyika mara moja kwa sababu uwezo huo haupo lakini azma hiyo ipo na mipangilio ipo na ndio maana tunesema kwamba hicho kituo kipo kitawekwa. Lakini kuhusu hali ya ulinzi na usalama itaendelea kwa sababu doria zinafanyika na ulinzi katika maeneo haya bado unafanyika kutoka katika vituo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hilo swalilake la pili, nataka nimhakikishie kwamba sisi kama Wizara na Polisi, suala la usalama tumekuwa tunalipa kipaumbele. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba hata tukitoka hapa tunaweza tukazungumza zaidi kuona ni njia gani tunaweza tukasaidiana ili kuona kwamba mambo yanakwenda sawa sawa.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Jiji la Tanga kuna baadhi ya Kata, wananchi walijitolea kujenga vituo vyapoli. Na kwa kuwa, vituo hivi sasa hivi vimefungwa na nguvu kazi ya wananchi inaonekana imepotea. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu kuvifunga vituo hivi? (*Makofi*).

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba tunayo taarifa kwamba vituo pahala pengi katika Tanzania, vinajengwa kwa nguvu za wananchi na Serikali imekuwa ikifanya yale ambayo yanawezekana ambayo yamewashinda wananchi. Lakini hii taarifa anayoisema Mheshimiwa Mbunge Nuru, kwamba kuna vituo ambavyo vimejengwa lakini vimefungwa, kwa kweli ndio mara ya kwanza mimi ninaipokea na ningombaa kama ikiwezekana tupate taarifa zaidi ili tuweze kujua vimefungwa kwa sababu gani na

kama kuna haja kwa kweli ya kuchukua hatua, tutizame ni hatua gani tunaweza tukazichukua. (*Makofi*)

Na. 148

Upatikanaji wa Maji Kupitia Fedha za Benki ya Dunia

MHE. PASCAL C. DEGERA aliuliza:-

Wilaya ya Kondoa ni moja kati ya Wilaya zilizopangiwa kupatiwa maji kupitia fedha za Mradi wa Benki ya Dunia:-

Je, kwa nini mradi huo umechelewa kuanza na sasa utanza kutekelezwa lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA(K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Julai, 2007 Wizara yangu kwa kushirikiana na *TAMISEMI*, ilianza utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini, kwa kutekeleza miradi inayoleta matokeo ya haraka wakati Halmashauri zinaendelea kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa vijiji kumi katika kila Halmashauri. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hilo swali lake la pili, nataka nimuhakikishie kwamba sisi kama Wizara na Polisi, suala la usalama tumekuwa tunalipa kipaumbele. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba hata tukitoka hapa tunaweza tukazungumza zaidi kuona ni njia gani tunaweza tukasaidiana ili kuona kwamba mambo yanakwenda sawasawa. kukamilisha maandalizi ya utekelezaji mradi wa vijiji 10 katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, utekelezaji wa mradi katika vijiji kumi ulianza lakini uligubikwa na matatizo mawili; tatizo moja ni uzoefu mdogo wa kuanda mchakato wa manunuzi katika ngazi ya halmashauri na hii ni kwa sababu wataalam wengi katika halmashauri za wilaya walikuwa hawana uzoefu wa kuanda mchakato wa manunuzi wa wataalam washauri kutokana na vigezo vilivyowekwa na Benki ya Dunia, hivyo kusababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa programu.

Lingine ni kwamba, nchi yetu ina uhaba wa wataalam washauri na hii imeleta usumbufu kwa baadhi ya halmashauri za wilaya kukosa idadi ya wataalam washauri wanaotakiwa kutokana na masharti ya manunuzi ya kimataifa yaliyowekwa na Benki ya Dunia. Hii imesababisha baadhi ya wilaya kurudia mchakato wa manunuzi ya wataalam wa utekelezaji wa programu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mrefu ulitumika katika maandalizi na mchakato wa kupata wataalam washauri, nafurahi kuriarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Halmashauri 123 kati ya halmashauri 132 sasa zimepata ridhaa kutoka Benki ya Dunia kusaini mikaba kati yao na wataalam washauri. Halmashauri zote 123 tayari zimeajiri wataalam washauri nao wameanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwezi Septemba, 2009, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa iliajiri mtaalam mshauri *Masochi Water Resources Exploration Company Ltd.*, anaendelea na kazi katika vijiji 27.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipoanza kutekeleza miradi inayoweza kuleta matokeo ya haraka, Halmashauri ya Kondoa ilichagua kutekeleza Miradi ya Chokolo, Mrijo Sekondari, Bukulu Sekondari, Bus Sekondari, Farkwa Sekondari, Keikei, Mirambo, Kiteo na Mitati. Halmashauri ilipewa shilingi 115,650,000 kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumefikia hatua ya utekelezaji, namwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wawe na subira kwa kuwa tunatarajia kuendelea na ujenzi wa miradi unaofanyiwa usanifu sasa katika mwaka 2010/2011.

Namshukuru sana Mheshimiwa Degera kwa ufuatiliaji wake wa karibu na ninamhakikisha yeye na Wananchi wa Kondoa kwamba, tatizo lao la maji sasa litapata ufumbuzi.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu la msingi Naibu Waziri amekiri kwamba kuna upungufu wa wataalam; na kwa kuwa katika Wilaya ya Kondoa utafiti ulishafanyika lakini zabuni ama nyaraka za zabuni zimeshindwa kuandaliwa kutokana na upungufu wa wataalam. Je, Wizara itakuwa tayari kumtuma mtaalam kuja kusaidia kuanda nyaraka za zabuni na kuzitangaza?

Kwa kuwa katika vijiji 27 alivyovitaja 17 vilikuwa vinahudumiwa na Mtaro wa Ntomoko na Mtaro wa Ntomoko sasa hivi umevurugika na wananchi wanapata shida sana ya maji; je, Wizara itakuwa tayari kusaidia angalau kufufua ule Mradi wa Ntomoko ili uweze kutoa huduma wakati wanasubiri utekelezaji wa miradi hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, labda tuweke rekodi vizuri, mimi nimetaja kampuni hapa ambayo inaitwa *Masochi Water Resource Exploration Company Limited* ambayo sasa hivi ndiyo imechukuliwa kama kampuni ambayo ni mshauri. Ukitsemu kampuni mshauri maana yake unazungumzia jicho la Halmashauri ya Kondoa kuititia maji kuhusu namna itakavyotekelawa *project* hii. Sasa Mheshimiwa Degera najua *concerns* zake ni kwamba, yeye anaona kazi hii haiendi vizuri. Sasa kwa mfano unamchukua mtaalam kutoka TAMISEMI unamwambia aende kule, anakwenda kufanya nini kwa sababu tunavyozungumza hapa tayari kazi hii sasa imeshafikia hatua ya kwamba sasa wako katika mchakato wa *ku-short list* na kila kitu ili wajue ni mkandarasi gani ambaye

atapewa kazi hii ambayo imezungumzwa hapa. Kwa hiyo, napata shida hapa kusema sawa tutampeleka mtaalam, sana sana nitakachofanya nitawasiliana na Hal mashauri ya Wilaya ya Kondoa na wakati huo huo na Waziri anayehusika na jambo hili kuwaambia jamani Mheshimiwa Degera anataka hili lipelekwe kwa haraka kabla ya mwezi Oktoba liwe limemalizika pale.

Ninataka nimthibitishie kuwa, taratibu zote zimekamilika, kitu kinachotakiwa ni kumpata *the lowest bidder* ambaye ameangaliwa ndiyo atangazwe na vigezo vyote vya World Bank tunavyo. Sasa kuhusu hili la Ntomoko ambalo analizungumza hapa, najua kwamba, Ntomoko ni shirika moja ambalo limesaidia sana katika kupatikana kwa maji. Kwa taarifa yako, nilifanya ziara katika Mkao wa Dodoma, kwa hiyo, mradi naufahamu. Ninajua kwamba, hiki ni kitu kingine lakini kama Ntomoko inaonekana itasaidia katika jambo hili, sina tatizo kabisa kushauriana nao ili tuone jinsi watakavyosaidia. Miradi ile mingine yote vijiji vile kumi nataka nithibitishe hapa kwamba, tayari sasa kazi hiyo imeshakamilika.

NAIBU SPIKA: Asante muda muda sasa naenda Wizara ya Katiba na Sheria.

Na. 149

Hitaji la Majengo ya Mahakama na Nyumba za Mahakimu - Rufiji

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Rufiji ni kubwa sana lakini haina majengo ya mahakama na nyumba za mahakimu:-

- (a) Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya mahakama na nyumba za mahakimu?
- (b) Je, Serikali imesaidia mahakimu wangapi kutoka Rufiji katika programu yake ya kuijiendeleza (*Continuing Education*)?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO
(K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mahakama ya Tanzania imekwishaanzisha miradi minge ya ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya na Mwanzo pamoja na nyumba za kuishi mahakimu kwenye wilaya mbalimbali hapa nchini; siyo vyema kuanzisha miradi minge mipya kabla hii ya zamani haijamilika. Hivyo basi, ujenzi wa mahakama na nyumba za mahakimu Wilaya Rufiji utapangwa katika awamu zijazo baada ya Serikali kukamilisha ujenzi unaoendelea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rufiji ina jumla ya mahakimu saba wa mahakama za mwanzo na hakimu wa wilaya mmoja, hakuna upungufu wa mahakimu katika mahakama ya wilaya na hii ni kutockana na takwimu za mashauri yaliyopo. Lakini kuna uhaba wa mahakimu wa mahakama za mwanzo watatu katika mahakama 12 zilizopo. Hata hivyo, tunataraji kuziba pengo hilo hivi karibuni baada ya kuajiri mahakimu wa mahakama za mwanzo 100 katika mwaka huu wa fedha.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesaidia mahakimu wa mahakama za mwanzo kadhaa kutoka Rufiji katika programu ya kuijendezea, yaani *continuing education*. Ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa kipindi hiki wapo mahakimu watatu ambao wanasona katika vyuo vikuu mbalimbali hapa nchini ambao wanatoka katika Wilaya ya Rufiji.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Ninaomba anisaidie; nimeuliza swali la msingi ni lingi jibu ni kwamba tuna programu itaisha lini ili na sisi watu wa Rufiji tuwe na imani kwamba tutapata hayo majengo?

(ii) Wakati huu wote kwa kukosa majengo ya mahakama, nyumba za kuishi mahakimu na ofisi za kufanya kazi, mahakimu hao wanafanya kazi katika hali ngumu. Je, Serikali itakubali kuwapa motisha maalum wakati wanapata matatizo haya mpaka watakapo jengewa nyumba, mahakama na ofisi zao?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali inafanya kazi zake kwa kufuatana na upatikanaji wa fedha. Ninaomba nimkumbushe jambo moja tu kwamba, hata Mwalimu Nyerere alisema kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo, hamuwezi kusema kwamba, kama una shilingi mbili utajenga kila mahali, tutajenga tofali moja moja tu mwisho wa siku hatuna nyumba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Prof. Mtulia Mwalimu wangu, nakuomba uamini tu kwamba, Serikali ina mpango wa kujenga. Kwa hiyo, awamu ambayo ipo sasa hivi itakapomalizika, ambayo inategemea pia na upatikanaji wa fedha, Serikali itaanza tena awamu nyingine ya kujenga nyumba za mahakimu pamoja na mahakama. Ninaomba nikwambie kwamba, *speed* ipo na inaendelea vizuri.

La pili, naomba nikueleze kwamba, Serikali imesikia wazo ulilolitoa kwamba, itoe motisha kwa hao mahakimu, sasa motisha yenye we itategemea pia na upatikanaji wa fedha. Ninaomba nikuhakikishie kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, itaangalia kama kuna uwezekano wa kuwapa motisha, maana yake kuangalia kama kuna uwezekano wa kuwatafutia nyumba kama hizo. Ninaomba nikwambie kwamba, kwa

sababu wewe umeonesha rai kwamba, kuna matatizo, mimi ninaamini kwamba, awamu inayofuata baada ya hii ya hivi sasa, Rufiji itapewa kipaumbele; naomba uwe na subira.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa muda umepita na maswali yenewe yamepita, sasa nitawatambulisha wageni.

Kwanza, tunao wageni wa Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ambao ni Dkt. Florens Turuka, yeye ndiyo Katibu Mkuu; yupo Dkt. Patrick Makungu, Naibu Katibu Mkuu; wapo Wakuu wa Taasisi na Vitengo mbalimbali vya Wizara; halafu wapo Wenyeviti wa Bodi ambao ni Mwenyekiti wa Bodi ya DIT, Prof. Idrisa Mshoro; pia yupo Mwenyekiti wa Bodi ya MIST, Eng. Wamanga; yupo Mwenyekiti wa TRCA, Jaji Chipeta; yupo Mwenyekiti wa Bodi ya TTCL, Prof. Mathew Luhanga; yupo Mwenyekiti wa Bodi ya COSTECH, Prof. Burton Mwamilia; yupo Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Posta, Dkt. Yamungu Kayandabila; yupo Mwenyekiti wa Watumiaji Huduma za Mawasiliano, Bi. Hawa Ngh'umbi; hawa wote sijui wamekosa nafasi au bado wanakuja.

Vile vile yupo Dkt. Naomi Katuzi, Mwenyekiti wa Bodi ya UCAF; Mkurugenzi Mkuu TCRA, Prof. Nkoma; Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Prof. Kondoro; Mkuu wa Taasisi ya Sayasni na Teknolojia Mbeya MIST, Prof. Msambichaka; Mkurugenzi Mkuu COSTECH, Dkt. Hassan Mshinda; Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TAC, Bwana Banzi; Posta Master Mkuu, Bwana Deus Mndeme; na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TTCL, Bwana Said A. Said; karibuni sana.

Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Prof. Msolla ambao ni Mzee Lazaro Nyamonga, ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Kilolo, nadhani wao wamekosa nafasi. Wapo pia watoto wa Mheshimiwa mabinti zake; Dkt. Ruth Msolla na Mrs. Joyce Sawala; ahsanteni sana, maana yake wewe unafuata njia za baba.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Maua Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ambao ni binti zake; Rahima na Salima Abdallah; karibuni sana kumsindikiza mama.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Damas Nakei, ambao ni watoto wake, naomba wote wasimame; nafikiri pia wamekosa nafasi, wengine wadogo kabisa; karibuni sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mkiwa Kimwaga, ambao ni Mwenyekiti wa CUF Wilaya ya Ilemela Mwanza, Maulid Simuyemba; Katibu wa CUF Wilaya ya Ilemela Mwanza, Ndugu Badru Abdallah; na Mnadhimu wa CUF Wilaya ya Ilemela Mwanza, Jamal Katima; asanteni mnakaribishwa sana.

Wapo wanafunzi 43 na walimu 8 kutoka Shule ya Msingi Buigiri Mission Dodoma. Hawa wanafunzi na walimu wako wapi wasimame; ahsanteni sana Buigiri ipo hapo hapa karibu.

Tuna akina mama 50 kutoka Kanisa la Assemblies of God Tanzania, wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Hao akina mama 50; ahsanteni sana, tunashukuru naona na watoto wadogo wapo tunafurahi.

Tuna wanafunzi 30 kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri Dodoma. Wanafunzi wa Jamhuri na Walimu naomba wasimame; ahsanteni sana, msome kwa bidii, ukombozi utatokana na elimu.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya BRC, BRC maana yake ni wale wanachama wa zoezi la kulenga shabaha. Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Shellukindo, anaona niwatangazie Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wachama wa Bunge Range Club kwamba, zoezi la kulenga shabaha ambalo awali lilipangwa kufanyika tarehe 4 Julai, limeahirishwa na badala yake litafanyika siku ya Jumatano tarehe 7 Julai, huko Makutupora JKT, kuanzia saa tatu asubuhi. Kwa hiyo, badala ya tarehe 4 Julai, litafanyika tarehe 7 na hiyo ni siku ya mapumziko ya Sikuu ya Sabasaba. Kwa hiyo, wale Wajumbe wa hiyo BRC wanakwenda Makutopora saa tatu asubuhi, najua mnaanza mnakokufahamu.

Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Raynald Mrope, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi kwamba, Siku ya Ijumaa, hiyo ni tarehe 2 Julai, saa moja asubuhi, kutakuwa na ndege kwenye uwanja wa ndege hapo Dodoma ya kuwapeleka Mtwara kushuhudia Uzinduzi wa Ukarabati wa Bandari ya Mtwara na Meli ya Kuchimbia Mafuta Ukanda wa Pwani ya Mtwara. Kwa hiyo, kuna mambo makubwa hapa; kuna uzinduzi wa ukarabati na hiyo shughuli nyingine ya kuchimba mafuta. Kwa hiyo, Wabunge wa Mtwara na Lindi, tarehe 2 Julai, saa moja asubuhi wawe kiwanja cha ndege kuna ndege, nadhani wameandaa ndege maalum na ninyi watu Mtwara muambizane kwa barua kwa sababu mpo wachache.

Baada ya kusema hivyo, tunaendelea na shughuli zingine.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 – Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga kuhusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liweze kupokea, kujadili na hatimaye kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa namna ya pekee kabisa, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuendelea kuwa na imani nami na kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi nyingi anazofanya kuhamasisha maendeleo katika Sekta mbalimbali za maendeleo hususan utunzaji wa mazingira. Aidha, nichukue nafasi hii, kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali Bungeni na kuhakikisha kwamba, utafiti unakuwa ni chachu ya Kilimo Kwanza; Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, kwa hotuba zao ambazo zimefafanua kwa kina utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Sera, Mipango na Mikakati ya Serikali na kutoa mwelekeo wa kazi za Serikali na kuhakikisha kwamba, utafiti unakuwa ni chachu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Kilolo na Uongozi wa Wilaya ya Kilolo kwa ujumla, kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo katika Jimbo letu. Aidha, kwa namna ya kipekee, namshukuru mke wangu Violet pamoja na familia yetu, kwa jinsi wanavyonipa moyo na ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na hotuba yangu, naomba uniruhusu kutumia fursa hii kukumbuka matukio mazito ya majonzi yaliyotokea tangu kumalizika kwa Mkutano wa 16 wa Bunge uliojadili Bajeti ya 2009/2010 mwezi Julai, 2009. Kwanza ni msiba wa kitaifa pale tulipompoteza Mzee wetu, Hayati Rashid Mfaume Kawawa, mionganoni mwa Waasisi wa Taifa hili, hapo tarehe 31 Disemba 2009. Tunaishukuru familia yake, kwa moyo wa subira waliouonesha kufuatia kifo hicho na tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu, azidi kuwapa Moyo wa ustahimilivu. Tukio la pili lilikuwa la kumpoteza Mbunge mwenzetu na mtetezi mahiri wa maslahi ya Wananchi wa Jimbo lake, Marehemu Mheshimiwa Sigfrid Seleman Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM). Pia, tunawaomba ndugu, jamaa na marafiki waendelee na moyo huo wa ustahimilivu waliokwisha kuuonesha wakati wa msiba huo. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuwapongeza Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene (CCM) na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu (CUF), kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuijunga na Bunge lako Tukufu. Aidha, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kuteuliwa kwao kunathibitisha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais kwa utendaji wao ulio makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi kilichopita na ambao wameweza kuandaa mpango wa mwaka wa fedha 2010/2011 na kuboresha hoja yangu ambayo naiwasilisha katika hotuba hii. Natoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na

Teknolojia; Dkt. Florens Martin Turuka, Katibu Mkuu; Dkt. Patrick James Makungu, Naibu Katibu Mkuu, Watendaji katika Wizara yangu pamoja na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara na Mashirika mbalimbali ya ndani na nje, kwa misaada na ushauri wao. Kwa namna ya pekee kabisa, natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kwa ushauri na maelekezo yao. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati (CHADEMA), ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara yangu na Waziri Kivuli wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii. Aidha, natoa shukrani kwa Wananchi wote wa Tanzania, kwa mchango wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ilikabidhiwa dhamana ya kuhakikisha kwamba, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, yaani TEKNOHAMA (*ICT*), Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, vinachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na jukumu hilo, Wizara hii imepewa dhamana ya kusimamia Taasisi, Mashirika, Tume na Kampuni ambazo zinachangia juhudzi za Wizara katika kuyafikia malengo na matarajio ya Wananchi. Taasisi zilizo chini ya Wizara hii ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*); Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*); Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (*NM-AIST*); Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (*TAEC*); Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*); Shirika la Posta Tanzania (*TPC*); Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*); Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*); na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali imetekeleza majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 – 2010, Sera ya Sayansi na Teknolojia, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA), Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu, na Sera ya Taifa ya Posta pamoja na maagizo mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2009/10, Wizara yangu ilitengewa jumla ya Shilingi 38,677,630,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 24,267,464,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, yaani mishahara na matumizi mengineyo na Shilingi 14,410,166,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, zikijumuisha fedha za ndani Shilingi 13,962,842,000 na fedha za nje kiasi cha Shilingi 447,324,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Juni, 2010 jumla ya Shilingi 23,640,128,955 zilikuwa zimetolewa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 97.4 ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Pia, kiasi cha Shilingi 10,705,032,073.54 zilikuwa zimetumika kwa upande wa fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 74.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA): Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, imetunga Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (*The Electronic and Postal Communication Act 2010*). Sheria hii, ambayo inawianisha Sheria ya Mawasiliano (1993), Sheria ya Utangazaji (1993) na Kanuni za Mawasiliano (2005), inalenga kuboresha usimamizi wa Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ili kuendana na mabadiliko katika Sekta ya Mawasiliano. Hii ni pamoja na kuboresha matumizi ya simu za viganjani, kusimamia mfumo mpya wa utangazaji wa digitali, kuanzisha rejestra ya utambuzi wa vifaa vya mawasiliano, kusimamia usajili wa simu za viganjani na kuhimiza na kuwezesha matumizi ya pamoja ya miundombinu ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ambao uliana rasmi mwezi Februari 2009. Kazi ya uchimbaji na ufukiasi wa nyaya za mawasiliano (*Optic Fiber Cable*) iliana tarehe 20 Julai, 2009 Mkoani Singida. Mkongo huu wa Taifa wa Mawasiliano utakapokamilika, utakuwa na urefu wa kilomita 10,674 ikijumuisha kilomita 7,000 zitakazojengwa na Serikali na kilomita 3,674 zilizojengwa na Mashirika ya TANESCO (2,050 km), TRL (854 km), TAZARA (200 km), TTCL (362 km) na SONGAS (208 km). Katika awamu ya kwanza, Mkongo umepita katika mikoa 16 ya Tanzania Bara (Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara na Kagera). Aidha, awamu hii inalenga kuufikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika maeneo ya mipaka na nchi jirani, yaani Mutukula (Mpakani na Uganda), Rusumo (Mpakani na Rwanda), Kabanga (Mpakani na Burundi), Kasumulo (Mpakani na Malawi), Namanga (Mpakani na Kenya), Tunduma (Mpakani na Zambia). Mkongo huu utaziunganisha nchi hizo za jirani na Mikongo ya Kimataifa ya Baharini ikiwemo SEACOM, UHURUNET, UMOJANET, EASSy na TEAMS.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi hivi sasa kazi ya uchimbaji na ufukiasi wa nyaya za mkongo umefanywa kwa kilometa 2,090 kati ya kilometa 2,305 (hii ni asilimia 91). Ufungaji wa mitambo katika Vituo vya Dar-es-Salaam, Morogoro, Kidatu, Ifakara, Kihansi, Iringa, Mtera, Dodoma, Manyoni, Singida, Katesh, Babati, Makuyuni, Arusha, Moshi, Same, Mkomazi, Hale, Tanga, Manga, Chalinze, Igunga, Nzega, Shinyanga, Mabuki, Mwanza, Geita, Biharamulo, Kabanga na Rusumo umekamilika na Mkongo uko tayari kwa matumizi. Aidha, ujenzi unaendelea katika maeneo yafuatayo; Iringa kuelekea Mbeya, Tunduma na Kasumulo; Arusha kuelekea Namanga na Mwanza kuelekea Musoma. Aidha, baadhi ya Ofisi za Serikali zilizoko Dar es Salaam na Dodoma tayari zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Ofisi hizo ni Ofisi ya Bunge (Dodoma); Chuo Kikuu cha Dodoma; Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia (Dar es Salaam na Dodoma). Vile vile, TTCL imeunganishwa kwenye Mkongo wa Baharini wa SEACOM na kupitia kwake, imeunganisha makampuni mengine yakiwemo SIMBANET, STARTEL, INFINITY, Celtel (T) Limited, CATSNET na SELCOM. Kuunganishwa

huko, kumewezesha mawasiliano ya simu na intaneti kuwa mazuri zaidi. Aidha, gharama za mawasiliano ya simu zimeendelea kupungua. Kwa mfano, gharama za kuunganisha simu za kimataifa zimepungua kutoka Sh. 1,775 mwaka 2000 na kufikia Sh. 467 mwishoni mwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya Mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano tayari imeanza. Awamu hii inahusisha maeneo yaliyobaki ya Tanzania Bara na Visiwani na kuhakikisha kuwa Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya zote yanaunganishwa na Mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa uunganishaji wa vyuo vikuu pamoja na vituo 83 vya utafiti kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaendelea. Maandalizi ya kuviunganisha vyuo na vituo vingine yanafanya kupitia mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia wa Science and Technology Higher Education Project.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na Ujenzi wa Kituo cha Huduma za TEKNOHAMA (*Centre of Excellence in ICT*) katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, ambapo tayari kompyuta zenye uwezo mkubwa wa ukokotoaji (*Super Computers*) zimebekwa. Ujenzi wa Kituo hiki unafanywa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya India. Kituo kitakapokamilika, kitaongeza uwezo wa nchi katika kufanya uchambuzi na ukokotoaji wa mahesabu unaohitaji uwezo mkubwa wa kompyuta (*complex computations*) kwa haraka zaidi. Kituo pia, kitatumika kutoa mafunzo na utafiti, tiba mtandao (*tele-medicine*) na elimu mtandao (*e-learning*). Ili kufikisha huduma hizi kwa jamii, Kituo hiki kitaunganishwa na vituo vingine 10 nchini katika majengo ya Shirika la Posta, Zanzibar na kwenye Mikoa ya Pwani (Kibaha na Bagamoyo), Arusha, Mwanza, Iringa, Mbeya, Morogoro, Dodoma na Mtwara. Tayari walimu tisa wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam wamekwishapata mafunzo ya miezi sita nchini India kujenga uwezo wa kuendesha Kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinapatikana hadi ngazi ya vijiji, Serikali imeendelea kuimarisha vituo vya mawasiliano vilivyopo na kuanzisha vituo vipyta. Idadi ya vituo vya mawasiliano imeongezeka kutoka vituo vinne mwaka 2008 hadi kufikia vituo tisa mwaka 2009. Hatua za ukamilishaji wa vituo vingine vitano zinaendelea na vitakamilika ifikapo Julai 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Access Fund*), uliana rasmi shughuli zake Julai 2009. Mfuko huu, ambao utaendeshwa kwa kushirikiana na sekta binafsi, utasaidia juhudhi za kufikisha mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara. Mambo mengine yatakayoshughulikiwa na Mfuko huu ni pamoja na kuimarisha huduma za simu za viganjani, kuongeza upatikanaji wa mawasiliano ya intaneti, kupeleka huduma za utangazaji kupitia radio za jamii (*community radios*) na kuongeza mtandao wa huduma za posta. Taratibu za uendeshwaji wa Mfuko huu zinakamilishwa ili Mfuko uanze kutoa ruzuku katika mwaka wa fedha ujao wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, imetoa leseni za mwingiliano (*converged licence*) kwa kampuni 14 za mawasiliano na hivyo kuongeza ushindani katika sekta ya mawasiliano. Idadi ya makampuni yanayotoa huduma za uunganishwaji wa simu za kimataifa (*International Gateways*) imeongezeka kutoka moja (TTCL) iliyokuwepo mwaka 2005 na kufikia sita hivi sasa. Makampuni hayo ni TTCL, Zantel, Telecom, MIC (T) Limited (Tigo), Celtel (T) Limited na Vodacom. Gharama za uunganishaji wa simu za kimataifa zinaendelea kupungua kutokana na ushindani uliojitekeza baina ya makampuni haya. Mamlaka ya Mawasiliano, kwa kuzingatia maelekezo ya Shirika la Umoja wa Kimataifa la Mawasiliano (*International Telecommunication Union - ITU*), imeanzisha mchakato wa kubadili mfumo wa zamani wa utangazaji wa analogia (*analogue*) kwenda kwenye mfumo wa kisasa wa dijitali (*digital*), yaani *Analogue to Digital Broadcasting*. ITU imepanga ukomo wa kufanya mabadiliko haya kuwa mwaka 2015. Tayari Makampuni matatu yameainishwa kutoa huduma katika mfumo huo mpya. Makampuni hayo ni StarMedia (T) Ltd na Agape Associates (T) Ltd ambayo tayari yameshapewa leseni husika na *Basic Transmission Ltd* ambayo iko katika mchakato wa kupata leseni. Vile vile, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetoa leseni 55 kwa makampuni binafsi kwa ajili ya huduma za Posta Kitaifa, Kimataifa na Kikanda. Hili ni ongezeko kubwa la watoa huduma hii ikilinganishwa na leseni 38 zilizokuwepo mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Kimataifa ya African Telecom People ya Ufaransa ambayo hushindanisha wasimamizi na watoa huduma za mawasiliano kimataifa, imeipatia tuzo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kuwa taasisi bora zaidi ya usimamizi wa masuala ya mawasiliano Barani Afrika kwa mwaka 2009. Pamoja na kuipongeza Mamlaka, ninaomba nitumie fursa hii, kuwashukuru Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka hii, watoa huduma za mawasiliano na Watanzania wote kwa ujumla, kwa kusimamia na kutekeleza vyema utoaji na utumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kufuata kanuni bora. Kupitia ushindi huu, ninaamini kuwa, Watanzania wameona jinsi taasisi yao ya kitaifa inavyofanya vizuri ikilinganishwa na taasisi za nchi nyingine Barani Afrika na kwamba, wataendelea kuipa ushirikiano wa karibu ili iweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa sayansi na teknolojia nchini, Serikali imeandaa na kuhuisha Sera zinazohusu sayansi na teknolojia na kuandaa mipango ya utekelezaji na ufuatiliaji wa Sera hizo. Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia imeridhiwa na serikali na utekelezaji wake umeanza. Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo iko katika ngazi za mwisho za maamuzi serikalini kuiwezesha ianze kutumika. Aidha, Serikali imeendelea pia kujenga, kuboresha na kupanua huduma katika taasisi mbalimbali zinazotekeleza majukumu mbalimbali ya maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela iliyopo Arusha. Uteuzi wa uongozi wa mpito wa Taasisi unaohusisha Makamu Mkuu wa Chuo na Naibu Makamu Wakuu wa Chuo wawili, umefanywa. Aidha, uandaaji wa mitaala, mapendelekezo ya muundo wa Taasisi (*Organization Structure*) na muundo wa utumishi (*Scheme of Service*) umefanywa. Taasisi inatarajia

kuajiri watumishi 108 mwaka huu wa fedha wakiwamo wanataaluma 45 na waendeshaji 63. Nafasi hizo zimekwishatangazwa. Aidha, ukarabati na ujenzi wa majengo katika eneo la Tengeru ambapo Taasisi itaanza kufanya shughuli zake, unatarajia kuanza mwezi Julai 2010 baada ya mchakato wa kumpata Mkandarasi kukamilika. Ukarabati na ujenzi huu unafanywa kupitia mkopo wa Shilingi Bilioni 38.7 kutoka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kupitia Kampuni ya *Pension Properties Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuziimarisha taasisi za sayansi na teknolojia zilizo chini ya Wizara ili ziweze kuongeza udahili unaohitajika katika kukidhi hitaji kubwa la wataalamu wenye ujuzi wa ufundi katika ngazi za kati za ufundi kwenye nyanja mbalimbali za sayansi na teknolojia. Hadi kufikia mwezi Oktoba 2009, Taasisi ya Teknolojia ya Dar-es-Salaam ilidahili jumla ya wanafunzi wapya 1,006. Katika kukabili ongezeko hili, Taasisi inaendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi (*Teaching Tower*). Aidha, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya iliongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 927 kwa mwaka wa masomo 2008/2009 na kufikia wanafunzi 1,242 mwaka wa masomo 2009/2010. Taasisi hii pia imeanzisha masomo ya shahada ya kwanza katika fani za mitambo, ujenzi, umeme, usanifu majengo, sayansi ya biashara na stashahada ya uhandisi wa kompyuta. Katika kukabiliana na ongezeko hili la wanafunzi, Taasisi imeendelea kuboresha miundombinu ya kitaaluma na ya huduma nyingine za msingi ikiwa ni pamoja na ukamilishwaji wa ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (*Tanzania Atomic Energy Commission*), imeendelea kusimamia matumizi salama ya mionzi. Aidha, Tume imesimamia miradi 9 ya kitaifa na miradi 30 ya kikanda inayohusisha matumizi mbalimbali ya nguvu za atomiki iliyofadhiliwa na Shirika la Nguvu za Atomiki la Kimataifa (IAEA). Tume imepima usalama wa mionzi kwa wafanyakazi (*personal dosimetry*) 1,180 katika vituo 309. Vile vile, Tume imekagua na kutathmini usalama wa mionzi katika vituo 106 kati ya vituo 150 vinavyotumia vifaa vya mionzi. Kati ya vituo vilivyokaguliwa, vituo 86 (81%) vilikidhi viwango vya usalama. Vituo 20 vilivyobaki vilipewa maelekezo ya kuboresha hali ya usalama. Pia, Tume imetoe leseni 174 (88.3 %) za kumiliki vyanzo vya mionzi kati ya waombaji 197 baada ya kukidhi viwango vya usalama. Aidha, Tume ilikusanya mabaki ya vyanzo vitano vya mionzi kutoka TANROADS na kufanya mabaki yote yaliyokusanywa na kuhifadhiwa na Tume hadi sasa kufikia 72.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, Tume ilikagua minara ya simu katika vituo 11 katika Mikoa ya Arusha na Manyara na kubaini kuwa viwango vya mionzi vilikuwa vya chini na visivyo kuwa na madhara kwa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha juu kabisa ambacho hakina madhara kwa binadamu kilichopendekezwa na *International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection* ni 1.0mW/cm^2 wakati viwango vilivyo kwenye minara ya simu ni 0.005mW/cm^2 . Aidha, katika kutekeleza majukumu yake ya ukaguzi, Tume ilikagua migodi mitano ya *Tanzanite One (T) Limited Mererani* (Manyara), Mradi wa Urani wa Mto Mkuru ulioko Namtumbo (Ruvuma), Mradi wa Urani wa Bahi (Dodoma), Mradi wa

Urani wa Manyoni (Singida) na kwenye machimbo ya mawe yanayotumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba Uchira (Moshi). Lengo la ukaguzi huu ilikuwa kuangalia hali ya usalama wa mionzi katika migodi hiyo ambapo ilionekana kutokuwepo athari za mionzi katika maeneo yote yaliyokaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa kutoa elimu na kujenga uwezo katika masuala ya mionzi hasa wakati huu ambapo nchi yetu imeonesha kuwa na rasilimali kubwa ya madini ya urani, Serikali kupitia Tume, kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, imeendesha semina kwa wafanyakazi 92 katika idara zenye vifaa vya X-Ray, viwandani, migodini na kwenye shughuli za ujenzi wa barabara. Aidha, Tume imeendesha semina nne kwa Viongozi wa Mikoa ya Ruvuma na Dodoma ambapo jumla ya viongozi 42 walishiriki semina hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwezo mkubwa wa Tume ikilinganishwa na nchi nyingine za jirani, Tume ilipewa jukumu la kuendesha warsha ya kikanda kuhusu uhakiki wa ubora wa vifaa vinavyotumika kupima mionzi. Warsha hiyo ilihuisha washiriki kutoka nchi 16 za Afrika (Madagascar, Mali, Ethiopia, Morocco, Sudan, DRC, Zambia, Tunisia, Ghana, Kenya, Uganda, Mauritius, Ivory Coast, Sierra Leone, Algeria na Tanzania).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imeendelea na juhudzi za kujenga uwezo wa watumishi wake. Jumla ya watumishi saba wanapata mafunzo katika ngazi mbalimbali; shahada ya kwanza (3), shahada ya uzamili (3) na shahada ya uzamivu (1). Mafunzo mengine yanaendelea kutolewa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki kupitia miradi mbalimbali inayoendeshwa na Tume kwa ushirikiano na Shirika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha utendaji wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), ambayo imeanza kutekeleza Mpango Mkakati wake wa mwaka 2009-2012 unaolenga kufanya mageuzi makubwa ya utendaji wa Tume. Aidha, Tume imeandaa miongozo mbalimbali kwa ajili ya kufanya tathmini ya ukuaji wa sayansi na teknolojia nchini ambapo imeweza kukusanya na kuchambua taarifa za awali kuhusu viashiria vya ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya sayansi na teknolojia nchini. Vile vile, Tume kwa kushirikiana na wadau imeandaa mpango (*framework*) wa namna ya kutumia fedha za utafiti zilizoahidiwa na kuanza kutolewa na Serikali kwa lengo la kufikia asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuandaa mpango wa matumizi ya fedha za utafiti, Tume pia imeimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha za Mfuko wa MTUSATE na kuweka kwenye mtandao. Vile vile, imekamilisha uandaaji wa masijala ya utafiti. Katika kupanua vyanzo vya fedha za utafiti, Tume imeanza kutoa taarifa ya fursa mbalimbali za fedha za utafiti zilizopo ndani na nje ya nchi na kuzitawanya kwa watafiti wote nchini. Tume imeendeleza ushirikiano na taasisi na mashirika mbalimbali katika kusimamia na kufadhili tafiti mbalimbali ikiwemo Serikali ya Sweden iliyochangia kiasi cha Sh. 321,200,413.54 katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Kupitia jitihada hizi, Serikali ya Sweden imekubali kuchangia jumla ya Sh. 4,811,000,000 katika kipindi cha

miaka mitano (2009 – 2013). Aidha, Shirika la Utafiti la Uholanzi limekubali kimsingi kuchangia katika MTUSATE.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 2005-2010 Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005-2010, ilielekeza Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kutekeleza majukumu muhimu yafuatayo:-

Mawasiliano: Kuboresha mtandao wa huduma za simu za mezani na za kiganjani hadi ngazi ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano ya simu nchini zinapanuliwa, Wizara, kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na wadau wengine, imeratibu shughuli mbalimbali zenye lengo la kuboresha mtandao wa huduma za simu za mezani na za kiganjani hadi ngazi ya vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa, makampuni 14 yamepewa leseni za kutoa huduma za mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya watumiaji wa simu za kiganjani kwa kigezo cha njia za simu (*line*) zinazotumika imefikia 18,207,390. Hili ni ongezeko la zaidi ya asilimia 400 ikilinganishwa na watumiaji 3,542,563 waliokuwepo mwaka 2005. Idadi ya simu za mezani hadi sasa ni 174,800 ikilinganishwa na 154,420 zilizokuwepo mwaka 2005. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 13.2. Ukuaji huu umepanua wigo wa mawasiliano ya simu na kuongeza huduma nyingine zinazoendana na matumizi ya simu hapa nchini. Huduma hizi ni pamoja na upatikanaji wa taarifa mbalimbali, huduma za intaneti, ulipaji wa ankara za simu, maji, umeme na huduma za kibenki (kutuma na kupokea fedha). Aidha, Mamlaka imeendelea kutekeleza agizo la Serikali la kusajili namba za simu kuanzia tarehe 1 Julai, 2009. Leo hii tarehe 30 Machi 2010, ilikuwa iwe ndiyo mwisho wa kusajili *line* na simu lakini kutokana na usikivu wa Serikali ya Awamu ya Nne ya CCM, imesikia kilio cha walio wengi ambao hawajasajili simu zao na *sim card* zao na hivyo kuongeza muda wa kusajili hadi Siku ya Alhamisi tarehe 15 Julai, 2010 na baada ya hapo simu zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa zitazimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Service Access Fund*), umeanza rasmi shughuli zake Julai 2009. Mfuko huu, kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, utasaidia juhudzi za kufikisha mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibashara. Pamoja na mambo mengine, Mfuko unategemewa kuchangia katika ujenzi wa minara, kupunguza gharama za kuunganisha mawasiliano ya simu na kuhamasisha matumizi ya simu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine katika huduma za simu nimekwishayataja ikiwa ni pamoja na idadi ya makampuni yanayotoa huduma za uunganishwaji wa simu za Kimataifa kuongezeka na gharama za uunganishaji kupungua kutokana na kuongezeka kwa ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Tanzania imeunganishwa na Mkongo wa Baharini wa SEACOM na EASSy ambapo inatarajiwa kwamba, baada ya kukamilika kwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaoendelea kujengwa, gharama za huduma za simu na intaneti zitapungua. Aidha, kasi ya mawasiliano ya intaneti itaongezeka sana. Vile vile, wananchi wataweza kupiga simu na kutumia huduma za intaneti mahali popote duniani na hivyo kurahisisha shughuli mbalimbali za maendeleo na za kukuza Uchumi wa Tanzania.

Kuhakikisha kuwa huduma za Posta nchini zinapanuliwa hadi vijijini ili kuongeza kasi ya usambazaji barua na vifurushi. Aidha, kuimarisha na kupanua mfumo mpya wa Mawasiliano unaotumia Teknolojia ya Kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta linaendesa ofisi 168 zinazotoa huduma kamili za posta ikiwa ni pamoja na utumaji na ulipaji wa fedha na usafirishaji wa nyaraka, vifurushi na vipeto vya haraka ndani na nje ya nchi. Vituo vya kutuma vifurushi vya haraka (*Expedited Mail Service*) vimeongezeka kutoka 121 mwaka 2005 hadi kufikia 148 mwaka 2009. Aidha, huduma za intaneti zinatolewa katika ofisi 23 za Posta nchini ikilinganishwa na Kituo kimoja kilichokuwepo mwaka 2000. Vile vile, kuna vituo vya posta 86 vinavyota huduma za kawaida za posta vinavyoendeshwa na wakala ikilinganishwa na vituo 84 vilivyokuwepo mwaka 2005. Vibali 2,878 vimetolewa kwa wafanyabiashara ili kuwa Wakala wa Shirika wa Makampuni ya kuuza stampu na shajala za posta. Sekta binafsi imepewa vibali na leseni za kutoa huduma za posta ili kupanua mtandao wa utoaji huduma, kuongeza ushindani na kuleta ubunifu katika kuendeleza shughuli za posta nchini, ambapo hadi kufikia Aprili 2010, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetoa leseni 55 kwa makampuni mbalimbali yanayotoa huduma za posta kitaifa na kimataifa ikilinganishwa na leseni 38 za huduma hizo kwa mwaka 2005.

Katika utoaji wa huduma za kifedha, kiasi cha Shilingi bilioni 41.5 za wateja zilipitia mtandao wa posta mwaka 2005 na kuongezeka kufikia Shilingi bilioni 46.4 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta linatekeleza Mradi wa *Counter Automation* unaotumia TEKNOHAMA na ambao umeunganisha Makao Makuu ya Shirika na Posta Kuu za Mikoa. Mradi wa *Counter Automation* umeliwezesha Shirika kutumia mtandao wa TEKNOHAMA katika kutuma fedha; kufuatilia mwenendo wa nyaraka, vifurushi na vipeto vya haraka kwa kutumia mtandao wa kompyuta (*Track and Trace*); na kupokea na kulipa fedha kwa niaba ya taasisi zingine kama vile Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) na kuuza hisa na kulipa magawio ya makampuni yaliyosajiliwa katika soko la mitaji. Aidha, Mradi wa *Counter Automation* umeboresha mawasiliano na mifumo ya habari ndani ya Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Anwani za Makazi na Simbo za Posta ulizinduliwa tarehe 18 Januari 2010 Mjini Arusha na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mfumo huu umeanza kwa majaribio katika Kata saba za Manispaa ya Arusha. Katika mwaka 2010/2011,

utekelezaji utafanywa Dodoma, Zanzibar na kumalizia sehemu zilizobaki Mkoani Arusha.

Kuongeza kasi ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kujenga uwezo wa kuratibu na kuimarisha mfumo huo na kuanzisha mfuko maalum wenye lengo la kupeleka huduma za simu na *internet* hadi vijijini. Katika jitihada za Serikali za kupeleka huduma za mawasiliano hadi vijijini, Serikali imeanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*) kama nilivyoeleza hapo awali. Madhumuni ya Mfuko huu ni kutoa ruzuku kwa wawekezaji watakaokuwa tayari kupeleka huduma za mawasiliano sehemu za vijijini na kwenye baadhi ya maeneo ya mjini yasiyokuwa na mvuto kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Mawasiliano Vijijini (*Telecentres*) vimeanzishwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Wasimamizi wa vituo hivyo wameelimishwa kuhusu umuhimu na matumizi endelevu ya vituo hivyo. Aidha, vituo sita vya Namtumbo, Ranya, Karagwe, Masasi, Mbozi na Mpanda vinakamilishwa na vinatarajiwu kuanza kutoa huduma ya mawasiliano kwa wananchi kabla ya mwezi Agosti, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, TEKNOHAMA: Kuifanya Tanzania kuwa Kiungo Kikuu cha Mawasiliano Nchini, Kikanda na Kimataifa (*Hub for ICT Infrastructure and Services*). Shughuli zinazotekelzwa na Wizara ili kufikia azma ya kuifanya Tanzania kuwa kiungo kikuu cha mawasiliano ni pamoja na kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kama nilivyoeleza hapo awali. Tayari Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umeunganishwa na Mikongo ya Kimataifa ya SEACOM na EASSy. Aidha, ujenzi wa Mkongo huu umekwishafika mpakani mwa Nchi za Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya. Ujenzi unaendelea ili kufikisha mipakani mwa Tanzania na Nchi za Malawi na Zambia kama nilivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, imewezesha kuanzishwa kwa Kituo cha Uandikishwaji wa Majina Miliki kwa matumizi ya Tovuti na Anuani Pepe Tanzania (*tzNIC*). Hadi kufikia mwezi Aprili 2010, *tzNIC* imesajili vikoa (*domain names*) 5,640. Uanzishaji wa kituo hiki ni muhimu sana katika kuboresha mawasiliano ya intaneti na usalama wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, imeratibu utekelezaji wa ujenzi wa Mradi wa *Super Computer* unaosimamiwa na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Kama nilivyoeleza hapo awali, Mradi huu utaunganishwa na vituo vingine 10 ambavyo vimewekwa katika majengo ya Shirika la Posta Zanzibar na Mikoa ya Pwani (Kibaha na Bagamoyo), Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa, Morogoro, Dodoma na Mtwara. Kwa hali hiyo, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itakuwa ni Kituo cha Umahiri (*Centre of Excellence*) katika nyanja za Teknohana kupitia Mradi huu.

Sayansi na Teknolojia: Utafiti na Maendeleo (*Research and Development - R&D*); pamoja na shughuli za Tume ya Sayansi na Teknolojia kutengewa kiasi cha

angalau asilimia 1.0 ya bajeti ya Serikali kila mwaka, Serikali inaendelea kuongeza tingo la fedha za utafiti kufikia angalau asilimia moja ya pato ghafi la taifa. Kama sehemu ya utekelezaji wa azma hii, Serikali imeendelea kutoa fedha za utafiti nchini kupidia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia (MTUSATE). Katika mwaka wa fedha 2009/10, Mfuko ilitengewa kiasi cha Sh. 900,000,000 kwa ajili ya tafiti zinazoendelea ambazo ni uzalishaji wa mbegu bora ya maharage ya soya yenye sifa ya kutoa mazao mengi kwa ekari; kutambua ujuzi asilia uliopo katika masuala ya bayoanuai ya mimea; lishe inayotokana na mazao na mimea ya misitu yanayoliwa; mchango wa misitu midogo katika kuongeza Pato la Taifa; mimea yenye viatilifu vyenye uwezo wa kuua mbu na kuzuia ugonjwa wa malaria nchini; upatikanaji wa dawa (*Extraction*) kutokana na mmea wa *Artemisin* za kutibu malaria - mmea huo unalimwa Njombe na Arusha; na utafiti uliowezesha kuhawilishwa kwa mashine ndogo inayoweza kuhamishika ya bayogesi (*Compact Portable Biogas*). Mashine hii inalenga kupunguza utegemezi wa nishati ya mkaa na kuni ambazo huchochea uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya utafiti na maendeleo moja kwa moja kupidia Wizara zinazosimamia taasisi za utafiti husika ikiwa ni pamoja na Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika; Maendeleo ya Mifungo na Uvuvi; Afya na Ustawi wa Jamii; Maliasili na Utalii; Nishati na Madini; Elimu na Mafunzo; na Viwanda, Bishara na Masoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa mara ya kwanza tangu nchi yetu ipate uhuru, Serikali ya Awamu ya Nne ya Chama Cha Mapinduzi, imeweza kutenga kiasi kikubwa cha fedha (Sh 30 Bilioni) kwa ajili ya utafiti hapa nchini. Kwa kuanzia, kiasi kikubwa cha fedha hizi kitatumika katika kujenga uwezo katika Taasisi na Vituo vya utafiti wa kilimo ili kutoa mchango mkubwa katika mpango wa Kilimo Kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume Sayansi na Teknolojia ikishirikiana na wadau mbalimbali imeanza mchakato wa kutambua vipaumbele vya utafiti vitakavyowezesha kufikiwa kwa malengo ya MKUKUTA na Milenia hapa nchini. Katika hatua ya awali, maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa ni:-

- (i) Kilimo na chakula ikijumuisha usindikaji;
- (ii) Afya;
- (iii) Mawasiliano, ikijumuisha usafirishaji;
- (iv) TEKNOHAMA;
- (v) Maji;
- (vi) Nishati (*Renewable sources, biofuels, na nuclear energy*); na

(vii) Mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Sayansi na Teknolojia imekusanya taarifa kuhusu ufahamu wa masuala ya hataza na hakimiliki katika taasisi za utafiti na vyuo vikuu nchini. Matokeo yanaonyesha kuwepo kwa ufahamu mdogo wa masuala ya hataza na hakimiliki. Hivi sasa, Tume inaendesa mafunzo kwa watafiti na wanasayansi mbalimbali nchini na pia inahamasisha kuwepo na mtaalam wa masuala ya hataza na hakimiliki katika kila taasisi ya utafiti. Mwongozo wa kuendesa shughuli hizo umetayarishwa na utasambazwa kwa wadau na taasisi zote za utafiti nchini ili kuimarisha usimamizi wa hakimiliki na hataza. Aidha, mchakato wa kuandaa Sera itakayosimamia usajili na kulinda hakimiliki za watafiti na wagunduzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo katika shughuli za kusajili hakimiliki za matokeo ya ubunifu wa watafiti. Mafanikio yaliyopatikana kuitia vyombo mbalimbali vya Kitaifa katika usajili wa hataza na hakimiliki ni:-

(i) Ofisi ya Msajili wa Mbegu mpya za mazao (*Registrar of Plant Breeders Rights*) amesajili jumla ya aina za mbegu 25 kutokana na maombi 36;

(ii) Taasisi mbili zinazofanya shughuli za utafiti ambazo ni Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) zimetengeneza miongozo na mifumo ya namna ya kulinda na kusajili Hakimiliki za matokeo ya ubunifu kwa watafiti wao; na

(iii) Hadi sasa Wakala wa Usajili na Leseni (BRELA) umesajili jumla ya hakimiliki na hataza 34.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamasisha na kuhimiza uzalishaji kibiashara wa zana (*Prototypes*) zinazotokana na tafiti mbalimbali ili ziweze kusambazwa kwa watumiaji. Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeanzisha ushirikiano wa Taasisi za Utafiti na Maendeleo (*Institutions Collaboration in Research and Technology Development*) katika uendelezaji na uhawilishaji Teknolojia hapa nchini. Taasisi zinazohusika katika ushirikiano huu ni *TIRDO*, *DIT*, *MIST*, *TATC – Nyumbu*, *TDTC-CoET*, *CAMARTEC*, *TEMDO*, *NHBRA*, *TaTEDO* na *SIDO*. Ushirikiano huu wa Taasisi umefanikisha kuchapishwa kwa vijarida vya teknolojia zilizo tayari kuhamashara na kusambazwa kwa watumiaji; utengenezaji wa mashine (*prototype*) ya kutengeneza matofali ya sementi na udongo inayotumia sementi kidogo na hivyo kupunguza gharama za ujenzi na ubunifu na usambazaji wa jiko sanifu (KUUTE) ambapo wajasiriamali katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Dodoma, Arusha, Singida na Rukwa wanatengeneza majiko haya na kuyauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, majiko haya hutumia mkaa kidogo zaidi na hivyo kupunguza matumizi ya mkaa. Shirika la Ushirikiano la Ujerumanii likishirikiana na wadau wengine linaeneza teknolojia hiyo sehemu mbalimbali nchini. Kuitia ushirikiano huo mashine ndogo ya *Biogas* inayohamishika (*Compact portable biogas machine*)

imehawilishwa kwa watumiaji mbalimbali. Matumizi ya mashine hii yamepunguza utegemezi wa nishati ya mkaa na kuni jambo ambalo huchochea ukataji wa miti na hatimaye uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya imeendelea na ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 350 kila moja. Aidha, Taasisi imekamilisha tathmini ya mali zilizokuwa katika eneo la taasisi lililoongezwa na taratibu za ulipaji wa fidia zinaendelea kukamilishwa. Mchakato wa kupata mkopo wa Sh 795,703,459 kwa ajili ya ujenzi wa Maktaba yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 2000 kwa wakati mmoja kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Elimu *TEA* upo katika hatua za kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa udahili wa wanafunzi, kama nilivyooleza hapo awali, Taasisi imeweza kuongeza udahili wa wanafunzi mwaka hadi mwaka kutoka wanafunzi 527 mwaka wa masomo 2007/2008, wanafunzi 927 mwaka 2008/2009 na kufikia wanafunzi 1,242 mwaka wa masomo 2009/2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 136 katika miaka miwili. Aidha, kama nilivyooleza awali, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya imeanzisha shahada ya kwanza katika fani za mitambo, ujenzi, umeme, usanifu majengo, sayansi ya biashara na stashahada ya uhandisi wa kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuhamasisha wanafunzi wa kike kusoma masomo ya sayansi. Serikali kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu imeanza kuendesha mafunzo maalum (*Pre-entry programme*) kwa wanafunzi wa kike katika kozi za ufundi na sayansi na kutoa mikopo kwa wanafunzi wote wa Elimu ya Juu wanaosoma masomo ya sayansi. Aidha, Serikali imeendelea kuwatambua na kuwatunuku wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo ya hisabati, kemia, elimu ya viumbe, fizikia, kilimo na kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2009/2010. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu imeendelea kutekeleza ahadi ilizotoa Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano. Wizara imekamilisha uanzishwaji wa vituo vitano vya mawasiliano katika maeneo ya Mrijochini-Kondoa, Kilolo (Iringa), Bagamoyo (Pwani), Wete (Pemba) na Masota A Tegeta (Dar es Salaam). Aidha, hatua za ukamilishaji wa vituo vingine sita katika Wwilaya za Namtumbo, Rorya, Karagwe, Mbozi, Masasi na Mpanda unaendelea. Vituo vinatarajiwa kuanza kazi kabla ya mwezi Agosti, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeratibu uanzishwaji wa Mfumo wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta nchini (*Physical Addresses and Postcode Systems*), ambapo uzinduzi rasmi wa mradi kitaifa ulifanyika mwezi Januari, 2010. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu mradi wa *PAN-African e-network* ambao unahusisha elimu mtandao (*tele-education*), tiba mtandao (*tele-medicine*) na Serikali mtandao (*e-government*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeratibu mafunzo kupitia na mradi wa Pan African e-Network ambayo yamefanyika kwa wasimamizi wa mradi kutoka katika vituo vya Taasisi ya Saratani (Ocean Road), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Ikulu. Aidha, kama nilivyoeleza awali, Wizara imesimamia uandaaji wa Sheria mpya ya Mawasiliano (Electronic and Postal Communication Act, 2009) ambayo ilitungwa na Bunge tarehe 29 Januari, 2010. Sheria hii inalenga katika kuendeleza sekta ya mawasiliano ya kielektroniki na Posta ikiwa ni pamoja na kuboresha matumizi ya mitandao na kupunguza madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi mabaya ya TEKNOHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kufuutilia ulipaji wa madeni ya Shirika la Posta yakiwemo madeni ya wastaifu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki ili Shirika la Posta Tanzania liweze kuondolewa mzigo wa madeni na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma zake kibiashara. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia mchakato wa kuiwezesha Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) kukopesheka, hivyo kuongeza mtaji na kuijimarisha kibiashara. Mchakato huu uko katika ngazi za maamuzi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, TEKNOHAMA. Wizara imeratibu maandalizi na kuwezesha utekelezaji wa programu mbalimbali za kuendeleza miundombinu ya TEKNOHAMA (*ICT-Infrastructure Development Program*) nchini. Hii ni pamoja na kuratibu na kusimamia awamu ya kwanza ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kama nilivyoeleza awali; kuwezesha utekelezaji wa programu ya kuendeleza mifumo, viwango na huduma za TEKNOHAMA (*IT Systems and Services Development Program*) nchini. Aidha, Wizara imeratibu na kusimamia Maandalizi ya Mtandao wa Elimu na Utafiti (*National Education and Research Network- NREN*) utakaounganisha vyuo vikuu na vituo vya utafiti nchini kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zingine za Serikali, imeboresha matumizi ya TEKNOHAMA katika ofisi za Serikali kwa kutoa viwango vya vifaa vya TEKNOHAMA kwa ajili ya ununuzi na utekelezaji wa mpango wa Serikali mtandao (*e-government*). Vile vile, kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara imeweza utekelezaji wa mradi wa Kitaifa wa *Super Computer* ya Taifa na vituo kumi (10) vya tiba mtandao (*e-medicine*) na elimu mtandao (*e-education*) kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Kama nilivyoeleza hapo awali, Kituo hiki kinajengwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya India.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sayansi na Teknolojia. Kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara imeendelea na mchakato wa kutunga Sera ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia, na Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo. Sera ya Bioteknolojia imekamilika na kuchapishwa. Vile vile, Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hii umeandaliwa. Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo iko katika hatua ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Rasimu ya sera ya Sayansi ya Teknolojia ya Nyuklia imeandaliwa na itajadiliwa na wadau mwezi Julai 2010. Kanuni za

matumizi ya mionzi zimeandaliwa na zitajadiliwa na wadau mwezi Julai 2010 na kufuatiwa na mchakato wa kuridhiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inahuisha Sheria na. 7 ya mwaka 1986 iliyoanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa. Aidha, hatua za awali za kuanzisha Kituo cha Uhawilishaji wa Teknolojia za Viumbe Hai (*The Life Science Business Innovation Park*) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zimeanza. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekamilisha hatua za awali za kuanzisha Kituo cha Taifa cha Baioteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatekeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa ushirikiano na Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Sekretariati na Kamati ya Kusimamia Programu imeteuliwa na ilianza kazi tarehe 1 Aprili, 2010. Aidha, Wizara imesimamia mchakato wa kuridhia Itifaki ya Kuunda Baraza la Sayansi na Teknolojia la Afrika Mashariki. Mchakato huu upo katika ngazi ya juu ya maamuzi Serikalini. Kuridhiwa kwa Itifaki hii kutaimarisha mahusiano ya nchi yetu na nchi zingine Kikanda na Kimataifa kwenye nyanja za sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilisimamia uanzishwaji wa Taasisi ya Sayansi, Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha, ambapo kama nilivyoeleza hapo awali, uongozi wa muda wa Taasisi umeteuliwa na kuanza kazi tarehe 1 Julai, 2009. Ukarabati na ujenzi wa majengo ya Taasisi hiyo utaanza hivi karibuni kufuatia kukamilika kwa taratibu za Mkopo wa Sh. bilioni 38.7 kutoka katika mifuko ya pesheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala na Rasilimali Watu. Wizara imeajiri watumishi 10 kwa mujibu wa ikama na mahitaji ya muundo mpya wa Wizara. Aidha, watumishi walioajiriwa wamepewa mafunzo elekezi katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Wizara pia imewapandisha vyeo watumishi sita wa kada mbalimbali kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyopo katika Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi za Mwaka 2002 na kwa kuzingatia utendaji wa kila mmoja kazini kwa mujibu wa Tathmini ya Utendaji Kazi (*OPRAS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi 13 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu, kati yao watumishi 10 wamefanya mafunzo ndani ya nchi na watatu (3) nje ya nchi. Aidha, watumishi 22 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ili kuongeza ujuzi, maarifa na ufanisi katika utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza mfumo wa kupima utendaji kazi kwa uwazi (*OPRAS*) kwa watumishi 127 wa Wizara kuitia mikataba ya kazi. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza mkakati na mpango wa kazi wa Wizara wa kupambana na rushwa na kuelimisha watumishi kuhusu sheria, kanuni na taratibu za

utendaji kazi katika utumishi wa umma. Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu umefanywa kupitia Kamati ya Uadilifu (*Integrity Committee*) ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kujikinga na kuepuka maambukizi mapya ya ukimwi, upimaji wa UKIMWI kwa hiari, matumizi ya dawa za kurefusha maisha kwa waishio na virusi nya UKIMWI na kupunguza maambukizo ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi waliopata maambukizi kujitokeza ili waweze kupatiwa huduma kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Serikali Na. 2 wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara imeendelea kutoa huduma bora kwa wateja wake kwa kuzingatia vigezo nya huduma vinavyopimika kwa mujibu wa Mikataba wa Huduma kwa Mteja wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sera na mipango. Pamoja na uandaaji wa sera mbalimbali nilizozitaja hapo awali, Wizara imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kipindi cha 2005-2010 ambao umewasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, Wizara imeratibu uandaaji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia (*Communication, Science and Technology Master Plan*). Mpango huu upo katika hatua za maandalizi yanayofanywa na Mshauri Mwelekezi. Vile vile, Wizara imeshiriki na kuchangia katika shughuli za ushirikiano wa Tanzania na nchi zingine Kikanda na Kimataifa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Afrika Mashariki kupitia Mikutano, Mikataba na Itifaki mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala mtambuka. Wizara imeendelea kusimamia uratibu na ukaguzi wa matumizi ya fedha za Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuwa na matokeo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika masuala yote yanayohitaji ushauri wa kisheria ikijumuisha masuala ya Mikataba, Miswada, Sheria ndogondogo, Kanuni, pamoja na mashauri mbalimbali yanayohusu Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuelimisha umma na wadau kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ambapo nakala 7,000 za vipeperushi kuhusu sera mbalimbali za Wizara; ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela-Arusha; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania na Vituo nya mawasiliano. Aidha, nakala 2,542 za Jarida la Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za sekta ya mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kupitia redio, luninga na matukio mbalimbali kama vile Mkutano wa *ITU* (Geneva),

Uzinduzi wa *SEACOM*, wageni mbalimbali wa Wizara akiwemo Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani, Siku ya Posta Duniani, Maonesho ya Nane Nane na Maadhimisho ya Miaka 30 ya Umoja wa Posta Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia, imeendelea kutoa taarifa na kuelimisha umma kuititia tovuti ya Wizara. Taarifa hizo ni pamoja na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya 2003, Sera ya Taifa ya Posta ya 2003 na Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya 1996.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa ununuzi wa bidhaa na huduma umefanya kulingana na kanuni, watumishi saba walijengewa uwezo kwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi ya taratibu na kanuni za manunuzi ya umma. Wizara pia imeandaa mpango wa ununuzi wa mwaka 2009/10 (*General Procurement Notice*). Zabuni 20 zenye thamani ya Shilingi bilioni tano zimeshughulikiwa. Wizara pia imeendelea kuandaa taarifa za kila mwezi kuhusu ununuzi na kuziwasilisha Mamlaka ya Ununuzi Tanzania. Aidha, Wizara imeweka mfumo wa kutunza taarifa mbalimbali za watumishi (*LAWSON*). Watumishi wawili walipewa mafunzo jinsi ya kuutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa watumishi 10 kuhusu namna ya kutunza siri za Serikali katika Kompyuta na mtandao yametolewa. Vile vile, kijitabu cha Mwongozo na Taratibu za Kutunza Siri za Serikali katika mtandao wa Kompyuta kimetayarishwa. Wizara imetayarisha miongozo ya mafunzo ya kompyuta kwa hatua ya mwanzo (*Basic Computer Application* na *Power Point Presentation*) kwa ajili ya mafunzo ya ndani ili kuwajengea uwezo watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili jumla ya wanafunzi 1006 katika programu mbalimbali zinazotolewa na Taasisi hiyo na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi wote mwaka 2009/2010 kuwa 2,263 ambalo ni ongezeko la asilimia 22.3 ikilinganishwa na mwaka 2008/2009. Aidha, Taasisi imeandikisha jumla ya wanafunzi wa kike 35 (Ufundi sanifu 27, Uhndisi wanane (8)) katika kozi ya mafunzo ya awali (*Pre-entry Training*) iliyoendeshwa mwezi Juni hadi Septemba 2009. Baada ya mafunzo hayo wanafunzi 28 (Ufundi sanifu 20, Uhndisi wanane (8)) walifaulu na kudahiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi imepeleka wafanyakazi 19 katika masomo ya juu kama ifuatavyo: wakufunzi 17 (Shahada ya Uzamili 10 na Uzamivu 7) na waendeshaji wawili (2) kwa Shahada ya Uzamili. Pia, Taasisi imeendelea kugharimia wafanyakazi wanaoendelea na masomo ya juu ndani na nje ya nchi 38, Wakufunzi 29 (Shahada ya Uzamili 12 na Uzamivu 17) na Waendeshaji 9 (Shahada ya Uzamili wawili (2), Stashahada ya juu wanenye (4) na Stashahada watatu (3)).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi imekamilisha maandalizi ya awali ya ukarabati wa hosteli sita za wanafunzi ikiwemo utayarishaji wa mahitaji ya vifaa vya ujenzi *BoQ* ambapo ukarabati utaanza mwaka 2010/2011. Vile vile, Taasisi imeendeleza ujenzi wa

jengo la madarasa, maabara na ofisi (*DIT Teaching Tower*) ambapo ujenzi uko katika ghorofa ya nane kati ya ghorofa 10 zitakazojengwa. Aidha, Taasisi imekamilisha ukarabati wa vyumba na kuweka vifaa na mitambo kwa ajili ya mradi wa *Super Computer*. Taasisi pia imekamilisha ukarabati na uwekaji wa mitambo vituo saba kati ya vituo 10 vya Habari Jamii Zanzibar, Kibaha, Bagamoyo, Iringa, Mbeya, Arusha na Mwanza. Mitambo ya vituo vitatu vilivyobaki (Morogoro, Mtwara na Dodoma) imeshapokelewa kutoka India na kupelekwa katika vituo hivi ambapo ukarabati unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 200/2011. Aidha, kama nilivyoeleza hapo awali, Wafanyakazi tisa watakaoendesha Kituo hiki wamemaliza masomo ya miezi sita nchini India na kurudi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi imewasilisha katika Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundji (*NACTE*) mitaala ya kozi za Stashahada ya *Biomedical Equipment Engineering* na *Communication System Engineering* ili kupata ithibati. Kozi hizi zitaanza kufundishwa mwaka wa masomo 2010/2011. Aidha, mtaala wa kozi mpya ya sita ya *Multimedia Technology* umekamika na kuwasilishwa *NACTE* kupata ithibati. Vile vile, Taasisi imekamilisha utayarishaji wa mitaala mipyä ya uanzishwaji wa kozi mpya tano za Stashahada za: *Heating, Ventilation, Air-conditioning and Refrigeration; Mechatronics; Electronics Equipment Maintenance; Geographical Information Systems na Transportation Engineering* na zinasubiri idhini ya Bodi ya Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi, kwa kushirikiana na Wizara, imekamilisha taratibu na kumilikishwa kilichokwuwa Chuo cha Ngozi Mwanza. Aidha, mafunzo yataanza baada ya ukarabati wa awali kukamilika. Katika kuhawilisha matokeo ya tafiti zake, Taasisi imetengeneza na kuweka taa mpya za kuongoza magari katika maeneo matatu ya barabara ya Ali Hassani Mwinyi sehemu za Salender Bridge na Barabara ya Kinondoni. Taasisi itaendelea kutangaza bidhaa kama hizi ili ziweze kutumika ndani na nje ya nchi. Napenda kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha matumizi ya teknolojia hizi katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya imeongeza idadi ya wanafunzi kutoka 927 kwa mwaka 2008/09 hadi kufikia wanafunzi 1,242 kwa mwaka 2009/2010. Hili ni ongezeko la asilimia 34 ambalo ni kubwa. Vile vile, Taasisi imeajiri wakufunzi 38, mafundi sanifu 17 katika fani mbalimbali na waendeshaji 26. Hii inafanya jumla ya waajiriwa wote wapya kuwa 81.

Aidha, Taasisi imeendelea kutoa mafunzo ya awali (*pre-entry course*) kwa wanafunzi wa kike katika masomo ya Sayansi, Uhandisi na Teknolojia. Jumla ya wanafunzi 50 walijiunga na mafunzo haya kwa mwaka 2009/2010, wasichana wakiwa 30 na wavulana 20. Mpango huu ni wa kudumu na unalenga kuwavutia wasichana wengi kuijunga na masomo ya Sayansi, Uhandisi na Teknolojia. Vile vile, Taasisi imefanya tathmini ya mali za wananchi waishio katika eneo la Taasisi kwa ajili ya ulipaji fidia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi imendelea kujizatiti na kupanua huduma zake kwa kuwa na chumba cha maabara, kununua vifaa vya maabara na kuanzisha mtaala wa

Sayansi na Teknolojia ya Maabara na mtaala wa Uongozi wa Biashara katika ngazi ya stashahada. Taasisi pia imeajiri waalimu watano na mafundi sanifu watatu ili kuongeza idadi ya waalimu katika fani mpya ya Sayansi na Teknolojia ya Maabara. Aidha, Taasisi inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili yenye ghorofa yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 350 kila moja. Ujenzi umefikia ghorofa ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi imepeleka jumla ya watumishi 40 masomoni kama ifuatavyo: Stashahada ya kawaida mtumishi mmoja; Stashahada ya Juu watumishi wawili; Shahada ya Kwanza watumishi watano; Stashahada ya Uzamili watumishi watatu; Shahada ya Uzamili 23 na Shahada ya Uzamivu watumishi sita. Pia, Taasisi imeendeleza ushirikiano na vyuo vya ufundi barani Afrika chini ya utaratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa - (CAPA)*. Aidha, Taasisi imeingia mkataba wa ushirikiano na *KIITEC (Kilimanjaro International Institute of Telecommunication and Computer)*. Vile vile, Taasisi inajiandaa kuwa na mikataba ya ushirikiano na Chuo cha Ufundi Arusha, Chuo cha Ufundi Lilongwe (Malawi) na *Bielefeld University of Applied Science* na *Technical University ya Dortmund* vilivyopo nchini Ujerumanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha imekamilisha maandalizi ya Mpango Kabambe wa Taasisi unaolenga kuiwezesha Taasisi kuanzishwa kwenye eneo lililokuwa linamilikiwa na *CAMARTEC*. Ili kuiwezesha Taasisi hiyo kuweza kuanza kutoa mafunzo, miundombinu ya umeme, maji na barabara imekarabatiwa. Udhili wa wanafunzi unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba 2010. Kama nilivyoeleza hapo awali, Mkataba kati ya Serikali na *PPL* umetayarishwa na kusainiwa mwezi Mei 2010, ambapo Serikali itakopeshwa kiasi cha Sh. 38,717,114,879. 66 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu muhimu. Miundombinu hiyo ni pamoja na vyumba vya miadhara, maabara na ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi imekamilisha uandaaji wa mtaala ya *Life Sciences and Bio-engineering, Mathematics, Computational and Communication Science and Engineering, Water Resources and Environmental Science and Engineering, Materials Science and Engineering* na mtaala wa *Sustainable Energy Science and Engineering*. Aidha, nafasi za ajira za wanataaluma na waendeshaji zimetangazwa na sasa Taasisi iko katika hatua ya kuajiri. Pia, Taasisi imekamilisha muundo wa utumishi (*Scheme of Service*) na iko katika mchakato wa kuunda vyombo vya kiutendaji (Baraza la Taasisi Seneti na kadhalika).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imekamilisha Mpango Mkakati na tayari umekwisheridhiwa na Bodi ya Tume na umeanza kutekelezwa kuanzia Januari 2010. Vile vile, Tume imeendelea kugharimia tafiti zilizo katika maeneo yaliyoainishwa kwenye vipaumbele vya utafiti vya Taifa. Aidha, miradi miwili imefadhliliwa na *MTUSATE* ambayo ni utafiti wa uimarishaji wa upatikanaji wa madini ya fosfori kwa ajili ya kilimo hai (*organic farming*) cha mazao ya mboga kwa kutumia mbolea ya Minjingu, na utafiti wa uchambuzi wa vinasaba na alama za vinasaba vinavyostahimili ugonjwa wa kiwele

(*mastitis resistance*) kwenye ng'ombe wa asili. Utafiti unalenga uboreshaji wa mbinu za kudhibiti ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na chanjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Juni 2009, Tume ilitisha maombi ya tafiti zinazozingatia mahitaji ya MKUKUTA na (*Millenium Development Goals - MDG*) ambazo zitafadhiliwa na Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (*MTUSATE*). Maombi (*proposals*) 107 yalipokelewa yenyе kuhitaji jumla ya Sh.10, 356,360,272. Mchakato wa kuchambua maombi haya umekamilika na miradi tisa yenyе thamani ya Sh. 793,861,760 itafadhiliwa. Miradi sita kati tisa iko kwenye sekta ya kilimo, miwili inayohusu mifugo na mradi mmoja uko katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki. Tume ilipima Sampuli zipatazo 4,564 za vyakula na mbolea na kuzitolea vibali (leseni). Utekelezaji wa jukumu hili ulifanikiwa kwa kiwango cha 175.5% ya malengo. Upimaji wa mionzi ulifanyika katika vituo 26 kama ilivyokusidiwa na upimaji wake unaendelea kila baada ya miezi mitatu. Vile vile, kama nilivyoeleza hapo awali, Tume ilifanya ukaguzi katika migodi mitano ambayo ni: Mgodi wa *Tanzanite One Limited* wa Mererani (Manyara), Mradi wa Urani wa Mto Mkujju, Namtumbo (Ruvuma), Mradi wa Urani wa Bahi (Dodoma), Mradi wa Urani wa Manyoni (Singida) na Machimbo ya Mawe yanayotumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, Uchira (Moshi Vijijini) ili kubaini hali ya usalama. Aidha, Tume iliendelea na upimaji wa viasili (viini) vya mionzi katika sampuli za hewa na mazingira katika kituo chake kilichopo Dar es Salaam katika Idara ya Fizikia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume iliratibu miradi tisa (9) ya kitaifa pamoja na miradi 30 ya Kikanda (*AFRA*) na miradi mingine 26 ya Kanda ya Afrika inayofadhiliwa na Shirika la *IAEA* na kuwasilisha mapendekezo ya uboreshaji wa miradi hiyo. Miradi hiyo ya Kitaifa ni *URT502: Enhancing Crop Productivity through Radiation* (US\$ 391,424); SUA-URT50: *Nuclear Techniques for the Monitoring of the Food Quality in the United Republic of Tanzania* (US\$ 264,310); TFDA-URT5026: *Improving Rice Varieties through Mutation Breeding and Biotechnology in Zanzibar* (US\$ 260,960); Ministry of Agricultural, Livestock and Envir. *Kizimbani Research & Training Station, Zanzibar- URT6021: Establishing a Radiotherapy Education and Training Programme* (US\$ 412,426); ORCI/MUHA-URT6022: *Establishing a Radiotherapy and Nuclear Medicine Services at the Bugando Medical Centre* (US\$ 1,379,036); Bugando Medical Centre- URT6024: *Molecular Genetic Analysis of Drug Resistant Isolates of M.Tuberculosis in Tanzania* (US\$ 326,284); Muhimbili University of Health and Allied Sciences-URT6025: *Improving and Expanding Nuclear Medicine and Brachytherapy Services at Ocean Road Cancer Institute* (US\$ 364,866); ORCI- URT8013: *Assessment of Groundwater Resources in Usangu Catchment by Use of Isotope Techniques* (US\$ 220,072); Rufiji Water Basin Office, Water Resource Iringa- URT9005: na mradi wa *Strengthening the National Regulatory Infrastructure and Radiological Protection of Workers Occupationally Exposed to Ionizing Radiation* (US\$ 165,865) wa TAEC.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imeshirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*IAEA*) kuendesha semina mbili kwa wafanyakazi 92 katika idara za *X-ray* viwandani, migodini na kwa wajenzi wa barabara. Pia, Tume imeendesha semina nne kwa viongozi

wa mikoa ya Ruvuma na Dodoma. Katika Mkoa wa Ruvuma, washiriki wa semina walikuwa 12 akiwemo Mkoo wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Mbunge wa Namtumbo, Wakurugenzi wa Halmashauri na wafanyakazi wa Mto Mkusu, *MANTRA*. Katika Mkoa wa Dodoma semina ilishirikisha viongozi 33, hususan Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, wakiwemo Mkoo wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya wote, Mbunge wa Bahi, Maofisa Usalama wa Mkoa na wafanyakazi wa mradi wa *URANEX*. Aidha, mipango imeandalili ili kutoa semina kama hiyo kwa viongozi wa Mkoa wa Singida. Pia Tume imeshiriki katika maonesho mawili yaliyoandalili na Tume ya Vyuo Tanzania (TCU) na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na kutumia fursa hiyo kuelimisha umma juu ya matumizi ya teknolojia ya nyuklia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imetoea jumla ya semina tano zilizohusisha wataalam wa nje na ndani kuhusu mada mbalimbali zikiwemo: *The national training course on radiation safety for radiation safety officers in medical diagnostic X-ray facilities; National training course on radiation safety for radiation safety officers in industry radiation facilities, Inter-regional seminar on IAEA's safeguards system for states with limited nuclear materials and activities, The 2nd East African Workshop on Electromagnetic field exposure and health: harmonizing EMF risk communication and EMF policy* na semina kuhusu *Regional training course on calibration of test instruments*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imeendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa kazi zake na pia inaendelea kufuatilia kwa karibu uanzishwaji wa ofisi visiwani Zanzibar. Aidha, Tume inaendelea na mpango wa kuanzisha ofisi mbalimbali za kikanda katika maeneo yaliyo na madini ya urani ili kuweza kufanya kazi zake kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta Tanzania linaendelea kutekeleza Mradi wa *Counter Automation* ambapo hadi sasa ofisi za Posta kuu za mikoa 14 zimeshaunganishwa kwenye mtandao wa kompyuta. Lengo ni kuziunganisha Posta zote kuu za mikoa yote nchini pamoja na Wilaya zake kwenye mtandao huu. Mafunzo mbalimbali yametolewa kwa wafanyakazi ili waweze kuzimudu vizuri kazi zao. Vilevile, mafunzo ya teknolojia mpya yanaendelea kutolewa na tayari wafanyakazi 60 wamepatiwa mafunzo ili kuwawezesha kutoa huduma bora kupitia *Counter Automation*.

Aidha, kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Shirika limeendelea kutekeleza mradi wa *Super-Computer* ambapo ofisi za Shirika la Posta zitatumika kwa ajili ya vituo vya kutoa huduma mbalimbali za TEKNOHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtandao wa Posta umepanuka na kuimarika na hivyo kuweza kufikisha huduma karibu zaidi na wananchi. Vituo vya Posta vinavyotoa huduma ya kutuma fedha, nyaraka na vifurushi vya haraka (EMS) ambazo zimeongezeka kutoka vituo 145 vinavyotoa huduma hiyo mwaka 2008 hadi kufikia 148 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Shirika limeendeleza na kuingia mikataba mipyä na Wizara mbalimbali, Taasisi za Serikali, Mabenki na Makampuni binafsi.

Mikataba hiyo inahusu kusafirisha barua, nyaraka na vipeto kwa njia ya *EMS*, kukusanya ada mbalimbali kwa niaba ya taasisi hizo, kulipa gawio (*dividends*) kwa niaba ya makampuni yanayolipa gawio kwa wanahisa wao na mkataba kuhusu uwakala wa Benki ya Posta.

Shirika limetekeleza muundo mpya (*Organization structure*) ambao unalenga kuleta ufanisi zaidi katika utendaji ndani ya Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika pia, limekamilisha ujenzi wa Posta mpya ya Temeke Dar es Salaam. Matengenezo yamefanyika katika Posta za Mbeya, Mererani, Namanga, Shinyanga, Sumbawanga, Songea, Korogwe, Mafinga, Kinampanda na Tarakea. Aidha, ukarabati wa Posta Kuu ya Tanga unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudzi za kujikwamua kutokana na ukosefu wa fedha, mchakato wa kupata fedha kwa njia ya ubia na mikopo kuitia viwanja ambavyo havijaendelezwa unaendelea vizuri. Mchanganuo unaoonyesha matumizi bora ya kila kiwanja umetayarishwa na kujadiliwa na Kamati ya Wataalam (*DTT*) ya *Consolidated Holding Corporation (CHC)* na kuridhiwa. Aidha, rasimu ya tangazo la kukaribisha wabia kuandika kuonyesha kusudio la ubia huo (*Expression of Interest*) imeshatayarishwa na kuwasilishwa *CHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya Simu Tanzania imefanikiwa kujenga jumla ya njia (Broadband lines) 500 kwa kutumia teknolojia ya fibre kwenda kwa wateja wake wakubwa ikiwa ni pamoja na taasisi za fedha za *Barclays Bank, NMB, NBC and CRDB*. Aidha, Kampuni imejenga Mtandao wa *fibre* kwenda kwenye majengo makubwa kama vile *Life House, JMALL, Mawasiliano House, Alpha House, Hifadhi House*, na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Pia, Kampuni imetekeleza mradi wa kubadilisha mitambo ya simu ya Dar es Salaam *NEAX, Pangani (DTS)* na Kibondo (*DTS*) na kuweka mitambo mipyä yenye uwezo wa kutoa huduma za kisasa kwa ajili ya simu na takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni imeshiriki katika kusimamia ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kampuni imetayarisha Mpango wa Biashara wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Maeneo yaliyoainishwa katika mpango huo yanalenga katika kuendesha kwa Biashara Mkongo huo. Miiongoni mwa maeneo yaliyoainishwa ni pamoja na wajibu wa *TTCL* katika uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na taratibu zitakazotumika katika utoaji wa huduma kwa wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ikishirikiana na wadau wengine wa mawasiliano nchini ilianzisha na kusimamia zoezi la kusajili simu za viganjani. Zoezi hili litakamilika tarehe 15 Julai 2010. Hii ni hatua muhimu sana katika kuelekea kwenye uunganishwaji wa huduma ya *Central Equipment Identification Register (CEIR)* ya hapa nchini na *CEIR* nyingine za nchi za Afrika Mashariki. Aidha, Mamlaka ikishirikiana na umoja wa watoa huduma ya

intaneti (*TISPA*) imenunu mtambo wa kuunganisha watoa huduma wa intaneti wa Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Mwanza ambayo kimsingi inaunganisha kanda za Mashariki, Kaskazini, Kati na Ziwa. Tathmini ya mafanikio ya mitambo hiyo inaonyesha kuongezeka kwa wadau waliojiunga na mitambo hiyo na hivyo jitihada ya kununua mitambo mingine na kuunganisha mikoa ya Mbeya kwa ajili ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Zanzibar zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2009/2010 kuhusu mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka analogia (*analogue*) kwenda dijitali (*digital*) ambapo mabadiliko hayo yanatakiwa kukamilika ifikapo mwaka 2015, Serikali imepiga hatua katika kutekeleza azma hiyo. Aidha, Kampuni tatu zimekubaliwa kuwa waunganishaji wa matangazo kwa kupitia teknolojia ya digitali. Kampuni hizo ni *Agape Associates (T) Limited, Basic Transimission Limited na StarMedia (T) Limited*. Taratibu za kugawa masafa yatakayotumika katika Mfumo huo mpya wa matangazo (*Digital broadcasting*) zimefanyika. Hadi sasa, leseni za kutumia teknolojia hii mpya ya utangazaji wa digitali imetolewa kwa Kampuni ya *Agape Associates (T) Limited na StarMedia (T) Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha mawasiliano na nchi nyiningine kwa lengo la kuyaboresha na kupunguza gharama. Uunganishwaji wa *Internet Exchange Points* za nchi za Afrika Mashariki unaendelea na upo kwenye hatua za awali. Kukamilika kwa zoezi hili kutaongeza usiri na usalama wa taarifa mbalimbali na kupunguza gharama za kutumia huduma za Mawasiliano. Vile vile, kwa kutumia mitambo ya ukaguzi kama vile *Frequency Monitoring Equipment, Automated Quality Mail System (AQMS)* na *Content Monitoring Equipment* Mamlaka inakagua na kuchunguza ubora wa huduma za mawasiliano ya simu, posta na utangazaji zinazotolewa nchini. Aidha, Mamlaka imeratibu shughuli za kampuni za simu nchini na hadi sasa kuna jumla ya watumiaji wa simu zaidi ya milioni 18 na watoa huduma za simu wapatao 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2009/2010. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, katika kipindi cha utekelezaji, Wizara yangu imekabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zilichangia katika kutofikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni tengeo la fedha za Utafiti na Maendeleo kutofikia lengo. Shughuli za utafiti na maendeleo katika mwaka wa fedha huu bado hazikuwa zimetengewa fedha za kutosha ili kuharakisha kufikiwa kwa kiwango cha asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa kama ilivyoahidiwa na kuagizwa. Upungufu huu wa fedha umeendelea kuathiri shughuli za utafiti na maendeleo. Wizara inaendelea kufuatilia suala hili ili fedha hizo zitengwe kwenye bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni uhaba wa wataalam wa kutosha katika nyanja mbalimbali kunakojitokeza kwa kuwepo na idadi ndogo ya wataalam, wataalam wengi kuwa wa umri mkubwa, wataalamu kutokwa na uelewa wa teknolojia mpya na uwiano wa kada mbalimbali kama vile uwiano wa kada ya wahandisi na mafundi wa ngazi ya cheti na diploma ambao umeathiri utendaji katika ya sekta. Wizara, kupitia Sera ya

Utafiti na Maendeleo inaandaa mikakati ya muda mfupi na mrefu kulipatia ufumbuzi tazito hili. Aidha, Serikali kuptitia Sekta mbalimbali ikiwemo ya Elimu iliendelea kushughulikia changamoto hii ili kuipatia ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni uelewa mdogo wananchi walio wengi juu ya umuhimu wa Sayansi na Teknolojia unaodunisha uhitaji na matumizi ya sayansi na teknolojia katika uzalishaji na katika upatikanaji na utoaji wa huduma za kijamii. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa sayansi, teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya nchi hasa wakati huu wa uchumi wa ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni Taasisi zinazohudumia Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuwa katika hatua ya kujijenga ama kutokana na kuwa katika hatua za kuanzishwa (kama vile Taasisi ya Nelson Mandela na Chuo cha Taaluma ya Bidhaa za Ngozi cha Mwanza), au kujipanua kama ilivyo kwa Taasisi za *MIST* na *DIT* ambazo zinaongeza michepao na udahili. Kwa pamoja, kuna changamoto nyingi ikiwemo uhitaji wa miundombinu na kiwango cha matumizi ya kawaida kikubwa kuliko ongezeko halisi la bajeti inayotolewa. Katika kupunguza athari za changamoto hii, Wizara imetumia njia mbalimbali ikiwemo ya kutumia mikopo toka Taasisi za Fedha. Hata hivyo, ufumbuzi wa kudumu, hususan katika gharama za uendeshaji, utahitaji ongezeko la bajeti katika miaka ijayo kuelekezwa katika Taasisi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kama ilivyoelezwa katika maelezo juu ya fedha za utafiti, Wizara bado inakabiliwa na changamoto ya kutopewa fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwemo ya ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano inayohitaji fedha nyingi. Hii ni pamoja na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, uwekwaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Simbo za Posta ambao unapaswa kuenda sambamba na utoaji wa vitambulisho vya mkazi. Kukamilishwa kwa miundombinu hii kutakuwa na manufaa makubwa kwa nchi kiuchumi na kijamii, lakini kunahitaji fedha nyingi katika hatua hii ya uwezekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto zilizojitokeza hapo juu, Wizara inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa umakini na kwa kuzingatia hali halisi ili kuwezesha upatikanaji wa miundombinu bora itakayowezesha uendelezaji wa sekta ya mawasiliano, teknolojia na sayansi nchini. Maendeleo ya sekta hii ni ya muhimu ili kutumia kwa tija rasilimali zilizopo nchini ikiwa ni pamoja na rasilimali watu yenye uwezo na maarifa wa kuibua na kutumia fursa mbalimbali zilizopo kuleta maendeleo na kuliiondoa taifa katika hali ya umaskini ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara yangu kuptitia Idara na Taasisi zake imejiwekea malengo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala na Rasilimali Watu. Wizara imepanga kuajiri watumishi wapya 10 kwa mujibu wa ikama na mahitaji ya muundo mpya wa Wizara. Aidha, watumishi watakaoajiriwa watapewa mafunzo elekezi kupitia Chuo cha Utumishi wa Umma. Pia, Wizara imepanga kuwapandisha vyeo watumishi 10 wenye sifa na wanaokidhi vigezo vya miundo yao ya utumishi na tathmini ya utendaji kazi kupitia mfumo wa tathmini wazi (*OPRAS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi 19 watapelekwa kwenye mafunzo katika taaluma mbalimbali. Pia, Wizara itatoa mafunzo kwa Waelimisha Rika 10 wa kutoa ushauri nasaha kuhusu maambukizi ya virusi vya UKIMWI na utoaji wa huduma kwa waathirika. Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao ili wale watakaobainika kuathirika wajitokeze na kupatiwa huduma. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa watumishi 127 kuhusu UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kupima tathmini ya utendaji kazi kwa uwazi (*OPRAS*), na kuelimisha watumishi kuhusu utekelezaji wa kanuni za maadili ya kiutendaji katika Utumishi wa Umma ikiwa ni pamoja na kuzuia na kupambana na rushwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sera na mipango. Wizara itarejea Mpango Mkakati wa Wizara (*Strategic Plan*) ya mwaka 2008/2009 – 2011/2012 na kusimamia Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2010-2015 katika Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Aidha, itasimamia utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi mbalimbali inayotekelzwa ikiwa ni pamoja na ile ya Taasisi zilizo chini yake. Wizara itaimarisha ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika masuala ya kisekta. Aidha, itaandaa, chapisho la takwimu mbalimbali zinazotoa taarifa ya maendeleo ya sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nyanja za mawasiliano, Wizara itaendelea kushauri na kusimamia utendaji kazi wa Kampuni ya Simu Tanzania, Shirika la Posta Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*). Pia, Wizara itaendelea na mchakato wa kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania ili yaweze kujenga uwezo na ufanisi wake wa utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa Anuani Mpya za Makazi na Simbo za Posta katika maeneo ya Arusha, Dodoma na Zanzibar. Hatua hii itaweka msingi wa hatua ya baadaye ya kueneza mradi nchi nzima. Wizara itakamilisha uaandaji wa Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta. Vile vile, itakamilisha utekelezaji wa mradi wa *Pan African e-Network* kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaanzisha vituo 10 vya Mawasiliano vijiji. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utendaji kazi wa vituo 15 vya Mawasiliano vilivyoanzishwa kwa lengo la kuvii marisha na kuhuisha uzoefu uliopatikana kuigwa na kunezwa sehemu zingine kuitia wadau mbalimbali wa maendeleleo zikiwemo Serikali za Mitaa. Wizara pia itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kusimamia utekelezaji na uridhiwaji wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa katika sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itakamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe wa TEKNOHAMA (*An intergrated ICT-Led Socio-Economic Development Master Plan for Tanzania*), na kuratibu hatua za awali za ujenzi wa kituo cha kitaifa cha kutunza kumbukumbu za TEKNOHAMA (*MegaData Centre*). Wizara pia, itaratibu utekelezaji wa programu ya kujenga uwezo wa rasilimali watu ya TEKNOHAMA nchini ili kupunguza uhaba wa rasilimali watu katika sekta ya TEKNOHAMA. Vile vile, Wizara itaratibu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Awamu ya Pili ya Ujenzi itakayolenga kufikisha huduma za mawasiliano katika makao makuu ya mikoa na wilaya Tanzania Bara na Zanzibar. Wizara pia, itaratibu utekelezaji wa programu ya kuendeleza mifumo, viwango na huduma za TEKNOHAMA (*IT Systems and Services Development Program*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaandaa viwango mbalimbali vya TEKNOHAMA vikiwemo vya *Software Hardware* na *Professional Certification*. Viwango hivi vitasimamiwa na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) katika ununuzi wa vifaa na huduma za TEKNOHAMA nchini. Vile vile, Wizara itaratibu uunganishwaji wa Wizara 15, Taasisi 50 za Serikali, na Vyuo Vikuu na Vituo vya Utafiti 27 nchini kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Aidha, Wizara itaratibu Mpango wa Kujenga Jamii Habari ikiwa ni pamoja na kujenga mazingira mazuri ya kutumia huduma ya TEKNOHAMA. Pia, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya TEKNOHAMA ya mwaka 2003 na kuandaa Sera ya Usalama wa Mtando (Cyber Security Policy).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Wizara itakamilisha uandaaji na upitiaji wa Sera na uandaaji wa mipango ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo, na; Sera ya Taifa ya Teknolojia za Nyuklia. Wizara pia, itasimamia upitiaji wa Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 iliyoanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania na uundaji wa Sheria ya uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu hapa nchini. Vile vile, Wizara itasimamia maboresho ya Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itakamilisha mikataba ya ushirikiano na nchi za India, Afrika ya Kusini na Msumbiji. Aidha, Wizara itasimamia uanzishwaji wa *Science, Technology and Innovation Park* na *Agricultural Biotechnology Centre*. Vile vile, Wizara itaratibu uridhiwaji wa mikataba mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala mtambuka. Wizara itaendelea kukagua na kutoa taarifa za matumizi ya rasilimali za Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Aidha, itafuatilia utekelezaji wa ushauri uliotolewa katika Taarifa za Ukaguzi ili kurekebisha kasoro zilizojitekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kusimamia Sera, miongozo na mikakati ya sekta ya TEKNOHAMA, Mawasiliano, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Vile vile, itasimamia na kuratibu uandaaji wa mikataba na uridhiwaji wa itifaki za kisekta. Aidha, itaandaa Miswada ya sheria na sheria ndogo zinazoihusu sekta ya Mawasiliano, TEKNOHAMA na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa kushrikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia itaendelea kushughulikia masuala ya madai na usuluhishi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vipeperushi, majarida, mabango, redio, luninga pamoja na magazeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaboresha daftari la vifaa na samani (*Fixed Assets Register*), kukagua, kuvirodhesha na kuviwekea alama ya utambuzi (*codification*) vifaa na samani zote kwa Wizara nzima. Aidha, itatoa mafunzo maalum kwa ajili ya kuelimisha watumishi juu ya taratibu na sheria ya manunuza ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 na kusimamia shughuli zote za ununuza na ugavi za Wizara kwa mujibu wa Sheria ya Manunuza ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005. Aidha, Wizara itaandaa taarifa za Ununuza za kila mwezi na kutoa taarifa kwa Mamlaka ya ununuza wa Umma kwa mujibu wa Sheria ya Ununuza ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itatoa mafunzo ya kompyuta na TEKNOHAMA kwa watumishi 30 katika maeneo ya *Basic Computer Application na ICT Security* ili kuwajengea watumishi uwezo wa kutumia kompyuta na mtandao ipasavyo (*e-Competence*). Huduma za Mawasiliano za intaneti, simu za mezani na Tovuti ya Wizara zitaboreshwa. Wizara itaandaa mfumo wa habari ambao utawezesha kupata taarifa mbalimbali na takwimu kutoka taasisi zilizo chini yake. Aidha, Wizara itatayarisha Sera ya Ndani na Mkakati wa Matumizi Bora ya TEKNOHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itadahili wanafunzi 1,665 katika programu za (*IT Basic Certificate 180, Diploma 965 na BEng 520*) na hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 2,715. Aidha, Taasisi itaendeleza wafanyakazi 15 katika masomo ya juu, wakufunzi 8 (Shahada ya Uzamili 4 na Uzamivu 4) na waendeshaji 7 (Shahada ya Uzamili 2 na Stashahada 5). Pia, Taasisi itaendelea kuhudumia wafanyakazi 48 walioko masomoni, wakufunzi 41 (Shahada ya kwanza 3, Shahada ya Uzamili 17, na Uzamivu 21) na waendeshaji 7 (Shahada ya Uzamili 2 na Stashahada 5).

Mheshimiwa Spika, vile vile, Taasisi itaanza kufundisha kozi mpya za Stashahada za *Biomedical Equipment Engineering* (35), *Communication Systems Engineering* (35), *Multimedia Technology* (35) na Stashahada ya Information Technology (35). Aidha, Taasisi itakamilisha taratibu za kuidhinishwa na *NACTE* kozi mpya za stashahada ya *Electronic Equipment Maintenance, Geographical Information System* na *Mechatronics*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi itakarabati na kufunga mitambo katika vituo vitatu (3) vya Habari Jamii vya mradi wa *Super Computer* vilivyoko Morogoro, Mtwara na Dodoma. Pia, Taasisi itakarabati mabweni mawili ya wanafunzi kati ya mabweni sita na barabara za ndani ya Taasisi na eneo la kuegeshea magari. Aidha, Taasisi itakarabati majengo na miundombinu ya maji, umeme na mawasiliano ya kilichokuwa Chuo cha Ngozi Mwanza ili kiweze kupokea jumla ya wanafunzi 60 wa kozi ya Stashahada ya Teknolojia ya Ngozi (30) na Bidhaa za Ngozi (30) katika mwaka wa masomo 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi itakamilisha ujenzi wa Jengo la madarasa, maabara na ofisi za wafanyakazi la *DIT Teaching Tower*. Aidha, Taasisi itaendelea kujitangaza ili kupata zabuni za kutengeneza na kuweka taa za kuongoza magari barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 1,242 hadi kufikia wanafunzi 1,800 ikiwa ni ongezeko la asilimia 45. Aidha, itaanzisha mafunzo ya fani ya Sayansi na Teknolojia ya Maabara na kudahili wanafunzi 25 katika fani hiyo. Taasisi vilevile, itatoa mafunzo ya awali kwa wanafunzi wa kike kwa lengo la kudahili wanafunzi wa kike 35. Pia, Taasisi itaajiri watumishi wapya 30 ili kuendana na uhitaji wa rasilimali watu unaotokana na kupanuka kwa Taasisi. Aidha, Taasisi itaandaa mitaala ya fani za mekatroniki, sayansi na teknolojia ya vyakula, uhandisi usalama, uhandisi elektroniki na mawasiliano na uhandisi madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi itaanza ujenzi wa jengo la maktaba litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,000 kwa wakati mmoja. Aidha, itakamilisha ujenzi wa majengo mawili ya mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 350 kila moja na kufanya ukarabati wa mifumo ya maji na umeme katika majengo manne (4) (*Blocks A, B C na D*). Taasisi pia, itakamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waishio katika eneo la Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi itaanzisha na kuendeleza uhusiano na taasisi mbalimbali za sayansi na teknolojia Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Aidha, Taasisi itafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taasisi unaolenga kuvutia uwekezaji au ufadhili katika maeneo mbalimbali ikiwemo ujenzi wa mabweni ya wanafunzi, nyumba za waalimu, hosteli, migahawa, kituo cha afya, kituo cha mikutano, na kituo cha huduma za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha itakamilisha ujenzi na ukarabati wa majengo ya miadhara, jengo la utawala, mabweni, na majengo ya maabara na karakana; na, miundombinu ya maji, umeme na barabara za Taasisi katika Kampasi ya Tengeru. Aidha, itanunua vitendea kazi na vifaa vya maabara (*Laboratory Equipment, Computers, printers, photocopiers and scanners*) na magari matatu. Pia Taasisi, itadahili wanafunzi kati ya 50 na 100 kwa kuanza masomo mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi itafuatilia upatikanaji wa Hatimiliki ya eneo la Taasisi lililoko Karangai katika Wilaya ya Arusha, itakamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe (*Master Plan*) wa Taasisi kwa eneo la Karangai, itakamilisha uandaaji wa *Charter* ya Taasisi. Aidha, Taasisi itaimarisha uhusiano na ushirikiano na vyuo na asasi mbalimbali nchini, Afrika ya Mashariki na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Sayansi na Teknolojia itasambaza taarifa za matokeo ya utafiti kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na watoa maamuzi ili zitumike katika kutengeneza sera, sheria na mipango. Lengo ni kuwa asilimia 20 ya taarifa zitakazotolewa zitumike na watoa maamuzi. Pia, Tume itaimarisha uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) kwa kuzingatia ushindani, uwazi na uwajibikaji ili uwe madhubuti, unaoaminika na wenye uwezo wa kusimamia vizuri fedha za utafiti ili kuvutia wadau wengine kuchangia Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume itaendelea kuratibu shughuli za utafiti nchini, ikiwa ni pamoja na zile zinazofadhiliwa na Mfuko wa *MTUSATE* na nyingine zinazofanyika nchini ili asilimia 50 au zaidi ya tafiti zinazofanyika ziwe zimelenga au kuzingatia vipaumbele vya taifa vya utafiti ambavyo ni Kilimo na chakula ikijumuisha usindikaji, afya, nishati mbadala, maji, TEKNOHAMA, mawasiliano na uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume itasajili asilimia 50 ya tafiti zote zinazofanyika nchini katika Vyuo Vikuu, taasisi za utafiti na kwingineko, ili kuwa na hifadhi ya taarifa (*data base*) za tafiti katika kituo kimoja. Aidha, itawezesha uhawilishaji wa teknolojia 10 zilizohakikiwa (*proven technologies*) zitakazochangia katika kukuza uchumi. Pia, Tume itaendelea kuelimisha umma juu ya umuhimu wa sayansi, teknolojia na ubunifu na jinsi vinavyochangia katika maendeleo ya nchi. Lengo ni kurusha vipindi 20 katika luninga, vipindi 20 katika redio, makala 24 katika magazeti na kushiriki katika maonesho manane (8) yanayohusu sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki Tanzania itatoa na kuimarisha huduma za kinga ya mionzi ayonisha kwa kukagua na kusimamia vituo 150. Pia, itapima viwango vya mionzi (*Personnel Dosimetry Service*) kwa wafanyakazi 1,300 na kufanya ukaguzi wa vituo vinavyotumia mionzi isiyoyonisha (*non-ionizing radiation*) kwenye minara sabini (70) kwa kushirikiana na TCRA. Vile vile, Tume itaendelea kukusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi na kuyahifadhi katika maabara maalumu *Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF* iliyoko Arusha na

itapima vyanzo vya mionzi katika sampuli za vyakula 5,000 katika mazingira kwenye vituo 26. Aidha, itaendelea na ukaguzi wa migodi ili kubaini hali ya usalama. Vile vile, itaendesha kituo cha kupima mionzi katika mazingira (*Radionuclide Monitoring Station*) kilichopo Dar es Salaam chini ya mkataba wa udhibiti wa matumizi ya silaha za kinyuklia (*Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty of Nuclear Weapons*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume itakamilisha rasimu ya kanuni za uchimbaji salama na usafirishaji wa madini ya urani. Aidha, Tume itaimarisha uwezo kwa kujenga maabara na kuwapatia mafunzo wataalam wa Tume katika viwango vya Shahada ya Uzamili (2), na shahada ya Uzamivu (1); Vile vile, itaimarisha huduma za matengenezo ya vifaa vya elektroniki na mashine za *X-ray* na kuimarisha Kituo cha kutoa mafunzo kwa wafanyakazi katika masuala ya mionzi kwa njia ya kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume itaratibu miradi ya Kitaifa na Kikanda (AFRA) katika Taasisi nane za Kitaifa zinazoghamariwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki na kusimamia mchakato wa kuandaa miradi mipyka kwa kipindi cha mwaka 2011/2013. Pia, Tume itaimarisha uendeshaji wa shughuli na majukumu yake, kwa kuendelea na juhudhi za kuanzisha ofisi ya kanda kwa kuanzia na mkoa wa Ruvuma (Namtumbo) na Zanzibar ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume itafanya utafiti katika migodi ya urani kwa nia ya kubuni na kutekeleza mbinu nzuri za kinga na matumizi salama ya mionzi na kutoa elimu kwa kuendesha semina kwa wafanyakazi wa migodi, viwandani, kilimo, ujenzi wa barabara, idara za *X-ray* na kutoa elimu kwa umma kwa njia ya redio, televisheni juu ya madhara ya uchimbaji, uhifadhi na usafirishaji wa madini ya urani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta Tanzania litaendeleza, kuongeza na kuimarisha matumizi ya TEKNOHAMA katika huduma zitolewazo na Shirika ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa vituo vya mawasiliano ya kisasa *Community Information Centres* ambapo vituo vipyka saba vya intaneti vitaanzishwa. Shirika litaongeza kasi ya kueneza huduma za Posta hadi vijijini ili kukidhi matakwa ya leseni ya kutoa huduma kutoka 358 hadi 367. Aidha, Shirika linatarajia kuongeza vibali vya kuuza stempu na shajala za posta kutoka 2,878 hadi 2,890 na vituo vya intaneti kutoka 23 hadi 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika litaendelea kuboresha muundo wa uongozi na mifumo ya uendeshaji wa Shirika pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi ili wawze kumudu matumizi ya teknolojia katika utendaji kazi. Mafunzo yatakayotolewa ni pamoja na kozi ya muda mfupi kwa watumishi wanane, huduma kwa wateja watumishi 18, TEKNOHAMA kwa watumishi hamsini 50 na utoaji wa huduma za Posta kwa watumishi 108. Pia, Shirika litaendelea kutumia majengo yake kibiashara na kuendeleza mchakato wa kutumia mikopo na wabia kuendeleza viwanja ambavyo havijaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika litakamilisha ujenzi wa uzio wa Posta ya Temeke na kuanzisha ujenzi wa Posta mipyka za Kibondo na Katesh. Pia Shirika litafanya

matengenezo majengo ya ofisi za Posta Kuu za Dar es Salaam, Shangani, Chake Chake, Mwanza, Singida na Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya Simu Tanzania itapanua mtandao wa simu za mikononi na wa data katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Zanzibar, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma na Mbeya, na kuwezesha mawasiliano katika sehemu za barabara kuu (*road coverage*). Miradi hii itajumuisha kuongeza uwezo wa huduma za simu na data kutoka idadi ya wateja 105,000 hadi 356,000 kufikia Juni 2011. Aidha, Shirika litapanua Mtandao wa intaneti (*Fixed Broadband*) kwa kuongeza uwezo wa mitambo kutoka wateja 29,000 waliopo sasa hadi kufikia wateja 43,500 ifikapo Juni, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni itaboresha huduma kwa kuweka mitambo ya *switches* za Kisasa inayotumia teknolojia ya kisasa ya *Next Generation Network* ili kukidhi mahitaji halisi ya kibiashara ya simu na *data*, kwa kuondoa mitambo ya simu ya zamani aina ya *NEAX*, *AXE10*, *DTS* na *GX 5000*. Pia, Kampuni itashiriki katika kusimamia ujenzi, kuendesha, kutunza, na kuendeleza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itaanzisha rejesta ya taarifa za simu (*Central Equipment Identification Register*). Kuwekwa mahali pamoja taarifa zote za simu kutawezesha kuwepo kwa matumizi mazuri ya simu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka itaendelea kuratibu ushiriki wa watoa huduma za Mawasiliano katika ujenzi wa mitambo ya intaneti (*Internet Exchange Points – IXPs*) na kuunganisha mitandao yao kwenye mitambo hiyo. Mamlaka, pia itaendelea kuratibu utekelezaji wa mfumo mpya wa utangazaji wa digitali (*Digital Broadcasting*) kwa kutoa elimu kwa umma na kwa watoa huduma hizo. Aidha, Mamlaka itanunua mitambo miwili ya kuunganisha intaneti katika miji ya Zanzibar na Mbeya, na itaratibu uunganishwaji wa Internet Exchange Points za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania kama ilivyoazimiwa na Umoja wa Wadhibiti wa Mawasiliano na Watoa Huduma ya Mawasiliano ya Simu na Posta Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka itaendelea kupokea na kutathmini maombi ya leseni, kutayarisha na kutoa leseni kwa makampuni yaliyosajiliwa; itaendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa huduma za mawasiliano kwa kuyafanyia ukaguzi makampuni yaliyosajiliwa ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vilivyowekwa kwenye leseni zao. Pia, Mamlaka itaendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu taratibu za kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka pale ambapo hawakuridhika na huduma walizopewa na mtoa huduma. Aidha, Mamlaka itaendelea kushirikiana na wadau wengine katika utekelezaji wa Mradi wa Kitaifa wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta (*New Addressing System and Post Code Project*) katika maeneo ya Zanzibar, Dodoma na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*) utatangaza zabuni ya miradi ya majaribio (*pilot project*) na miradi mikubwa ambayo itawezesha upelekaji wa mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa kufikisha huduma za intaneti kwa kuzingatia kanuni za Mfuko. Mfuko pia, utaratibu ukusanyaji wa takwimu zinazohusu upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa kushirikiana na taasisi zingine. Aidha, Mfuko utaratibu uanzishwaji wa huduma za Posta katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maaazimio na mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inaazimia kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambaao umetilia mkazo katika maeneo ya kuendeleza ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kuhamasisha na kuratibu matumizi yake hadi ngazi ya mtumiaji (*last mile connectivity*). Hii ni pamoja na kuhamasisha juhudhi shirikishi na ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership*) zitakazowezesha kuunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa mashule, hospitali, vyuo, mahakama, na vikundi mbalimbali vya kiuchumi na vya mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGO's*). Faida ya kufanikisha juhudhi hizi ni pamoja na kuziba pengo la uhaba wa walimu pamoja na Madaktari uliopo kupitia elimu mtandao (*e-education*) na afya mtandao (*e-health*) na kuwezesha wakulima kupata taarifa za soko kuhusu mazao wanayolima kwa urahisi zaidi. Aidha, wananchi watapata huduma za mawasiliano kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta ambaao una lengo la kurahisisha upatikanaji wa anuani kamili za makazi zinazoonyesha mitaa, majina ya majengo na uwekaji wa namba za nyumba, mambo ambayo kwa pamoja yatarahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kibiashara na kijamii kama za uokoaji wakati wa dharura za: utoaji wa huduma ya gari la wagonjwa, maji, umeme na mawasiliano; ugawaji misaada na ukusanyaji wa kodi mbalimbali za Serikali. Mambo mengine yatakayofanywa kwa urahisi ni pamoja na utambuaji wa wananchi kupitia Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi (*RITA*), uandikishaji wapiga kura, utoaji wa vitambulisho vya mkazi kupitia Mamlaka ya Vitambulisho Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaelekeza juhudhi zake pia katika ujenzi wa Kituo cha Kutunza kumbukumbu za TEKNOHAMA (*Mega Data Centre*). Kituo hiki kitaimarisha mawasiliano ya kimtandao ya ndani ya nchi na nje ya nchi na kitatoa mchango mkubwa katika kuendeleza utafiti, ubunifu, na uvumbuzi wa kisayansi na kiteknolojia. Pia, Kituo hiki kitaliingizia Taifa mapato kutokana na huduma za kuhifadhi taarifa na kumbukumbu kitakacho zitoa kwa watumiaji mbalimbali yakiwemo mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itajielekeza katika kuimarisha, kupanua na kuendeleza Taasisi za Sayansi na Teknolojia zilizo chini ya Wizara, kwa lengo la kutoa wataalam wengi zaidi katika fani ya Sayansi na Teknolojia. Hii ni pamoja na kukamilisha ukarabati na taratibu za uanzishwaji wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson

Mandela, Arusha. Aidha, Serikali itapitia na kuboresha mfumo wa sayansi na teknolojia na ubunifu nchini (*National Innovation System Reform*) kwa kushirikiana na UNESCO.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea na juhudzi za kuenga fedha inazopata katika kugharamia shughuli za Utafiti na Maendeleo ili kufikia angalau asilimia 1.0 ya Pato Ghafi la Taifa (*GDP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, jitihada zitaelekezwa katika kuongeza nguvu katika shughuli za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza rasilimali za Mfuko ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano hasa katika sehemu ambazo hazina mvuto wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itakamilisha Kanuni za Uchimbaji na Matumizi ya Madini yanayotoa mionzi ili shughuli hiyo ifanywe kwa usalama na iweze kuleta manufaa katika maendeleo ya Tanzania hasa wakati huu ambapo kuna uwezekano mkubwa wa kuanza kuchimbwa kwa madini ya urani nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea na jitihada za kuimarisha uwezo wa Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania kwa kulipa malimbikizo ya madeni ya Serikali yatokanayo na huduma zilizotolewa na Mashirika hayo pamoja na kuangalia uwezekano wa Serikali kutoa dhamana ili asasi hizi ziweze kuchukua mikopo yenye masharti nafuu na hivyo kuyaongezea uwezo wa kupanua, kuendeleza na kutoa msukumo zaidi wa kufikisha huduma za Mashirika haya hadi vijijini na kwenye maeneo ambayo hayana mvuto mkubwa wa kibiashara kwa sekta binafsi kuingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wadau na wahisani mbalimbali kwa michango yao mikubwa katika Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wahisani hao ni pamoja na Marekani, Sweden, Norway, Finland, Uhlanzi, Japan, Jamhuri ya Korea ya Kusini, China, India, Benki ya Dunia, Umoja wa Mataifa na UNESCO. Mashirika mengine ni pamoja na Jumuiya ya Madola, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani na *Third World Academy of Sciences, International Foundation for Sciences*. Mashirika haya yameonesha nia ya dhati kusaidia maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wizara inaahidi kuendeleza ushirikiano huu. Aidha, naishukuru sekta binafsi kwa mchango wao katika kuendeleza sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia na hivyo kuongeza mchango wa sekta hii katika maendeleo ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha Wizara yangu kutekeleza mipango iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2010/2011, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.71,017,600,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Sh.26,590,690,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yaani mishahara na matumizi mengineyo, ambapo Sh 15,290,382,000 ni kwa ajili ya Mishahara na Sh.11,300,308,000 ni kwa ajili ya Matumizi mengiyo na Sh.44,426,910,000 ni kwa ajili ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo Sh.42,426,910,000 ni fedha za ndani na Sh. 2,000,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, wenye viti wa Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu. Aidha, pamoja na hotuba hii kuwepo katika vitabu tunavyovitumia hapa Bungeni leo, hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara ambayo ni www.mst.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Hoja hii imeungwa mkono, sasa tunaendelea na hatua inayofuata. Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na Wizara hii. Unajua kufuatana na Kanuni siyo lazima wasimame Mawaziri, tu kwa hiyo wanaweza kusimama na watu wengine. Kwa hiyo, kama mmesimama wengi mmefanya vizuri. Wakati wa kusimama Mawaziri tu ulikuwa wa Chama kimoja. (*Makofi*)

MHE. ALHAJ MOHAMMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu Taarifa ya Kamati, kuhusu utekelezaji wa Bajeti wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea naomba nichukue nafasi hii kutoa rambirambi. Kwa taarifa ambazo tumezipata asubuhi hii ni kwamba, yale matangazo ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa jana, kuhusu ile ajali ya ndege, yule kiongozi Meja anatoka kwenye Jimbo langu, kwenye Kijiji cha Minyughe. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kutoa rambirambi zangu na pole sana kwa familia ya kijana huyu pamoja na yule mwenzake na tumwombe Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hawa peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati yangu kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 kuhusu utekelezaji wa Bajeti wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi kwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa maandalizi na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hii mbele ya Kamati kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya 2010/2011. Aidha, Wizara iliwasilisha pia Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati na Mipango ya Bajeti ya mwaka uliopita wa 2009/2011 na kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii Kamati ilipata fursa ya kujadili:-

- Utekelezaji wa Malengo yake kwa mwaka 2009/2010 na malengo yanaoombewa Bajeti kwa mwaka 2010/2011;

- Muhtasari wa mgawanyo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Idara na Taasisi kwa Mwaka 2009/2010;

- Utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya mwaka 2009/2010; na

- Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 Kamati ilitoa maagizo 25 kwa ajili ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha. Kamati iliridhika na utekelezaji wa maagizo hayo, kwani maagizo mengi yalitekelezwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa malengo, ambayo hayakutekelezwa ni kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Wizara, ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha na mambo yanayohitaji kufanyiwa utafiti wa kiufundi na mipango ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2009/2010. Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010 Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Sh. 602,000/= kama Mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi 2010, Wizara ilikusanya jumla ya Sh. 56,877,146/=, ambazo sehemu kubwa ya fedha hizo zilitokana na mauzo ya nyaraka za zabuni mbalimbali ikiwa ni ongezeko la asilimia 9,448 ya makisio kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilitarajia kutumia jumla ya Sh. 24,267,464,000/=, kati ya fedha hizo sh.10,512,134,100/= ni kwa ajili ya mishahara na sh. 13,755,329,900/= kwa ajili ya matumizi mengineyo hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010 jumla ya sh. 9,517,118,160/= kwa ajili mishahara zilikuwa zimetolewa na sh. 10,719,193,586/= kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 ziliidhinishwa jumla ya sh. 14,410,166,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo; kati ya fedha hizo sh.13,962,842,000/= zilikuwa ni fedha za ndani na Sh. 447,410,166,000/= zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Mei 2010 jumla ya Sh. 10,140,366,413/= zilizopokelewa, kati ya fedha hizo Sh. 9,562,842,000/= zilikuwa ni fedha za ndani na Sh. 577,524,413 /= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na teknolojia imefanikiwa kutekeleza majukumu mengi ikiwemo haya yafuatayo:-

- Wizara imetekeliza maagizo ya yote ya Kamati licha ya kukabiliwa na uhaba wa fedha katika utekelezaji wa majukumu yake.
- Kuratibu na kusimamia ujenzi wa Mkongo wa Taifa.
- Kukamilisha uanzishaji vituo vitano (5) vya Mawasiliano katika mikoa ya Pwani, Dodoma, Kaskazini Pemba, Iringa na Mbeya.
- Kuendeleza ujenzi wa Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam.
- Ujenzi wa Makao Makuu ya Tume ya Nguvu za Atomiki ya Tanzania.
- Kuendeleza ukarabati wa jengo la Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia.
- Kutunga Sheria Mpya ya mawasiliano ya Ki-elektroniki (*The Bill of Electronic and Postal Communication Act, 2010*) iliyopitishwa katika Mkutano wa 18 wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana zilikuwepo pia changamoto ambazo Wizara ilikutana nazo, ikiwa ni pamoja na:-

- Kutokuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti na maendeleo. Aidha, kutotekeliza kwa ahadi ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete ya kutenga asilimia moja ya pato ghafi la bajeti ya kwa ajili ya shughuli za utafiti.
- Kushindwa kupeleka kwa wananchi matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kwa ajili ya kuyatumia ikiwa ni pamoja na kutozalisha bidhaa zilizobuniwa na wagunduzi wa Kitanzania na hivyo kujenga picha kuwa hapa nchini hakuna wagunduzi wala watafiti.
- Uhaba wa raslimali watu kwenye sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia. Aidha, wataalam wengi waliopo wana umri mkubwa, kutokuwa na uwiano wa kada ya wahandisi na mafundi wa ngazi za cheti na diploma ikiwemo wengi wao kutokuwa na uelewa wa teknolojia mpya.
- Uelewa mdogo wa namna masuala ya sayansi na teknolojia yanavyohusiana moja kwa moja na maendeleo ya uthumi wa nchi yetu hivyo elimu zaidi inahitajika kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Kutokuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maendeleo iliyokwishaanzishwa ikiwemo:-

- Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambao hautengewi fedha za ndani za kutosha;

- Ukamilishaji wa Mfumo wa Anwani za makazi na simbo za Posta ambao pia utasaidia mkakati wa utoaji wa vitambulisho na utarahisisha ukusanyaji wa kodi ya majengo pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali;

- Ujenzi na ukarabati wa Taasisi za Sayansi na Teknolojia kama vile Chuo cha Ngozi Mwanza, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya na kadhalika;

- Kukosekana kwa sheria na uratibu wa matumizi ya miundombinu kwa ajili ya watoa huduma za misingi ya kijamii (*Public utility services*);

- Kutokuwepo kwa mfuko maalum ya kuendeleza wagunduzi, wavumbuzi na vijana wenye vipaji;

- Kutokuwepo Sera ya Taifa ya Miliki Ubunifu nchini (*Intellectual Property Rights*);

- Kutokuwa na Wataalam wa kutosha katika baadhi ya maeneo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; na

- Kutokuwa na mazingira ya kuibua na kuendeleza vipaji vya ubunifu na uvumbuzi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kujiwekea mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo, ikiwa ni pamoja na:-

- Kupanua wigo wa mifuko ya Fedha za utafiti kwa njia ya Taasisi kushirikiana na Sekta mbalimbali za Kijamii na za Kiuchumi kwa lengo la kupanua ufadhilli;

- Kuhuisha mfumo mzima wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini ili kuleta usimamizi mzuri na ufanisi;

- Kuanzisha mfumo wa Sheria unaofaa kwa maendeleo na uhawilishaji wa teknolojia ikiwemo haki za ubunifu, ufuataliaji na udhibiti wa uchaguzi na uhawilishaji wa teknolojia pamoja na usalama wa viumbe;

- Kuanzisha vituo vipya vya Sayansi na Teknolojia vyenye lengo la kutoa elimu katika ngazi mbalimbali pamoja na Uzamili na Uzamivu na kuwa na utaratibu wa kuwabakiza katika utumishi wa Wizara *retention scheme*; na

- Kuanzisha utaratibu wa utambulishaji, ukuzaji na uendelezaji wa vipaji maalumu, na uwezo wa sayansi na teknolojia mionganoni mwa Watanzania, hasa vijana kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2010/2011, Wizara ilizingatia Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti (*MTEF 2009/2010-2011/2012*) uliotolewa

na Wizara ya Fedha na Uchumi, Mpango Mkakati wa Wizara (*Medium Term Strategic Plan*), maelekezo na malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Dira ya Taifa ya Maendeleo – 2025, Sera ya Sayansi na Teknolojia, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA), Sera ya Taifa ya Mawasiliano kwa Simu pamoja na Sera ya Taifa ya Posta na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa na Wizara ya Mawasiliano zimegaiwa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Hivyo basi, fedha kiasi cha sh. bilioni 71,921,932,142/= katika Mwaka wa fedha wa 2010/2011 zinaombwa kwa ajili kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- Kuendelea na mchakato kwa kushirikiana na Wadau wote wa ndani na nje wa kujenga, kuimarisha na kuendeleza matumizi ya huduma za mtandao wa teknolojia ya habari na mawasiliano – TEKNOHAMA nchini.

- Ukamilishaji wa uanzishaji na uendeshaji wa Mfuko Maalum wa kufanikisha maendeleo ya huduma za mawasiliano kwa wote nchini.

- Utekelezaji wa miradi ya mawasiliano, Posta, vituo vya mawasiliano (*telecentres*) hususan sehemu za vijiji kwa lengo la kupunguza umaskini na kuongeza ajira.

- Uanzishwaji na uimarishaji wa huduma za Tovuti na Barua Pepe vijiji kama sehemu ya programu ya ujenzi wa Jamii Habari na uelewa (*information/knowledge Society*).

- Kufanya upembuzi yakini na kufunga Mtandao wa Mawasiliano wa Elimu na Utafiti (*National Research and Education Network*) katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti zilizoko Dar es Salaam na Zanzibar chini ya udhamini wa Benki ya Dunia.

- Kuratibu tafiti za kisayansi katika maeneo yenyе kipaumbele Kitaifa (kilimo na chakula, viwanda, nishati, maliasili na mazingira).

- Kuandaa Benki ya Takwimu (*Database*) ya wanasyansi nchini kwa ajili ya kubaini fani zao na kiwango cha elimu walichofikia na maeneo wanayofanyia utafiti.

- Kuanzisha vituo vipyा vya Sayansi na Teknolojia, kuhuishwa mfumo wa Sayansi, Teknolojia na ubunifu nchini kwa kushirikiana na (UNESCO).

- Kuendelea na Ukaguzi wa Vituo vya matumizi ya mionzi isiyoayonisha ikiwemo minara 70 ya simu za mikononi na radio.

- Kuongeza idadi ya wanafunzi, kuboresha mitaala ya mafunzo na kuvijengea uwezo Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*) na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*).

- Kuimarisha Uongozi na uendeshaji wa Wizara, kuwaendeleza Wafanyakazi katika mafunzo na kuwajengea mazingira mazuri ya utendaji kazi.

- Kuendeleza ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kuhamasisha na kuratibu matumizi yake hadi kufikia ngazi ya mtumiaji.

- Uanzishwa wa Anwani za Makazi na Simbo za Posta ambao una lengo la kurahisisha upatikanaji wa anuani kamili za makazi zinazoonyesha mitaa, majina ya majengo na uwekaji wa namba za nyumba, mambo ambayo kwa pamoja yatawezesha upatikanaji wa anuani ya mwananchi na hivyo kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kibiashara na kijamii.

- Ujenzi wa Kituo cha kutunza kumbukumbu za TEKNOHAMA (*MEGADATA CENTRE*) kitakachoimarisha mawasiliano ya kimtandao ya ndani na nje ya nchi na kuliingizia mapato Taifa kutoka na huduma zitakazotolewa na kituo hiki.

- Kuimarisha, kupanua na kuendeleza Taasisi za Sayansi na Teknolojia zilizo chini ya Wizara kwa lengo la kutoa wataalamu wengi zaidi katika fani ya Sayansi na Teknolojia.

- Kuongeza nguvu katika shughuli za mfuko wa mawasiliano kwa wote kwa kushirikiana na sekta ya binafsi kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma za mawasiliano.

- Kukamilisha kanuni za uchimbaji na matumizi ya madini yanayotoa mionzi ili shughuli hiyo iweze kuleta manufaa katika maendeleo ya nchini yetu hasa wakati huu ambapo kuna uwezekano mkubwa wa kuanza kuchimbwa kwa madini ya urani.

- Kuimarisha uwezo wa Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) na Shirika la Posta Tanzania (*TPC*) kwa kulipa malimbikizo ya madeni ya Serikali yatokanayo na huduma zilizotolewa na Taasisi hizo pamoja na kutoa dhamana ya Serikali ili kuchukua mikopo yenye masharti nafuu, hivyo kupanua, kuendeleza na kutoa msukumo wa kufikisha huduma unganishi za mawasiliano hadi vijijini na maeneo ambayo hayana mwelekeo wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inakadiriwa kuwa na matumizi ya sh. bilioni 71,921,932,142/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara imetengewa jumla ya sh. bilioni 26,590,690,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida,

ambapo sh. bilioni 15,290,382,000/= kwa ajili ya kulipia mishahara ya Watumishi wa Mashirika na sh. bilioni 11,300,308,000/= ni fedha za Matumizi Mengineyo (*OC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara imetengewa sh. bilioni Sh. bilioni 45,331,242,142/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya hizo Sh. bilioni 42,426,910,000/= ni fedha za ndani na Sh. bilioni 2,904,332,142/= ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuijadili Mpango na Bajeti hiyo kwa kina, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla. Serikali ianze miradi baada ya kufanya utafiti wa kutosha kuhusu uwezekano wa kuitekeleza kikamilifu bila kuishia njiani na hivyo kushindwa kupata matokeo yaliyokusudiwa na kupoteza fedha, ambazo zingetumika katika utekelezaji wa miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kubuni mikakati ya kupata fedha za ndani ili kuiwezesha Wizara hii kutekeleza mipango ya miradi ya maendeleo kama ilivyojipangia bila kutegemea fedha za Wafadhili. Uzoefu umedhihirisha kuwa fedha za kutoka nje kwa Wafadhili hucheleva kupatikana kwa muda muafaka na hivyo kuchelewesha baadhi ya miradi inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa Kamati imebaini kwamba ushauri wa Bunge uliokubaliwa na Serikali wa kuliokoa Shirika la Posta katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 haujatekelezwa kikamilifu, ushauri huo unakwamishwa na urasimu mkubwa wa Hazina. Kulikoni? Kamati inasisitiza kuwa ushauri huo utekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inasikitishwa na kusuasua kwa mradi wa Anuani Mpya za Makazi na Simbo za Posta, ambapo kwa mwaka 2009/2010 ulifanywa kwa majaribio katika Kata saba (7) katika Manispaa ya Mji wa Arusha tu. Awali mradi huo ulikusudiwa kufanyiwa majaribio katika Mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Singida, Dar es Salaam na Zanzibar. Hata hivyo katika Bajeti ya 2010/2011 hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili kuendeleza mradi huo kwa mwaka huu wa fedha. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha na kukamilisha mradi huu kama ilivyoazimiwa kwa ajili ya kuharakisha maendeleo, kwani ikizingatiwa ukubwa wa nchi yetu ukamilishaji wa mradi huu unaweza kuchukua miaka minge na hivyo kuongeza gharama ya mradi huu bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali ili kukamilisha mapema mradi wa Anuani Mpya za Makazi na Simbo za Posta na kuleta ufanisi; Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani na TAMISEMI, kwa vile mradi huu ukikamilika utasaidia kufanikisha mradi wa vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kuimarisha Shirika la Posta nchini kwa kulipatia mtaji utakaowezesha kuweka mitandao ya *internet* katika utoaji wa huduma zake ili kuhimili ushindani unaotokana na mabadiliko ya teknolojia, ambapo

watu binafsi wamejiingiza katika biashara ambazo zilikuwa zinafanywa na Shirika hilo peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kuhakikisha kuwa agizo la Mheshimiwa Rais la madeni ya Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) na Shirika la Posta Tanzania (*TPC*) linatekelezwa. Madeni ya Shirika la Posta ya Mfuko wa Pensheni za Mashirika ya Umma (*PPF*) sh. 19,548,583,570/=; deni la Pensheni za Wafanyakazi waliokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki sh. 8,200,000,000/= na kulirejeshea Shirika la Posta sh. 2,117,997,680/=, ambazo ni fedha zake za kuendeshea Shirika. Madeni hayo yalipwe ili kuепusha usumbufu kwa Wafanyakazi wanaostaifu na kuwezesha Shirika kijiendesha kibashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali ifanye juhudzi za makusudi za kuikwamua Kampuni ya Simu Tanzania kifedha na kiutendaji kwa kuidhamini ili iweze kukopeshwa kiasi cha US\$ Milioni 180.1 zinazohitajika kwa ajili ya Mpango Mkakati wa Biashara (*Strategic Business Plan*) wa miaka mitatu (2010-2012). Aidha, Hazina ihakikishe kuwa Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali zinalipa malimbikizo yote ya madeni yanayotokana na matumizi ya simu za *TTCL* ili Kampuni hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Wizara na Taasisi zitakazokaidi kulipa madeni; basi Hazina wawakate moja kwa moja kutoka katika *OC* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroni na Posta ya mwaka 2010, Kamati inaishauri Wizara kukamilisha mapema iwezekanavyo Kanuni ili kuiwezesha Sheria hiyo kutekelezeka. Kamati inaipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) kwa kuendesha vizuri zoezi la usajili wa namba za simu za mikononi (*Sim Cards*). Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka hiyo, Kamati inashauri kuwa juhudzi ziongezwe hasa za kufikisha taarifa za mwisho wa usajili wa namba hizo kuwa ni tarehe 30 Juni, 2010 kama ilivyotangazwa hapo awali.

Naishukuru Serikali kwamba imeona ni afadhali kuongeza kwa busara zake nampongeza hatua hiyo matumaini yangu ni kwamba wananchi wataitikia ili ifikapo tarehe 15 Julai tuwe tayari tumeshasajili simu zetu. Kwani kutokana na maeneo mengine kuwa pembezoni na kutokuwa na njia za mawasiliano za uhakika huenda tangazo hilo la tarehe ya mwisho ya usajili isiwafike walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee Kamati yangu inayapongeza Makampuni ya Simu za Mikononi kwa jitihada zao za kupanua huduma za mawasiliano ya simu hadi vijijini. Aidha, makampuni haya yamekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa Wananchi wanafikishiwa huduma ya usajili wa kadi za simu hadi maeneo waliyopo, hii imetoa fursa nzuri kwa wateja hao wengi kusajili simu zao. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kufuta kodi na tozo mbalimbali, ambazo zinazochangia kumwongezea mteja wa mwisho gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kukamilika kwa Mkongo wa mawasiliano nchini kutasaidia sana kuongeza ufanisi katika sekta ya mawasiliano na kwa kuwa Mkongo huo bado haujakamilika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudzi za

makusudi ili mradi huo ukamili. Pamoja na kuimarisha huduma za mawasiliano, Mkongo huo utasaidia katika kupunguza gharama kwa watumiaji wa simu za mikononi. Kamati pia inashauri kuwa Mkandarasi anayeteuliwa aajiri watu au vijana wa eneo husika na sio kuajiri kutoka nje ya Wilaya au Mkoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuweka juhudzi za makusudi ili kuinua maendeleo ya sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) nchini, na kwamba elimu hiyo iingizwe kwenye mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu nchini. Hii itasaidia kupata kizazi kijacho chenye Wataalam wa uhakika katika kusukuma maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukua kwa kasi kwa mabadiliko ya teknolojia, na ili kuingia katika mfumo huo na kwenda na wakati, Serikali haina budi kuwa na mkakati maalum wa kujenga miundombinu na kutumia nishati mbadala pale ambapo hakuna umeme wa uhakika kuwezesha TEKNOHAMA kusambaa hadi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mgogoro wa ardhi katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha katika eneo jipya unatatuliwa; na kwamba Serikali ikamilishe malipo ya fidia kwa Wananchi waliohamishwa ili kupisha ujenzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na mahusiano mazuri na kati ya chuo na Wananchi, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Moshono – Nambala na Nambala – Tengeru ili kurahisisha mawasiliano na huduma za kijamii kuwafikia Wananchi kirahisi. Hili linawezekana kwani, Serikali iliweza kufanya hivyo Chuo Kikuu Cha Dodoma (barabara ya Dodoma Mjini – Chuo Kikuu cha Dodoma) na Chuo Kikuu cha Mzumbe (barabara ya Sangasanga – Mzumbe) ili kuendana na hadhi ya Taasisi hii pamoja na umuhimu wake Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna Watanzania wenyewe vipaji vya ugunduzi, Kamati inaishauri Serikali ifanye juhudzi za makusudi za kuhamasisha ugunduzi huo kwa kutunga sera maalum na sheria ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazogunduliwa (*prototypes*) zinatengenezwa kwa wingi kwa ajili ya matumizi ya wananchi, hii itaokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, Wanataluma wa Taasisi za Teknolojia za Dar es Salaam (*DIT*) na Mbeya (*MIST*) wameweza kutengeneza taa za kuongozea magari barabarani, lakini hawajapewa fursa ya kuzalisha kwa wingi kwa ajili ya matumizi ya barabara zetu. Aidha, Jeshi la Wananchi wa Tanzania wameweza kutengeneza magari yaliyopewa jina la “Nyumbu”, lakini bado hakuna uhamasishaji na uwezeshwaji wa kutosha kuwatia moyo wagunduzi hao ili kuzalisha bidhaa hizo kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inasisitiza kuwa elimu ya Sayansi iimarishe katika shule za msingi pamoja na sekondari; ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa Walimu wa masomo ya sayansi na kujengwa kwa maabara ili kuwaandaa vijana kwa ajili ya masomo ya sayansi na sio kungojea hatua ya vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2001 (*Public Procurement Act, 2004*) ni kikwazo kwa maendeleo ya ugunduzi hapa nchini kwani kila ununuzi lazima ufanywe baada ya kupitia mchakato wa zabuni. Kwa kuwa Taasisi zetu zinazofanya ugunduzi hazina uwezo wa kushindana na Wazabuni kutoka nje ya nchi; Kamati inaishauri Serikali kutoa maelekezo maalum kwa Wizara, Idara, Mashirika, Taasisi, Halmashauri na wengineo kutumia bidhaa zinazotokana na ugunduzi wa ndani kama ilivyofanya nchi ya India, ambayo mpaka sasa magari yote ya Serikali ni yale yalijotengenezwa nchini humo. Hii itaongeza soko la ndani na kuokoa fedha zinazotumika kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipewa maelezo kuwa fedha za matumizi mengineyo (*Other charges*) zimepungua zikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita kutokana na maelekezo ya kuondoa ununuzi wa magari katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2010/2011. Pamoja na nia nzuri ya Serikali, Kamati inaishauri kuwa, maelekezo hayo yatolewe kwa kuzingatia hali halisi ya Taasisi husika. Kwa mfano, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha ni mpya na uongozi wake umeteuliwa hivi karibuni, ni dhahiri kuwa hawana vitendea kazi ikiwemo magari. Pamoja na kubana matumizi chuo hiki kipewe upendeleo wa pekee ili kiweze kupata magari na vitendea kazi muhimu ili kuendeshea shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nchi zilizoendelea ugunduzi wa kisayansi unafanywa na Majeshi, Vyuo Vikuu na Taasisi za Sayansi na Teknolojia unastahili kupewa kipaumbele. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira mazuri na kuzijengea uwezo wa kifedha Taasisi zetu, kujenga maabara za kisasa zenye vifaa na mashine za kutosha kuwawezesha Wahandisi na Wataalam wetu kufanya kazi zao za kiutafiti; kujenga karakana zenye sifa na viwango; kwani katika Taasisi zetu majengo, vifaa na mashine zilizopo ni chakavu na zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ianzе utaratibu wa kusajili na kulinda (*patenting and protecting*) hakimiliki za matokeo ya ubunifu kwa Watafiti. Itungwe sheria ya kulinda hakimiliki ili kuwapa nguvu Wagunduzi na kulinda ugunduzi wao. Aidha, Serikali ianzishe mfuko maalum wa kuendeleza Wagunduzi, Wavumbuzi na Vijana wenye vipaji. Hili liende sambamba na uanzishwaji wa shule maalum za vijana wenye vipaji ili kuimarisha nyanja za ugunduzi na uvumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuinua shughuli za utafiti hapa nchini Kamati inasisisitiza utekelezaji wa agizo la Rais la kutenga asilimia moja (1%) ya Pato Ghafi la Taifa kwa ajili ya shughuli za utafiti. Aidha, ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa tija na kwa lengo lililokusudiwa fedha zote za utafiti ziratibiwe na Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Sheria iliyoanzisha Tume hiyo irekebishwe ili iweze kutekeleza jukumu hilo jipya ipasavyo. Inasikitisha sana kuwa mpaka leo hii Tanzania inaagiza vijiti vya kuchokonolea meno (*toothpick*) kutoka nje ya Tanzania wakati nchi ina neema ya miti na mbaa nydingi na nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali iendelee kutoa elimu na kuimarisha huduma za kinga ya mionzi kwa Wananchi na kutoa huduma ya upimaji wa mionzi (*Personnel Dosimetry Service*). Aidha, katika mwaka huu wa fedha Serikali haikutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa chombo cha kuhifadhi mionzi. Wakati kwa mwaka 2009/2010 zilitengwa shilingi bilioni moja kwa ajili hiyo, ambapo zilitolewa shilingi milioni 450 tu ambazo nazo zilikuwa ni chini ya nusu ya kiasi kilichotakiwa, hii inakwamisha taasisi husika kufikia malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia iweze kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka 2010/2011, inaomba iidhinishiwe jumla ya sh. 71,017,600,000/=. Kati ya hizo fedha za Matumizi ya Kawaida ni sh. 26,590,690,000/=, ambapo sh. 15,290,382,000/= ni fedha za mishahara na sh. 11,300,308,000/= ni fedha za Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Bajeti ya Maendeleo zinazoombwa ni sh. 44,426,910,000/=. kati ya hizo sh. 42,426,910,000/= ni fedha za ndani na sh. 2,000,000,000/= ni fedha za Nje. Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na kupitia kifungu kwa kifungu na kuridhika nayo na sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kupitisha maombi hayo yenye jumla ya sh. 71,017,600,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Aidha, nawashukuru pia Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Dr. Florens M. Turuka Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; pamoa na Wataalam wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao umeiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha Taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa. Ushirikiano wao na kujituma bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha Taarifa hii, ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Alhaji Mohammed Hamisi, MissangaMwenyekiti; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mjumbe; Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mjumbe; Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mjumbe; Mheshimiwa Paschal Costantine Degera, Mjumbe; Mheshimiwa

Bakar Shamis Faki, Mjumbe; Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mjumbe; Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mjumbe; Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mjumbe; Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mjumbe; Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mjumbe; Mheshimiwa Herbet James Mntangi, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Gertrude Ibengwa Mongella, Mjumbe; Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mjumbe; Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mjumbe; Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mjumbe; Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi, Mjumbe na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninawashukuru sana Wajumbe hawa wa Kamati ya Miundombinu kwa imani yao kwangu kwa kipindi chote cha miaka mitano (5) na kwa ushirikiano wa hali na mali walionipa. Namwomba Mwenyezi Mungu Wajumbe hawa pamoja na mimi *Inshallah* atujalie tushinde uchaguzi mkuu ujao na kuturudisha katika Bunge lijalo tuendelee kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Didimu Kashilillah, Makatibu wa Kamati Ndugu Justina Mwaja Shauri na Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, shukrani za pekee ziwaendee wapigakura wangu wa Jimbo la Singida Kusini kwa kuniamini, kwa muda wa miaka 10 na kwa kushirikiana kupata maendeleo ya kuridhisha hadi sasa Jimbo la Singida Kusini limegawanywa kuwa Majimbo mawili; yaani Singida Magharibi na Singida Mashariki. Nawaomba Wananchi wa Singida Magharibi waendelee kuniamini katika mitano ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika hoja hii.

MHE. SAID A. ARFI – MSEMADI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa Bungeni tukiwa hai na wazima. Pili, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia. Kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 99(3) na (7), toleo la mwaka 2007, na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed pamoja na Naibu wake Dr. Slaa kwa msaada na ushauri walionipa kutekeleza vyema kazi zangu kama Waziri kivuli wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Nimejitahidi kadri ya uwezo wangu wote na kuonyesha kuwa hawakukosea katika uteuzi huu. Vile vile nawashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Kati kwa ushirikiano walionipa kwa muda wote wa utumishi wangu kwao na kunivumilia katika kufanya kazi yangu vizuri, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu.

Nawaahidi kuwa nitakuwa nao na sitapoteza imani yao kwangu na kwa chama changu CHADEMA ambacho nitumaini la Watanzania. Ni matumaini yangu kwamba hawatakosea na kufanya kosa ili tukamilishe yale tulioanza kwa pamoja kwani Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kikwete alipata kuwaambia wananchi wa Mpanda: “Tunajenga nyumba moja ya nini kugombania fito”. Yeye atasema na sisi tutafanya ni dhahiri kwamba mwenye macho haambiwi tazama, kwa mabadiliko makubwa na maendeleo yaliyopatikana katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda, Mbunge mwenzangu wa Mpanda Mashariki kwa ushirikiano alionipa na kwa kauli yake ya kiungwana kwa wananchi wa Mpanda kuwa nimekuwa msaada mkubwa sana kwake ye ye katika kuwasilisha matatizo ya Mpanda na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu sasa kuwashukuru sana wananchi na wapiga kura wa Jimbo la Mpanda Kati, viongozi wa ngazi mbalimbali wa Serikali na Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini kwa dhati kabisa nisiwasahau kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa kwa ushirikiano walionipa. Tanzania ni yetu sote, tutajenga pamoja kwa pamoja tunaweza. Sitawaangusha wala kuwasaliti wananchi wa Mpanda kwa heshima kubwa walionipa ya kuwatumikia na kuwasemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Msolla, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara na Tasisi zake kwa ushirikiano walionipa wakati wote na juhudhi wanazozifanya kuhakikisha mawasiliano yanafika nchini kote. Wahenga walisema mkono hujikuna unapofika, pamoja na changamoto zilizopo msikate tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Bunge kwa namna mlivyoendesha vikao vyote kwa umahiri na ustadi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika taarifa zake za mwaka wa fedha uliopita za utekelezaji ilionyesha kuwa imetengeneza mpango wa utekelezaji (*Action plan*) pamoja na mikakati kwa sera mbalimbali kutumika pindi tu zitakapopitishwa na mamlaka husika. Sera hizo ni:-

- Sera ya TEKNOHAMA;
- Sera ya Taifa ya Utafiti;
- Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia;
- Sera ya Taifa ya Nyuklia; na
- Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia Ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kupidishwa kwa sera si tatizo bali tatizo ni bajeti ya utekelezaji wa sera hizo. Kitaaluma ni kwamba haiwezekani kuwa na mpango wa utekelezaji bila ya kuwa na bajeti ya utekelezaji. Tuliishauri Wizara kuzingatia uwezo wa kutekeleza mipango yake. Ni vyema sasa Wizara ikatueleza hatua ilizochukua na mafanikio yaliyopatikana hadi sasa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka kipaumbele ni sera ipi inaweza kutekelezwa kwa haraka na kuleta tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuzingatia uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo ya fedha yanayoikabili Wizara, Kambi ya Upinzani haikuridhishwa na fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha kwa Wizara hii na tunajiuliza kama dhamira na utashi wa kisiasa upo wa kuipeleka nchi hii katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Kambi ya Upinzani inayo mashaka makubwa kama mafanikio yanayokusudiwa kwa kasi zaidi kama wanavyotaka tuamini iwapo maeneo ya kuchochea kukuza na kusukuma maendeleo hayakutengewa fedha za kutosha na hasa wakati hazina inaposhindwa kupeleka fedha kwa wakati kama zinavyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yetu ya mwaka jana tulieleza nanukuu: “Kambi ya Upinzani inasikitishwa na namna maagizo ya Rais yanavyopuuzwa na watendaji hususan Hazina. Rais aliagiza tarehe 17.2.2009 itengwe asilimia moja ya pato ghafi la Taifa kwa ajili ya utafiti na kuratibiwa na Wizara hii yenye dhamana juu ya sayansi na teknolojia.” Mwisho wa kunukuu. Aidha, Kambi ya Upinzani ilipendekeza hiyo asilimia moja ya pato ghafi la Taifa iende Tume ya sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Kambi ya Upinzani imefarijika Serikali kuzingatia ombi letu, hata hivyo pesa iliyotolewa si asilimia moja ya pato ghafi la Taifa (*GDP*), hivi ni mpaka lini Rais ataendelea kupuuzwa na watendaji ambao kwa dharau kubwa wameshindwa kutekeleza agizo la Rais wetu au tukubali kuwa huo ni mwendelezo wa maagizo yasiyotekelze? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA). Mfuko wa Mawasiliano. Mfuko huu ambao unatunishwa kwa pamoja na sekta binafsi na Serikali utasaidia juhudhi za kufikisha mawasiliano katika maeneo ambayo yasiyo na mvuto wa kibashara. Pamoja na mengine utachangia katika ujenzi wa minara, kupunguza gharama za maunganisho ya simu na kuhamasisha matumizi ya simu za viganjani, mawasiliano ya intaneti, kupeleka huduma za utangazaji kupertia radio za jamii na kuongeza mtandao wa huduma za posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wamechoka kusikiliza maneno matamu, wanachohitaji ni utekelezaji wa hayo ambayo yanaweza yakabadilisha maisha yao.

Kambi ya Upinzani inahitaji maelezo ya fedha zilizotengwa kwa mwaka huu kiasi cha shs. 419,068,000. Zitatumika vipi katika utekelezaji wa hayo tuliyotaja hapo juu, aidha, tunahitaji kujua toka kuanzishwa kwa mfuko huu ni kiasi gani cha fedha kimekwishachangiwa, hususan Makampuni ya simu yamekwishachangia kiasi gani katika mfuko huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia ya habari (*ICT*), Kambi ya Upinzani katika hotuba yake ya mwaka 2009/2010, iliitaka Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kuwa matumizi ya *ICT* yanatiliwa mkazo na kuanzishwa mitaala kuanzia shule za msingi. Kambi ya Upinzani inayo mashaka makubwa sana kama utafiti na maandalizi ya mitaala imekwishaandaliwa na utekelezaji wake hatua kwa hatua hususan upatikanaji wa umeme vijiji ambapo mahitaji yake ni makubwa kuliko hata mjini. Kufanikiwa kwa mpango huu kunahitaji umakini mkubwa na si kauli za kisiasa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imeridhishwa na hatua zinazochukuliwa za kuvunganisha vyuo vikuu na vyuo vya utafiti katika mkongo wa Taifa wa mawasiliano. Kambi ya Upinzani inahitaji mkongo huu utumike kwa kuleta tija inayokusudiwa kwa kuwepo na vitendea kazi katika vyuo vyetu vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya mawasiliano (*TCRA*) Kambi ya Upinzani inaipongeza mamlaka kwa kupata tuzo ya Kimataifa kama taasisi bora zaidi ya usimamizi wa masuala ya mawasiliano barani Afrika kwa mwaka 2009. Hata hivyo pamoja na kazi nzuri wanayoifanya kwa niaba ya wananchi, Kambi ya Upinzani inaiomba Mamlaka kuongeza muda wa kusajili simu zao kwa kuzingatia hali ya mawasiliano na ukubwa wa nchi yetu kama Botswana, kinchi kidogo chenye mtandao bora zaidi na watu wachache ili wachukua miezi 18 kukamilisha zoezi la usajili. Kwa kuwa kuna maandalizi ya kitambulisho cha Taifa kama tutaweza kusajili watumiaji wa simu wote itarahisisha kuhamisha na kubadilishana taarifa. Tuna imani kuwa miezi 12 iliyotolewa ni michache mno kwa kuzingatia mazingira halisi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Mkongo wa Taifa ambao uliana mwezi Julai 2009 Mkoani Singida, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu ni lini Mikoa ya Rukwa, Tabora, Lindi, Mtwara na Ruvuma itaunganishwa na Mkongo wa Taifa na kwa nini mikoa hii imekuwa yenyе kusahaulika katika mipango ya maendeleo ya nchi hii? Tunaitaka Serikali kuondoa kadhia hii ya upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa hiyo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba *TTCL* ndio iliyokuwa imepewa jukumu la kusimamia ujenzi, uimarishaji, uendelezaji wa miundombinu ya msingi ya mtandao wa simu nchini (*National Communication backbone*) na pia itakuwa mhimili wa kutoa huduma kwa watoa huduma wengine (*carrier of carriers*) na itasimamia matumizi ya mkongo (*optic fibre*) wa njia za kupitisha mawasiliano. Kambi ya Upinzani inataka Serikali itoe taarifa juu ya utekelezaji wa jukumu hilo ambalo *TTCL* ilipewa baada ya kunyang'anywa jukumu lake la kutoa huduma za simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) imesajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, kifungu Na. 212, ikiwa imeundwa mwaka 1994 baada ya kuvunjwa kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania (*TP&TC*). Kufuatia kuvunjwa kwa *TP&TC* ziliundwa taasisi tatu tofauti ambazo ni za Shirika la Posta Tanzania (*TPC*); Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) na Tume ya Mawasiliano Tanzania (*TCC*), sasa ikiwa ni mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* ilibinafsishwa na Serikali mnamo tarehe 23, Februari 2001, ambapo muungano wa makampuni (*consortium*) ya *Mobile Systems International (MSI)* ya Uhlanzi (sasa *ZAIN* au *CELTEL INTERNATIONAL* hapo awali) na *DETECON* ya Ujerumani, walinunua na kumiliki asilimia 35% ya hisa na asilimia 65% zikaendelea kuwa mikononi mwa Serikali ya Tanzania. Mkataba unawapa haki wenye asilimia ndogo kusimamia na kuiendesha *TTCL*. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ni lini mkataba huu utapitiwa upya na kuwapa fursa Watanzania wenye hisa nyingi kusimamia na kulientesha Shirika la *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya hisa asilimia 35% za *TTCL* kwa mbia *MSI/DETECON* kwa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 110. Dolla milioni 60 zililipwa wakati wa kusaini mkataba na dola milioni tano zililipwa baada ya mahesabu ya mwaka 2000 kukubaliwa kwa pande zote mbili, yaani Serikali ya Tanzania na Mwekezaji *MSI/DETECON*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa chimbuko la Kampuni hii ni *TTCL*. Mchakato wa kuzaliwa kwa *Celtel* kilitokana na mauzo ya Kampuni ya *TTCL* kwa *MSI/DETECON* ambayo hatimaye mgogoro wa thamani halisi ya Kampuni ulipelekwa kwa usuluhishi na *MSI/DETECON* walitanguliza malipo ya *USD65 millioni* na kusalia salio la *USD 45 millioni* ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania 49 bilioni kwa thamani ya wakati huo. Kambi ya Upinzani inataka kujua salio hilo limelipwa au bado?

Kambi ya Upinzani bado hairidhishwi na maelezo yanayotolewa juu ya kubadilishwa kwa jina toka *Celtel* kuwa *Zain* kwamba ni jina la Biashara (*Brand Name*) inaaminika kwamba *CELTEL INTERNATIONAL* ameuza hisa zake zote kwa kampuni mashuhuri ya simu za mikononi ya Mashariki ya Kati (*Middle East*). Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya uchunguzi wa kina juu ya jambo hili ambalo linawanyima usingizi Watanzania ambao wamechoka kuibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hapo juu, Kambi ya Upinzani inahitaji kupata maelezo:-

(i) Malipo yaliyosalia katika mauzo ya *TTCL* yamelipwa au ndiyo tumeliwa?

(ii) *Celtel* kwenda *Zain*, kwa kuwa Serikali ni mbia mkuu, je, alishirikishwa katika makubaliano hayo na tumefaidika vipi kama nchi?

(iii) Kuna taarifa kuwa *Zain* Afrika ikiwemo *Zain* Tanzania imeuzwa kwa mwekezaji toka India, Serikali kama mbia ina kauli gani na tumefaidika vipi na mauzo hayo?

(iv) Kwa kuwa mara kadhaa tumeomba mikataba ya mauzo na ubia iangaliwe/ipitiwe upya Kambi ya Upinzani inataka kufahamu kama kipo kipengele ndani ya Mkatuba kinachompa haki Mbia wa hisa chache kuwa na sauti ya kukubali au kukataa katika uendeshaji wa kampuni na kama hakipo ni kwa nini?

(v) Kwa kuwa tulitunga sheria ndani ya Bunge ya kuyataka Makampuni ya Simu kupeleka hisa zao kwenye Soko la Hisa la Dar es salaam, kwa nini Serikali imeshindwa kununua hisa za *Zain* hadi zimeuzwa kwa Kampuni ya India badala ya kuziingiza kwenye soko la hisa ili wazawa waweze kuzinunua?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Kambi ya mwaka 2009/2010, tulihoji kasi ya Serikali ya kuanzisha vituo vya mawasiliano (*Tele-centrers*), hadi sasa vituo vilivyokuwa vimepangwa kwa mwaka wa fedha uliomalizika havijaanza kazi, kituo cha Mpanda kimojawapo kati ya vituo vitano. Tunahitaji tupate maelezo juu ya mipango hii inayojirudia rudia kila mwaka. Aidha, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na kasi ndogo ya kukamilisha mradi wa *Super Computer* katika taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ambao unafanywa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya India. Kuchelewesha mradi huu ni kuchelewesha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sayansi na teknolojia. Pamoja na jitihada zinazofanywa za kudahili wanafunzi wengi katika vyuo vya sayansi na teknolojia, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa udahili huo uende sambamba na huduma zinazohitajika kuwepo na madarasa ya kutosha, maktaba yenyе vitabu, maabara zenye vifaa vya kutosha, karakana zenye vifaa vinavyokidhi kwa mafunzo na viwango vinavyokubalika katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia, mfano mzuri karakana ya chuo cha *MIST* Mbeya ambayo ina vifaa chakavu vilivyoachwa na Warusi miaka 30 iliyopita, inasikitisha sana. Kadhalika mabweni yatakayotosheleza kwa wanafunzi kusoma vizuri na fedha za kutosheleza kwa chakula na mafunzo ya vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na idadi ndogo ya wasichana wanaojiunga katika Vyuo vya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Mkakati maalum wa kuwawezesha na kuwaendeleza wasichana na kupenda masomo ya sayansi utiliwe mkazo sambamba na mafunzo kwa walimu wa masomo ya sayansi katika shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi na vyuo vyote havikutengewa fedha za kutosha ili kutimiza mipango yao waliyojiwekea katika kuleta mabadiliko ya kweli kwenye sayansi na teknolojia. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwekeza vya kutosha katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya nguvu za atomiki. Kambi ya Upinzani inaipongeza kamisheni ya atomiki ambayo inafanya kazi katika mazingira magumu sana, kazi yao pia ni hatarishi. Tulishauri Serikali iwapatie *risk Allowance* na *insurance*. Tunaomba ufanuzi kama jambo hili limeteklezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Tume hii kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya athari, kujikinga au kujilinda kutokana na mionzi, pia Serikali ihakikishe kwamba Tume hii imepata magari ili kuwarahisishia kufanya ukaguzi wa mara kwa mara mikoani na kila watakapohitajika basi wafike bila matatizo. Pia wapewe vifaa ili wafanye kazi zao kwa ufanisi. Aidha, Tume iongeze juhudhi katika kudhibiti mionzi katika vyakula, kukagua vyanzo vyta mionzi na ukaguzi wa migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi kumekuwepo na wimbi kubwa la wawekezaji katika utafiti na uchimbaji wa Urani (*Uranium*). Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze imefikia wapi katika kuandaa sera ya Nyuklia? Kadhalika tunaomba maelezo wanaochimba na kutafiti ni utaratibu gani unaowaongoza katika kufanya kazi hiyo, pia wachimbaji wadogo wadogo wamepata elimu ya kutosha kuhusu madhara na kinga katika uchimbaji wa Urani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Posta/ anuani za alama za posta kutokuwalipa wastaifu kwa wakati ni kuvunja haki za msingi za binadamu, watumishi waliokuwa wa Shirika la Posta la Afrika ya Mashariki wako katika mateso makubwa, wachache waliolipwa kutokana na mapato kidogo ya Shirika la Posta. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kurejesha fedha zinazolipwa na Shirika la Posta ili kuliwezesha lifanye kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko kama Posta itaendelea hadi lini kuwa chini ya *CHC*, aidha Serikali ifanye maamuzi ya haraka kulinusuru shirika hili kwa kuchukua hatua za haraka kusawazisha mizania ya Shirika la Posta na kuwekeza kwa kuwapa mtaji na dhamana ya Serikali (*Government Guarantee*) ili shirika liweze kupata mikopo toka taasisi za fedha liweze kuendesha kazi zake kwa ufanisi na kuhimili soko la ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu alama na anuani za Posta, Kambi ya Upinzani bado ina mashaka sana juu ya mafanikio ya mpango huu na muda utakaochukua na hasa mpango huu kuanza katika Miji iliyopangwa Arusha na Dodoma haitatoa uhalisia wa ugumu wa kuweka anuani au alama za posta katika maeneo ambayo hayakupangwa kwa mpangilio hususan katika Jiji la Dar es Salaam. Pia Kambi ya Upinzani inataku kujua gharama za mradi huu na muda wa kukamilisha mradi huu kwa nchi nzima. Aidha, inayo hofu kwamba mradi huu utahitaji fedha nyingi kama muda wa kukamilika hautafahamika. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa fedha za kutosha kwa mradi huu ili ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Afadhali wewe hukuwaambia wale wa CCM wasichaguliwe. Mheshimiwa Nakushukuru sana kwa mawasilisho yako. Tunao wachangiaji wanane. Kuna Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid ye ye hajachangia hata mara moja. Waliochangia mara moja ni Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Manju Msambya na wengine atawataja Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge kutokana na kazi nyingine ambazo haziwezi kuzuilia nitamwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai apokee kiti wakati sisi tunaendelea kufanya kazi nyingine.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job y. Ndugai) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji. Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Mheshimiwa Paul Lwanji ajiandae.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nitoe shukrani kwa kupata hii fursa ya kuchangia kiti kikiwa kimekaliwa na Mwenyekiti mwenzangu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa hai na kwa kunipa afya kuweza kuzungumza hapa. Vilevile nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuniamini na kwa mashirikiano ya hali ya juu ambayo wamenipa kwa kipindi hiki cha miaka mitano ambayo nimekuwa Mbunge wao na nawaahidi kwamba tutaendelea kuwa pamoja kama ambavyo tumeendelea kushirikiana na Mwenyezi Mungu akitujalia basi nitakuwa tena mbele yao kwa ajili ya kuomba ridhaa yao kwa mara nyingine tena ili kuweza kuja kuwawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Msolla pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Maua Daftari kwa uwasilishaji wa bajeti yao ingawa wamewasilisha muhtasari lakini tumepata maelezo ya kina na tumeridhika kwamba ni mazuri tu. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kukuombeeni Wabunge wenzangu kwamba Bajeti hii tuijishe kwa asilimia mia moja. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuipongeza Wizara kwa kiasi kikubwa sana kuweza kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kutekeleza mambo mengi sana ambayo kwa miaka mitano sekta hii ilikuwa imepanga itayafanya. matatizo ya hapa na pale yapo ni hali ya kawaida, hakuna aliyekamilika isipokuwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, m jitahidi kwamba mambo yote yakae sawa. Vilevile nikupongezeni Wizara kwa sekta ya mawasiliano ya simu kwa kuweza ku-cover maeneo makubwa sana ya nchi yetu lakini mmejitahidi sana kwamba sekta yenu ime-cover maeneo makubwa sana ya nchi lakini nakuombeni sasa m jitahidi sana muweze kufika katika vijiji ambavyo viko *remote* sana katika nchi ili Watanzania wote tuweze kuunganika kwa pamoja katika mawasiliano hasa ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niipongeze Wizara kwa huu Mkongo wa Taifa (*Optic fiber*) ambao unasambazwa kwa *speed* kubwa sana, wale wote wanaopita katika njia mbalimbali katika mikoa ya nchi yetu mtakuwa ni mashahidi wa kazi kubwa sana inayofanywa ya usambazaji wa Mkongo huu. Lakini labda niseme kwamba mkongo huu matumizi yake yawe ni *demand driven*. Currently mkongo unaonekana ni *supply driven*, uwe ni *demand driven* kwa maana kwamba waruhusiwe *private sectors* wenye uwezo wa matumizi wa *bandwidth* kubwa waweze kutumia ipasavyo hii teknolojia ambayo imeingia. Uwezo wa mkongo ule kwa kazi mbalimbali ni mkubwa sana lakini tusiishie tu uwe unatusaidia katika mawasiliano tu ya simu na kwa kiasi fulani *internet*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa sana umesaidia sana kushusha gharama kwa baadhi ya maeneo na ushahidi hasa ni kwa wale ambao wanatumia mawasiliano hasa ya *internet* kwa upande wa Dar es Salaam ni kwamba gharama kwa kiasi kikubwa zimeanza kuja chini na *speed* ni nzuri sana ya matumizi ya mawasiliano haya. Kwa hiyo, Wizara iweze kulismamia na kuliratibu vizuri zaidi suala hili ili wananchi walio wengi hapa Tanzania waweze kufaidika lakini pia watu waelimishwe jinsi ambavyo wataweza kufaidika na kitu hiki ili waweze watumiaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mawasiliano ya simu za mkononi, napenda pia niipongeze Wizara. Mmefanya juhudhi kubwa sana, mawasiliano yako kote kama nilivyozungumza. Maeneo makubwa sana ya nchi yamekuwa *covered*, lakini kuna matatizo madogo madogo ambayo sasa Wizara inabidi iyaangalie na nitatoa mfano. Kwa mfano kwa sisi tunaotokea visiwani na watumiaji zaidi wa Zantel, kule kwetu kuna tatizo kidogo na *connectivity* ya Zantel Ni mara nyingi sana unaweza ukampigia mtu hata kama yupo hapo jirani yako usimpate simu inakwambia iko *busy* lakini simu iko wazi lakini humpati tu. Inaonekana pana tatizo kidogo upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunajaribu kuzungumza na watu wa *Customer Care* hasa ya Zantel lakini hatuoni juhudhi yoyote ambayo inachukuliwa na kampuni kurekebisha suala hili la mawasiliano upande huu wa Zanzibar. Lakini pia kwa wale ambao wanatumia *internet* kupitia hii hii Kampuni ya Zantel unapofika Zanzibar *connectivity* hata kama unatumia *moderm* ya *speed* kubwa kwa kweli unachukua muda mwangi sana kufanya jambo dogo sana. Yaani *connectivity* iko *slow* sana. Si kila mtu anapenda kubeba simu nne au tano, lakini kampuni zinawalazimisha watu aidha, uwe na simu yenye *line* mbili au ubebe simu mbili. Wengine hawataki kubeba simu mbili na mtu anataka kumiliki simu moja tu. Kwa hiyo zihimizeni hizi kampuni ili angalau ziweze kuweka sawa masuala ya mawasiliano ya simu hasa huku visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, jambo lingine ambalo nilitaka kuligusia kidogo ni suala la kodi, *capital gain tax*. Suala hili hasa naikusudia kampuni ya Zain Tanzania. Zain wakati ilipochukuliwa kutoka Celtel wenzetu Kenya inaonekana walifaidika walipata hii kodi, lakini sisi Tanzania hatuna hakika kama tulifaidika na hili na kubwa zaidi ni kwamba sisi Tanzania Serikali ina-share ndani ya hii kampuni. Wenzetu Kenya sidhani kama hata wanazo *share* za Serikali ndani ya kampuni ya Zain ya Kenya. Sasa hivi kuna tetesi kwamba huenda ikauziwa kampuni moja kubwa ya India.

Tanzania pengine tutakuwa tuna-*brief* tu ya suala hili lakini wenzetu Kenya wameshaunda Kamati ya Watalaam wa Kodi ili ku-*asses* itakazopata Serikali kabla ya kuruhusu uhamisho huo. Tatizo hilo pia kimsingi liko katika nchi nyingine za Afika ambazo *Zain* ina-*operate*. Sasa kwa upande wetu sisi Tanzania kisingizio cha kwamba *Zain* Tanzania inamilikiwa na *Zain International* nadhani hakina mantiki sana. Tuwe makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana labda niseme tu kwamba, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kumpongeza mtoa hoja wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na nawatakia kila la kheri. Niseme awali tu kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si siri kwamba simu za mkononi zina faida kubwa, zinaleta maendeleo na sasa hivi mkulima anaweza akajua bei ya mazao yake akiwa hapo hapo hana haja ya kusafiri. Anajua wapi atauza na ni kwa bei gani. Pia zimeleta ajira, watu wanauza kadi, watu wanachaji simu, watu wanapiga miziki humo, wanauza vipuri, imeleta ajira kwa kweli, sisi kwa kweli hatuwezi kukataa hilo. Simu zimeokoa muda wa kutembea, huhitaji sasa hivi kutembea kwenda kumsalimia jamaa yako tu, kwenda kumtakia hali, unamtakia hapo hapo na huku unafanya shughuli zako za maendeleo na Serikali imefaidika kuhusu mitandao hiyo kwenye masuala ya mapato.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka 2008 makampuni ya simu yalilipa kodi ya shilingi bilioni 40 pamoja na VAT ya shilingi bilioni 105. Makampuni haya ya simu pia yameweza kuendesha *promotions* mbalimbali, watu wamezawadiwa ushindi wa magari, nyumba na kadhalika. Hatuwezi kupuuza hili, makampuni ya simu *through cooperate social responsibility* yametoa michango mbalimbali katika shughuli za maendeleo zikiwemo *computer*, madawati na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado tuna tatizo la gharama ya miito. Simu siyo anasa tena, ukweli ndio huo, simu zinachangia sana katika kuleta maendeleo lakini gharama zake zimeendelea kuwa kubwa. Pamoja na faida kubwa sana zinazotengeza lakini bahati mbaya ni kwamba bado kuna tatizo hilo kwamba nyakati za miito bado gharama zake ni kubwa. Ningeiomba Serikali ijaribu kuona uwezekano wa kuyashawishi makampuni haya yasadie katika kupunguza hii bei ili mwananchi wa kawaide aweze kunufaika na huduma hii. Sasa mtu ananunua simu, kazi yake ni ku-*beep* tu basi haileti picha nzuri, inakuwa ni kitu amekiweka kama mapambo lakini anapokuwa na shida simu ndio ingemsaidia ili aweze kutatua matatizo yake lakini anakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia wabuni ubunifu mwengine, waje na *solar* zaidi kwa maeneo ambayo hakuna umeme maana kuna tatizo kubwa la *charging*, mtu yuko Kintanula, amenunua simu kule anai-*charge* vipi, mpaka asafiri aende ku-*charge* au labda anaenda kutafuta betri za ajabu ajabu na hili nalo liangaliwe. Ninaombwa wakati

watu wanatajirika kwa simu hizi, basi kuwa utajiri huu u-*trickle down* kwenda kupunguza hayo matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waangalie sana eneo langu, ninashukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kunisaidia sana katika kuyashawishi makampuni haya kuweka minara katika maeneo yangu. Pale Itigi minara yote ipo na simu zinasikika vizuri tu lakini ukishatoka maeneo ya Doroto kwenda Legezamwendo kwenda maeneo ya Mgandu pamoja na kwamba kuna minara pale lakini simu hazisikiki, wananchi hawana mawasiliano yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda mpaka ufile Mitundu, napo pale unakuta kuna mnara ndiyo maeneo ambapo pana mawasiliano, Mgandu Complex pale lakini ukishatoka maeneo ya Kalangali kuelekea Kilombo na Kirumbi kwenda Mwamajembe watu hawasikii. Sasa watu wamebuni, kuna vichuguu, kuna miti ambayo wanaitumia kama minara, mtu mzima kuparamia miti kwa ajili ya mawasiliano haya, ni hatari au kwenye kichuguu na maeneo hayo kuna simba na mambo mengine, ni hatari. Kwa hiyo, ninaomba waangalie kama wameweza kuweka minara maeneo hayo waweke vitu ambavyo vinaweza vikasimamia hiyo huduma kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka hapa Mwamagemebe unafika mpaka Rungwa. Rungwa wameweza mnara, mnara uko pale ni watu wa Rungwa wanasikia lakini watu wa Kintanula na Mwamagemebe wao hawapati mawasiliano. Sasa hawa watu wanaiona hiyo minara lakini hawapati huduma. Nilishawasilisha hoja hizi na nilipata *ki-note* kutoka kwa Naibu Waziri kunihakikishia kwamba maeneo hayo yataangaliwa, ikiwepo maeneo ya Idodyandole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idodyandole nao pia wana vichuguu maalumu na mnavyojua ndugu zangu maeneo yetu ya vichuguu hufuga nyoka. Kwa kweli kuna wakati fulani mtu mmoja wa Idodyandole aliumwa na nyoka kwa sababu alikwenda maeneo ya kichuguu, sasa hatujui kama alikwenda kupiga simu au vipi lakini hii ni moja ya athari na siyo ustaarabu mtu mzima kuamka asubuhi unakwenda kwenye vichuguu kwa ajili ya kutafuta mawasiliano. Mimi rai yangu ni kwamba maeneo yale ambayo tayari yana minara lakini bado mawasiliano hayasambai vizuri basi wajaribu kutafiti waweze kuona ni nini wataweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango ya makampuni haya ya simu, ninaona kama vile kuna kaupendeleo. Wanapochangia kwenye shughuli za maendeleo naona kama vile wanachaguachagua maeneo, aidha, kwa kuangalia umuhimu wa mtu lakini mimi kwa muda wa miaka mingi tu toka nikiwa katika nafasi hii, nimejaribu sana kuyaomba makampuni haya ili waweze kutusaidia katika michango mbalimbali ya huduma za jamii na ahadi lukuki tu nimezipata, tatizo unapofika muda ulioahidiwa unakuta majibu hayapatikani lakini unaona katika matangazo mbalimbali zawadi

zimetolewa au michango imetolewa maeneo mbalimbali. Naomba kujuu hawa watu wanatumia vigezo gani kutoa hiyo misaada? Minara iko maeneo yote na faida wanapata kutoka maeneo yote, sasa wanatumia kigezo cha faida kama sehemu fulani kuna faida zaidi au labda kwa mkubwa fulani kuna mapato zaidi? Ninaomba hili nalo liangaliwe, ni hiari yao lakini sasa tungependa wawe *fair* katika *distribution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Simuoni Mheshimiwa Simbachawene, kwa hiyo, namwita moja kwa moja Mheshimiwa Manju Msambya na Mheshimiwa Tatu Ntimizi ajiandae.

MHE. MANJU S.O. MSAMBYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi nina mchango mfupi tu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalamu wake, kwa kazi nzuri ambayo wanafanya na ninaamini kabisa kazi wanayofanya inaonekana karibuni kwa Watanzania wote. Namuomba Mungu awajalie warudi tena na wakirudi wapate dhamana walijonayo ili waendelee kulitumikia Taifa letu katika dhamana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, mimi nina mambo matatu tu ya kuzungumzia ambayo nimewahi kuongea na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa nyakati tofauti na ninakumbuka Mheshimiwa Waziri aliniambia niandike barua na nikaandika, ni kuhusu utawanyaji wa simu mwambao mwa Ziwa Tanganyika Kusini. Mheshimiwa Lwanji amesema hapa si jambo jema mtu mzima kwenda kwenye vichuguu, asubuhi ya leo mimi nimepigwa simu kutoka kwenye Kata yangu moja ya Kalya, mtu anatembea kutoka Makao Makuu ya Kata mwendo wa saa mbili kwenda kwenye mlima kutumia mnara ambao uko upande wa pili Mkoa wa Rukwa. Sasa saa mbili zinazopotea za uzalishaji kijijini, ni hasara kubwa sana kwa Taifa. Ninaomba Wizara iwahimize hao wenyе makampuni ya simu waweze kuona umuhimu wa kusambaza simu hizi kwa wananchi vijijini kwenye Jimbo langu hasa kuanzia Vijiji vya Kata ya Sunuka, Sigunga, Igalula, Buhingu na Kata ya Kalya. Kule zipo pesa nyingi, zimedala tu vijiji vya wavuvi na wakulima na wamenunua simu wameziweka ndani kama mapambo. Wanazitumia wanapokuja Kigoma mjini tu au wanapoamua kupanda milima na sisi hatuna uzoefu wa kupanda milima kwa ajili ya shughuli kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo kubwa zaidi katika Kata ya Igalula, kampuni ya ZAIN takribani miaka mitatu sasa wamejenga mnara pale lakini mnara huu umekaa kama pambo, hauzinduliwi na haufanyi kazi. Mara ya mwisho nimefanya ziara pale mwezi wa nne, nimeulizwa maswali nikashindwa kujibu, nilikuwa ninajikanyaga tu. Naomba Wizara iwashtue hawa wenyе hii kampuni angalau hata huu mnara uliojengwa pale uanze kufanya kazi. Maana itatokea siku moja, sina neno zuri sana la Kiswahili la

kuzungumza lakini kwa Kiingereza watu wanaweza kufanya *vandalism* kwenye mnara ule na tusije tukawalaumu maana wanaona hauna faida nao. Ni vizuri basi mnara huu uanze kufanya kazi kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasemaji wale wawili waliotangulia wamezungumzia Mkongo wa Taifa na matumizi yake. Naona tunajielekeza sana kuupeleka kwenye nchi jirani lakini kwenye baadhi ya Mikoa hatuipi umuhimu, hebu tutazame na Mkoa wa Kigoma tunahitaji huduma za simu kwa gharama nafuu kupitia mkongo huu. Kimsingi linaonekana ni dogo lakini mimi ninaliona lina umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya ZAIN imekuwa ikibadili majina na inahamisha umiliki kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwagine lakini ilipopata jina la ZAIN siku ile ambayo kampuni hii imezinduliwa kwa jina hilo la ZAIN alizaliwa mtoto ambaye alipewa jina la ZAIN na ninadhani alipotimiza mwaka mmoja ilifanyika sherehe, je, kampuni hii itakapobadilisha jina sasa na waliahidi kuwa wataendelea kumtunza mtoto huyu kwa muda wote na kumsomesha, itakapobadilisha jina na umiliki ukawa kwa mtu mwagine ahadi ya mtoto huyu itakuwaje? Linaweza likaonekana dogo lakini kwa sababu ni ahadi ilitolewa na kampuni ikiwa kwenye jina la ZAIN sasa tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa wako wachangiaji nane lakini mimi sitaki hata kuchukua hizo dakika kumi zilizotengwa, nitumie nafasi ya mwisho kuwashukuru sana wananchi wa Kigoma Kusini, kwa dhamana waliyonipa ya kuwa mwakilishi wao lakini nawashukuru nikimaanisha na Serikali. Mwaka 2000, watu wa Kigoma Kusini walifanya makosa, Mheshimiwa Mstaafu Benjamin Mkapa aliwaahidi kuwapa Wilaya, bahati mbaya kosa walilofanya siwezi kulitaja hapa wanalijua wenyewe, Wilaya ile hawakuipata, safari hii wameipata ni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inapokusudia kutoa kitu huwa ni sikiu na inatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kigoma Kusini limekuwa ni Wilaya ya Uvinza. Lile linalojulikana kama Jimbo la Kigoma Kusini ndiyo Wilaya ya Uvinza. Ninaamini mimi nitarudi hapa si kama tena Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini ila nitarudi kama Mbunge wa Uvinza. Sasa naomba Serikali iichukulie Wilaya ya Uvinza kama ni Wilaya katika Mkoa wa Kigoma ili Wilaya isimegwe ikahamishiwa kwingine maana naona kumeanza kuwa na *political gimmicks* zinataka kufanyika kwa Jimbo la Kigoma Kusini la Wilaya ya Uvinza, Chunya wamekataa, Igalula wamekataa, Kaliua wamekataa sasa mipaka imeanza kutoka katikati ya Kigoma na Tabora, inapelekwa upande wa Tabora ili kuanza kutengeneza mazingira ya kulimega Jimbo hilo. Ninaomba Serikali isikie, walivyokataa Chunya na watu wa Kigoma Kusini ambao ni Uvinza wanakataa kuwa na *political gimmicks* kwenye Wilaya ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ambayo nilikuwa ninaisubiri. Mheshimiwa Msambya alipokuwa anaongea ameitaja sana Igalula sasa msifikiri ni Igalula ninakotoka mimi. Bahati mbaya wameweka Igalula na wenzetu huko Kigoma, kwa hiyo, mimi Naongelea Igalula ya Jimbo siyo Igalula ya Kijiji, ya Wilaya mpya ya Uvinza, naomba hilo lieleweke kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba sana watu wa mtandao, hawa wafadhili wetu, watu wengi wamejiandikisha mwanzo kabisa lakini tangu juzi, jana kila ukienda unaambiwa wewe orodha hii haumo, hujajiandikisha, sasa hii inaleta hofu kwa wananchi. Tunaomba sana hasa Wabunge wengi wamekwenda kucheki orodha ya simu zao wanaambiwa haumo katika orodha, tunaomba pengine wajaribu kutazama *record* zao ili wahakiki vizuri tupate ufumbuzi wa tatizo hili la kuonekana kwamba Wabunge hatujajiandikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mtandao ndani ya Jimbo langu la Igalula, sasa nazungumzia juu ya Jimbo langu la Igalula siyo Kijiji cha Igalula, ninashukuru sana Serikali imejaribu kunisaidia kupitia hawa wafadhili katika Kata chache. Lakini Jimbo langu ni Jimbo ambalo lina matatizo sana na mtandao sehemu nydingi simu hazisikiki, pori ni kubwa wasifikiri kwamba katika mapori kule hakuna watu, wako watu na wakifanya sensa leo watashangaa umati wa watu ulioko pale sasa ndiyo maana Mavuvuzela wanaenda kutumia nafasi za Mawaziri hao, ooh, nimeongea na Profesa Msolla akasema atanisaidia, atakusaidiaje yeye? Wakati tunapitia katika Wizara ili kuwahamasisha hawa wafadhili lakini wanashindwa kuhamasishwa wanambiwa kule Jimboni msiwe na wasiwasi Profesa Msolla nimekwishamwambia kama alivyoambiwa Ngeleja nimeambiwa na Profesa Msolla kuwa baada ya mwezi mmoja mtandao utaingia katika Kata zetu, jamani! Mimi naomba leo Profesa atufafanulie kidogo kama kweli ameahidi watu kwamba yeye ndiye atakayepeleka mitandao hiyo. Nakuomba sana ushirikiane na Wabunge ambao tuko katika nafasi hizi ndio ambao tunakuona, nakuona wewe, namuona Naibu Waziri, najua wale wafadhili hawawezi kuja bila Serikali lakini nani wa kuzungumza? Ni sisi Wabunge. Kwa hiyo, namwomba sana angalau leo anieleze hizi Kata za Lutende, Miswaki, Kizengi, Nsololo na Kata ya Miyenze, kuna Kata karibu nne, tano zina tatizo sana la mtandao, zitashughulikiwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo hili ni kubwa, linapakana na Mheshimiwa Missanga, Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Rostam Aziz, Mheshimiwa Selelili, Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Kaboyonga. Sasa mnionee imani jinsi hawa watu wanavyopata shida ya mtandao, usafiri wenywewe tumezungumza jana haupo, nyie wenywewe mmesikia reli matatizo, barabara matatizo, sasa kama hawa watu hata mtandao wa kuwasiliana hawana, ni matatizo. Naomba wapatiwe mitandao hii ili tuweze kupata mawasiliano ya kupata huduma za kijamii. Naomba sana mlitazame, najua siyo kazi ya Serikali lakini kupitia mkono wa Serikali wananchi hawa watapata mawasiliano mazuri ili angalau huduma zao ziweze kusikika hata kwa mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina maneno mengi ya kuzungumza katika Wizara hii lakini kubwa ni mtandao ndani ya Jimbo langu. Mwaka jana mlisema kwamba kwa sababu ya uchumi ulikuwa na matatizo, tukapewa Wilaya moja tu katika Mkoa wa Tabora ambayo ni Wilaya ya Urambo wakasema ikiwa afadahli basi watarudi tena katika sehemu ambazo walikuwa wameachia. Sasa ninaomba sana *TIGO* ni mmoja wao ambao hawajafika kabisa katika Jimbo langu la Uchaguzi, *VODACOM* ni tatizo katika Kata ya Goweko, wamesimamisha mitambo yao lakini mawasiliano ni hafifu mpaka upande kwenye miti, wananchi wangu nina wahitaji kwenye kura sasa wakiwa wanapanda kwenye miti wanaanguka na kuvunjika miguu watakwendaje kwenye upigaji kura? Au wanakwenda kwenye vilima kuna nyoka na unajua katika Jimbo hili nyoka Koboko ndiyo mahali pake. Sasa wanapanda kwenye vichuguu hivi wanakutana na Koboko wanawauma, wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutakuwa na wapiga kura kweli kwa Chama cha Mapinduzi? Naomba muwaonee imani siyo mimi tu Mbunge ambaye napiga kelele hapa katika Bunge, naomba sana mtandao huu na mnihakikishie kwamba angalau mmewashawishi, mnawenza mkawa hamkuwashika mikono lakini sauti zenu Serikali watajitahidi kuona kwamba hawa wananchi kweli wanahitaji huruma hii wapate mtandao kwa ajili ya mawasiliano kwa sababu wanakosa huduma. Huduma ya Serikali wanaikosa, huduma yao wao wenye kutoka kijiji hadi kijiji wanaikosa, kutembea katika vijiji, haya matatizo yakizidi katika Jimbo hili jamani tutakwenda wapi? Tutakuwa watu wa visiwani. Jimbo la Igalula wapo watu wengi tena wazuri tu wafugaji nyuki, mifugo ya kawaida, wakulima wa mchele, ukitaka mchele wanalima mchele, wanakula mchele, sasa muwaonee huruma hawa watu wanataka mawasiliano ili tupate biashara. Unakwenda katika Kata ya Miyenze, Kata ya Loya mtu mmoja ana gunia 200, 300 anakwambia aah, safari hii mpunga nimepata kidogo sana, hapo ana magunia 100 sasa atasafirishaje kama hana mawasiliano? Hana barabara, hana reli, ndege, hawana haja ya ndege, watu wangu hawapandi ndege lakini wanahitaji barabara, wanahitaji mawasiliano ambayo hawana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba chonde Serikali watazameni kwa macho ya huruma watu hawa na mimi kwa sababu nakwenda kule tena ili tukamalize awamu hii, nilimwambia Waziri Mkuu hii wanaita Halmashauri, tutakwenda wapi kama hawana mawasiliano? Halmashauri hii Waziri Mkuu aliahidi angalau tutapata Halmashauri yetu na sasa na mimi nakuongezea tu hapo Profesa lakini unajua kabisa kwamba Halmashauri hii inakuja na ikija wapate faraja, wapate mawasiliano mazuri ya mtandao. Hata wasiojua kusoma, anapiga simu mpaka mwenyewe unafurahi. Ukimwambia tu namba yangu hii, anakwambia ngoja naingiza sasa hivi. Unampelekea vocha anakuambia usiwe na wasiwasi nitajie namba. Sasa wanawenza kuwa hawana elimu lakini utalaamu wa kutumia simu za mikononi ndiyo mahali pake katika Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Profesa, hebu nitazame kwa macho ya huruma, wewe mwenyewe umesema unataka kurudi kule hata mimi nataka kurudi nisije nikalia bure kama nilivyotaka kulia mwaka jana. Wewe mwenyewe unarudi kwenye Jimbo na watakupokea vizuri, Dokta Maua kule Pemba huna matatizo nao, sasa

nakuomba na mimi msinipe matatizo yasiyokuwa na sababu kwa sababu wananchi bado wananiaka, sasa nikienda tena wataniuliza mama mtandao uko wapi, ulituambia wafadhili wanashughulika? Sasa kushughulika kwao siyo wao ni kupitia kwenu. Hapa Mwenyezi Mungu anasema niombeni nami nitawapa, sasa mimi naomba kupitia kwenu, Mitume wamewekwa ili tufike kwa Mwenyezi Mungu, unapita kwa Nabii Issa, unapita kwa Mtume Mohammed lakini lengo lako ni kwenda kwa Mwenyezi Mungu. Mimi nasema hivi mtandao huu siwezi kuwaendea peke yangu bila msaada wenu ninyi wawili na Serikali yetu ya CCM ambayo ninaipenda kabisa na ninaimani tatarudi tena katika uongozi, sasa uongozi atarudi Kikwete peke yake bila sisi wasindikizaji? Tatarudi vipi kama haya mambo hayawezi kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana wapiga kura wangu wengi wanaipenda CCM, wanaipenda Serikali yao na kuitumikia Serikali yao, lakini mambo madogo madogo kama haya wasaidieni ili waoneshe upendo na nguvu. Huwezi kusema kwani simu tu, hapana ni nyongeza unaweza kupika mchuzi kama hukutia chumvi hauwezi kukolea sasa hii ni katika kuwakoleza hawa wapiga kura. Nazungumza kwa uchungu na kwa imani kabisa ya wananchi wangu, naomba mtandao katika Jimbo langu katika maeneo niliyoyazungumza, hebu jaribuni kuwashawishi. Dokta Maua wewe hodari sana wa kushawishi hawa wafadhili, umeeleza hapa katika Bunge hili kwamba nimekwenda nimewasadid, sasa mimi Dada yako hutaki kunisaidia, unasaidia wengine tu, mimi nitashangaa sana, kumbuka tulikotoka, hujataja kabisa Jimbo la Igalula, sijakuona wala sijakusikia, sasa inakuwaje yaani urafiki unaishia hapo hapo? (*Makofi*)

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa maandalizi na uwasilishaji mzuri wa hotuba ya bajeti hapa Bungeni. Naomba nianze kwa kutamka kabisa kwamba naunga mkono hoja hii ya Waziri asilimia mia kwa mia(*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru na kumpongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, kwa kazi yake nzuri ya kuhamasisha hasa kampuni ya ZAIN kuweza kujenga minara pale miwili katika Jimbo langu, katika Mji Mdogo wa Malinyi na Mji Mdogo wa Mtimbira. Sasa ninaendelea kumuomba na barua ameshaiandika kwa ZAIN na nakala kwangu kuwaomba sasa wafikirie ujenzi wa minara miwili mingine ya Itete na Iragua. Wakijenga minara hii mingine miwili, watakuwa wamekamilisha kutoa huduma ya simu za mkononi Jimboni kwangu maana zimebakia Kata mbili au tatu hivi, hizi zikikamilika kwa kujenga hii minara miwili basi mambo yatakuwa bomba kimawasiliano katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile naambibiwa kwamba ZAIN wanataka wajenge minara mingine miwili katika Mji Mdogo wa Malinyi na Mji Mdogo wa Mtimbira kwa lengo la kuimarisha usikivu. Hili mimi nalikubali na kuliunga mkono, lakini mimi ningefikiri kipaumbele ingekuwa katika eneo ambalo halina mawasiliano

kabisa au mawasiliano ya shida zaidi. Kwa sababu inakuwa kama unamwongeza chakula mtu aliyekuwa na chakula tayari na unamnyima yule mtu ambaye hana chakula. Mimi nadhani mantiki ingesaidia sana kuwapa hawa watu ambao hawana halafu tuendelee kuimarisha kule ambako usikivu una matata. Eneo hili ambalo bado hawajapata huduma lina watu karibu 75,000. Hawa watu siyo wachache, ninamuomba Naibu Waziri aendelee kuwahimiza hawa ili tuweze kupata huduma hii muhimu kwa Kata ya Itete na Iragua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niipongeze Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya mwaka huu ya kutenga fedha nyingi za utafiti wa kisayansi. Jambo hili lipi katika Ilani ya Chama chetu ya mwaka 2005 na tulisema kabisa kwamba ifikapo mwaka 2010 itengwe kiasi cha asilimia moja kwa utafiti wa kisayansi na hili halina ubishi. Mimi nimefurahi vile vile kwamba Waziri amesema atapendelea kufanya utafiti wa Kisayansi wa Kilimo. Jambo hili kwanza linaunga mkono kaulimbi ya Serikali ya Kilimo Kwanza lakini zuri zaidi ni kwamba nchi zote zilizofanya mapinduzi ya kijani yaani *green revolution*, yalitokana kwanza na utafiti wa kilimo ambao ulielekeza katika kuzalisha mbegu bora, wanaita *high yielding varieties* za mpunga mfupi, kazi imefanyika sana vizuri kule Manila Philippines lakini kwa kuzisambaza katika nchi zote zilizofanya Mapinduzi ya Kilimo, India, Thailand, Vietnam, Malaysia na kadhalika. Jambo hili ni zuri la *ku-focus* katika utafiti wa sayansi ya kilimo ili tuweze kuunganisha mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili katika utafiti ni lile la matumizi mazuri ya mbolea. Nchi zote walizofanya Mapinduzi ya Kijani walifanya kazi nzuri katika matumizi ya mbolea ambazo haziharibu udongo. Jambo hili nalo ni muhimu kulitilia mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la tatu, ni utafiti katika kilimo cha umwagiliaji. Nchi yetu hii ni kubwa mno, haiwezi kutegemea mvua, kwa mfano sisi mwaka huu katika Jimbo la Ulanga Magharibi tulipata mpunga mzuri sana lakini mvua za mwezi Mei mwishoni ambazo si za kawaida zimeharibu mpunga. Mpunga umelala upo chini ya maji, tumepata matatizo makubwa. Kwa hiyo, suala la utafiti ni muhimu katika kilimo na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *combination* ya mbegu bora, matumizi bora ya mbolea na madawa na kilimo cha umwagiliaji, ndipo kutafanyika Mapinduzi ya Kilimo katika nchi hizi ambazo zinaongoza katika kilimo. Nchi kwa mfano ya India kulikuwa na njaa sana katika miaka ya 1960 mpaka 1970 lakini kuanzia miaka ya 1980 mpaka leo India ina *surplus* kutoptana na Mapinduzi ya Kilimo ya Kijani. Sasa hivi anayetoea mchele mwingi ni Thailand ndiye anayetuongoza lakini anafuatiwa karibu kabisa na Vietnam nchi ambayo imepigana vita kwa miaka mingi na wakubwa kabisa wa Duniani, Wamarekani, sasa hivi wanatoa mpunga na mchele mwingi na siri yake ni hii katika Mapinduzi ya Kijani ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne katika utafiti, naomba sasa tukamilishe utafiti huu wa gari letu Nyumbu. Duniani kote watu waliofanya maendeleo ya viwanda mojawapo ni kutengeneza gari. Chukua mfano wa Japan ya miaka ya 1960, Toyota ya zamani siyo Toyata ya leo, siku hizi wote hapa watu wa Serikali mnataka Shangingi VX8 lakini kama wewe unaikumbuka Toyota ya miaka ya 1960, mimi zamani nilikuwa Bwana Shamba kule Geita, Sengerema, hawa jamaa wa *Nyanza Cooperative union* walikuwa wanunua sana Toyota, ulikuwa unatapakaa vumbi kama vile upo nje kwenye *Station Wagon* ya Toyota, lakini leo ndiyo gari bora katika nchi yetu hapa na tuna magari mengi sana ya Kijapan. Sasa ninyi mnashindwa nini kuendeleza utafiti wa Nyumbu, Nyumbu tulifika mahali pazuri sana, sasa wapeni fedha na rasilimali waanze kuzalisha angalau Manyumbu 30. Nyumbu ni gari ya Tanzania tunayotengeneza katika utafiti wa Kijeshi, tutengeneze gari ile ili na sisi tuenze kupiga hatua katika suala la teknolojia. Maana teknolojia yenyewe ndiyo hiyo na kutengeneza magari ni teknolojia kubwa sana na watu wote wamefanya. Wahindi, Wachina, siku hizi ukienda China kule hata *Bulck*, hili gari ya Marekani inatengenezwa kule China. Kwa hiyo, mimi naomba tuenze kuipa pesa tusipige siasa tu, tuwape pesa vijana hawa kama wale wa *CARMATEC* wana vitu vizuri sana wanatengeneza, tuwape sasa pesa wafanye *production*. Hii *production* ya mkono ndiyo maana vitu vyao vinakuwa ghali sana, ni vizuri lakini vinakuwa ghali, hata *quality* inakuwa tatizo na mimi nakuombeni fanyeni jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, ni Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, jambo hili ni zuri sana. Uamuzi wa Serikali katika kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ni jambo zuri, lakini sasa tunataka tujue tumefikia wapi maana tuna karibu miaka miwili ya utekelezaji. Ni Wilaya zipi tayari zimefikiwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano? Je, kama zimefikiwa tayari zimeanza kufaidika? Kwa sababu Mkongo wa Taifa utasaidia mawasiliano ya simu za mkononi na *internet*. Mimi leo nikitaka kutumia *laptop* yangu mpaka niende Mahenge Makao Makuu ya Wilaya kwa sababu kuna *TTCL* pale lakini nikienda Malinyi kule siwezi kupata, nilijitahidi kuweka *ZAIN* matata matupu, shilingi elfu kumi, natumia kwa dakika tatu, sasa utaweza hii kweli? Kwa hiyo, mimi naomba kujua ni wapi tumefika ili tuweze kuzingatia matumizi mazuri haya ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na kuunganisha Mkongo huu na jirani zetu. Ni jambo jema hili kwa sababu Tanzania kijiografia ipo katikati ya nchi nyingi za Afrika ya Mashariki na Afrika ya Kati. Kwa hiyo, sisi Tanzania kuwapelekea huduma za Mkongo nchi za jirani, ni jambo jema na ni jambo la kibiashara pia. Ndiyo maana sisi tulitaka kuchukua fursa hii ya kijiografia tuwe *hub* hapa na *hub* yenyewe ndiyo hiyo ya Mkongo, itakuwa mojawapo licha ya *hub* ya miundombinu mingine ya barabara, reli na kadhalika. Tunafanya hilo na tufanye kwa nguvu zetu zote ili kuwezesha Taifa letu kuwa msaidizi, *facilitator* wa maendeleo ya kiuchumi na jamii katika nchi za jirani zetu ambazo ni nyingi, zipo zaidi ya tisa nadhani. Ninaomba Waziri katika *windup* yake basi tujue tumefikia wapi katika utekelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia na nawashukuru sana kwa kunipa fursa hii, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Dokta Juma Ngasongwa kwa mchango wako na leo tumejahamu vizuri kwamba kumbe kitaaluma ni Bwana Shamba, ahsante sana. Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko ajiandaye.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninamshukuru Mungu kwamba tupo hapa kwa ajili ya kuzungumzia mambo ya kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wanaohusika kwenye sekta hii ya mawasiliano. Leo ni siku ambayo wengi watataka kujua hatma ya ushindani iliyopo katika sekta hii. Tulikuwa na Shirika letu la Posta ambalo kwa sasa kwa kweli ni wachache sana wanalitumia, mabasi yamekuwa yakifanya huduma hiyo ya Posta, wamejitokeza pia watu wengine ambao pia wanafanya huduma hiyo kwa namna nyingine. Lakini siyo hivyo tu huduma nyingi zilizokuwa zinafanya na Posta sasa hata ile ya kutuma hela unawenza ukafanya kwa kutumia simu yako ya mkononi M-PESA. Mimi najiuliza ushindani mkubwa huu, Shirika letu hili litapona? Nini hasa kifanyike ili tuweze kulinusuru shirika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ule ukurasa wa 25 kwenye kitabu cha Waziri, ameweza kutuonesha ni jinsi gani kwa mwaka huduma mbalimbali zimeweza kuongezeka. Lakini zimeongezeka kwa asilimia ndogo sana. Ipo huduma aliyoizungumzia pale kama ya viyuo vya Posta, vilikuwa 84 kwa mwaka mzima vimeongezeka viwili tu vikawa 86. Mimi najiuliza tumejipanga vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuijuliza hayo niseme tu kwamba hii ni changamoto na mimi pia niombe endapo wanataka Posta iingie kwenye ushindani, ili iweze kushindana na hizi njia zingine ambazo zinafanya shughuli hizo hizo zilizoshamiri, basi Posta iwezeshwe. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashika ya Umma, tuliona kwa kweli wanachopewa ili waweze kuingia kwenye ushindani ni kidogo sana. Ninaomba kutoa rai kwamba Shirika hili liangaliwe ili liweze kuwa kwenye ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nitoe pongezi zangu kwa Serikali kukamilisha ile awamu ya kwanza ya Mkongo wa Taifa. Lakini kukamilika huko imetuwa ni faraja na mimi ninayetokea Moshi ambako Mkongo huo umefika, tulitarajia mambo mengi sana yafanyike mara moja. Mojawapo ni *Internet Service Providers* wajiunge ikiwemo ile ya Kicheko na tulitarajia kwamba hata huduma hiyo itakuwa haraka zaidi (*faster*) lakini mpaka sasa hivi imetuwa ni shida na niseme ni balaa tupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajasiriamali hawa walijiandaa na wakawa wamejenga namna ya kuunganishwa kwa sababu Mkongo huo ukitaka kuunganishwa, wenyewe ulifukia Posta, lakini kila wakitaka kuunganishwa wamekumbana na vikwazo kadhaa. Mojawapo ni kwamba viunganisho hakuna na ukitaka viunganisho hivi mpaka upate kwa yule Mchima aliyejenga Mkongo na Mchima akiulizwa inakuwa haiwezekani kwa sababu viunganisho viliyopo sasa hivi ni vile vya mradi tu, wakitaka wasubiri kwa miezi kadhaa isiyopungua miezi kumi na sita. Sisi tunajiuliza, hivi kweli Mkongo umefika na watumiaji hawawezi kutumia maana yake ni nini? Ninaomba wakati Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho yake aweze kuwaelezea hawa wajasiriamali ni jinsi gani wataweza kujiunga haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama pia za kujiunga zipo juu, gharama hizi zinifikai dola efu ishirini na tano kujiunga tu na kama mjasiriamali huyo akifanikiwa kujiunga basi kutumia aliye dola elfu mia moja themanini kwa kutumia. Hivi kweli kwa mtu wa kawaida ambaye ndiye anayetoa huduma atawenza kufanya vitu hivyo? Napendekeza waunganishwe halafu walipe kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo lingine pia ni *capacity charge*, kiwango ambacho kinatolewa kwa wao ni kikubwa mno zaidi ya matumizi na hapa ni kama STM1 ambayo ni 155MBPS. Hiyo ni kubwa zaidi yaani *just too much* kwa huduma hizo za *internet*. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atoe pia elimu kwa umma kama kuna au njia ambayo itawenza ikarekebisha jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kadhaa ambazo wao watumiaji au wadau hao walikuwa wanaona kwamba zingeweza zikarekebisha hali hiyo, mojawapo ni kama ile ambayo endapo wataweza kuunganishwa kama Chuo Kikuu cha Dodoma kilivyouniganishwa au labda Bunge tulivyouniganishwa, basi wao pia wataweza kutoa huduma hiyo kwa bei nafuu zaidi na watu wengi wataweza kunufaika. Ni mambo mengi hapo ambayo wadau hao wangependa kueleweshwa na ninaamini kabisa kwa vile wachangiaji si wengi utampa muda kama Kanuni zitaruhusu Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi ili watu hao wapate amani. Kwanza Tanzania nzima nadhani wako kumi na tano tu ni watu wanaofahamika, ni watu ambao wanaweza wakafuatiliwa, kwa hiyo, si jambo ambalo litakuwa tatizo sana kwa wao kutumia huo Mkongo nionavyo mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kuhusu Mkongo wetu wa Taifa na eneo ambapo umefika ikiwemo Moshi, naomba sasa nitoe shida kuhusu gharama za kutumia *internet*. Mpaka sasa bado ziko juu ukilinganisha na matumizi au na jinsi ambavyo watu wamehamasika kutumia *internet*, sijui kuna mpango gani wa kuweza kufanya huduma hiyo ikawa nafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hiyo tu, maeneo mengine ukitoka nje ya Tanzania tu hapa hapo Kenya ukiwa na *laptop* yako popote hata ukiingia hapo kantini

unafungua unaanza kusoma vitu vyako na kutuma. Hapa kwetu ni mpaka uende kwenye *Internet café* au uende eneo ambalo lina *Internet*, tatizo ni nini hasa? Mimi naomba kwa niaba ya wengine tueleweshwe ni lini na sisi basi tutakuwa na *wireless* tukifika tufanye vitu vyetu kwa kutumia *computer* zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu hawa wenye simu wakiwemo *VODACOM*, *ZAIN*, *ZANTEL* na nyinginez, sasa hivi hata kule vijijini wengi ni watumiaji wa simu hizo. Lakini zaidi ya kununua vocha na kutumia wao hawafaidi chochote mpaka atokee mtu aanze kwenda kuombaomba huko kwenye hizo kampuni asaidiwe kama ni elimu ya ujasiriamali asaidiwe au hata wodi ya wagonjwa asaidiwe vyote hivyo ni omobaomba tu. Ni lini basi Waziri atakaa na hawa watu ambao wana mapato mazuri waende awamu kwa awamu kusaidia maeneo tofauti kwa sababu watumiaji haohao ndiyo wanaofanya wao wakawa hapa nchini kwa raha zao na pia kwa mapato ambayo yamekithiri? Mimi nimeona niombe kwa ujumla kwamba wale watuamiaji wa vijijini wangetaka pia kuona wanafaidika na huduma ambayo wao ni wadau wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii kuwatakiia ninyi wote ushindi katika uchaguzi unaokuja na mimi mwenyewe niendelee kuwaomba wale akima Mama wa Mkoa wa Kilimanjaro kwamba naomba tuendelee kuwa pamoja, nia ninayo na bado nguvu za kuwatumikia ninazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond, wakati unamalizia kujaribu kuonyesha nia yako, nimemuona Mheshimiwa Ndesamburo anageuka kabisa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Basil P. Mramba, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu ajiandae kumalizia.

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami nianze kwa kuunga mkono kabla sijasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa sekta hii ndogo ya mawasiliano, TEKNOHAMA na yote hayo, ni mojawapo ya hotuba nzuri sana kipindi chote cha Awamu ya Nne, nafikiri inatia matumaini angalau kwa sababu sasa tunaanza kuona mambo ya kileo yakiingia kwenye nchi. Tukishapata huu Mkongo wa Kitaifa na yale yote yanayoendana, nchi yetu itakuwa imeshaingia kwenye dunia ya kwanza, ni mapinduzi makubwa kabisa. Lakini kwa sababu kama alivyosema msemajii aliyenitangulia mambo haya siyo rahisi watu wakaweza kuyaewa lakini nina hakika watakuja kuyaona na hilo ndiyo jambo la maana, *E-commerce*, *E-Government*, *E-Medical treatment* na kadhalika yote hayo watakuja kuyaona na yatakuwa ni ya mshangao mkubwa. Kwa hiyo, nawapongeza sana na ninaunga wenzangu mkono wale wanaosema muendelee hivyo hivyo kwa kasi mpya zaidi na kwa uelewa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nikubaliane na yote aliyosema Mheshimiwa Shally Raymond, ni ya kweli na ndiyo ingekuwa mwanzo wa kuonyesha vitu mionganoni mwa wananchi kwamba vitu hivi kweli vinawezekana. Kwa hiyo, naunga mkono yote hayo aliyoomba na kama yangefanikiwa kwa kweli itakuwa ni mapinduzi makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kwenye huu Mkongo wa Taifa, nirudie kusema rasmi kwamba kwetu Rombo ukituunganisha Makao Makuu ya Wilaya na Mkongo, tutakuwa tumefaidika lakini siyo ya kutosha, sisi tungependa kuunganishwa na Kenya pale Holili au Taveta kwa jina la Kenya na Tarakei au Oloitokitoki kwa jina la Kenya, mkitufikisha hapo halafu mkazungusha nyuma ya Mlima mpaka Makao Makuu ya Hai basi tutakuwa tumefika sawasawa pale tunapostahili kufika. Nina hakika Waziri na Naibu Waziri wananielewa na niko tayari kushirikiana nao kuwaonyesha njia na kuwapa habari zaidi kama wanazihitaji. Lakini kwetu bila Holili na Tarakea hatujafaidika sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni swalii, hivi ni Wilaya ipi au zipi tena Tanzania ambazo bado zina usikivu mdogo wa redio? Unajua usikivu wa redio una uhusiano na mambo ya *licensing* ya kutoka *analogy* kwenda kwenye utaratibu wa *digital*. Sasa mimi nauliza sielewi sawasawa hivi kama unaweza ukaitoa televisheni ikaenda *digital* na tukaona vizuri, je, redio haiwezi kushughulikiwa? Maana bado wengine tunategemea sana redio za nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa taarifa yako kusikia *TBC One* au *TV* yoyote ile, ukiondoa ile *TV*, *TBC* kwangu hakuna, sisi tunategemea redio ya jirani, sasa mpaka lini? Hata televisheni zao, mimi naona televisheni ya Kenya Citizen au ile ya Serikali ya Kenya kwa ubora zaidi kuliko za huku kwetu Tanzania yaani kuliko *ITV* na *TBC* na mimi sielewi kwa nini kwa sababu toka miaka ya 1990 tulikuwa tunaahidiwa ubora wa kuona na kusikia mpaka leo hatujaupata sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la ubora ni kubwa kwa sababu hata hizi simu za mikononi kilichokuwa kinazunguza na wote hawa toka Dr. Ngasongwa na wengine wengi, walikuwa wakizungumza hapa habari za kupanda miti ili upate usikivu. Hili tatizo la usikivu ni kubwa kabisa na ninafikiri naweza nikasema kwamba ingawa tumeendelea sana tuna mitandao ya aina mbalimbali kila mahali lakini bado liko tatizo kubwa kabisa la ubora yaani *quality*. Yuko Mheshimiwa mmoja hapa alisema watu wanapanda miti, mimi nikiwa ndani ya nyumba yangu pale kijijini ambapo nimezungukwa na watu wengi wenye mitandao nikiwa ndani siwezi kupata usikivu wa mtandao wowote mpaka niende *bedroom*, sasa mambo haya ya kwenda *bedroom* kwenda kusikiliza simu ni jambo gani hili? Au nitoke nje kabisa na wakati mwininge ni usiku na pengine mvua inanyesha na kadhalika, nitoke nje ndiyo nikapate usikivu. Hili tatizo la usikivu ni kubwa sana nadhani hizi kampuni zimekazania zaidi kutandaza badala ya kusikika au kusaidia usikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kule kwangu nikienda kwenye vijiji fulani fulani ghafla simu yangu inakufa na ninaalikwa Kenya kwamba “*welcome to Kenya*”, mtandao wa Kenya unanikaribisha mara moja na kuniambia jinsi ya kubadili zile namba za mtandao za mwanzo na mambo ya namna ile yaani naingia Kenya mara moja. Sasa wala sijui kama nikipiga simu kwenye maeneo hayo kama ni *trunkcall* bei ni ile ile ya Kitanzania na ni sawasawa na ningepiga nikiwa Moshi au ni namna gani? Kwa hiyo, mimi nimezingirwa kabisa kwani usikivu ni mbovu katika Wilaya nzima ya Rombo, simu moja lazima uipige mara tatu au nne ndiyo umalize mazungumzo yako kwa sababu ya kukatikatika mara kwa mara. Kwa hiyo, mimi naomba hilo labda iwe ni ajenda ya Wizara kuona namna ya kusaidia kukatikatika na usikivu maeneo yote ili angalau tujisikie kwamba tumeingia kwenye dunia ya kisasa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni Shirika la Posta na Benki ya Posta. Zamani wakati wa *East African*, Simu na Posta zilikuwa zimeunganishwa baadaye yanayoendelea sasa yakawa ndivyo yalivyo. Lakini Shirika la Posta lina mtandao mpana sana kila mahali *almost* kila Tarafa ina Shirika la Posta lakini Benki ya Posta haipo kila Tarafa au kila Kijiji. Kwa hiyo, mimi ninadhani wakati umefika wa kuona namna ya kuunganisha Benki ya Posta ambayo hata yenyewe sasa hivi haina mtaji wa kutosha, ina tatizo la mtaji na Shirika la Posta ili wafanye kazi moja. *In other ways* kama haiwezekani kuziunganisha kabisa na mimi nakubaliana na wale wanaosema kwamba hili Shirika la Posta halitakuja kukaa lifanye kazi kibiashara, nimesoma hapa kama kazi yake itakuwa ni ya vifurushi na vifurushi vijijini havipo, vijijini kuna mazao mimi naona *future* ya Shirika hili ni duni kabisa, bora turudi upya tuangalie lilivyokuwa kwa ile *East African Community* ya kwanza namna ya kuziunganisha ili zifanye kazi moja, moja kubwa ni hii ya kupeleka shughuli za fedha vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pamoja na kuwa na benki zetu hizi za *CRDB*, *NMB* na kadhalika hatujafika vijijini yaani *penetration* ya benki zetu vijijini ni ndogo. Lakini kwa kushirikisha Benki ya Posta na ikapewa fedha au mtaji zaidi na mtandao huu wa Posta katika vijiji, Posta wanaweza wakawa ni kitu kimoja au ni *agent* nafikiri tatizo la mikopo chini ya utaratibu wa Kilimo Kwanza litakuwa limekwisha kabisa. Hilo ndiyo lilikuwa ombi langu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaomba tena kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofsi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatiwa na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na ninadhani Mheshimiwa Simbachawene anaweza akapata nafasi.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi naomba kama walivyosema wenzangu kwanza Prof. Peter M. Msolla na timu yako niwape hongera sana. Ukisoma hotuba hii na hasa ukiangalia malengo ya 2010/2011, utaona kabisa ni hotuba makini ambayo inaonyesha *exactly* wanataka kutoka wapi na kwenda wapi. Kwa hiyo, Prof. Peter M. Msolla hongera sana, ni hotuba nzuri sana na kama alivyosema Mzee Mramba ni kati ya hotuba ambazo ni

nzuri, haina makonakona yasiyoelewaka, sasa mimi nataka kabisa kuweka kwenye record, that it is a good start.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba pia kwanza niwashukuru wenzangu wa kule Kasulu, naomba kwa namna ya pekee niwashukuru Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa ujumla wao wamekubali kunichangia fedha ili kuchukua fomu. Madiwani hao wamenichangia shilingi 250,000/=, nawashukuru sana kwa fedha walizonichangia na niwaambie tu kwamba tuko pamoja, mimi ni wao na wao ni mimi. Nawashukuru sana kwa kazi nzuri hiyo ya kunichangia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba kwa namna ya pekee kwani ndiyo tunamalizia kipindi chenyewe, niwashukuru watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, viongozi wa dini, viongozi wa Wilaya na Mkoa, kwa kunipa ushirikiano mkubwa sana katika kipindi changu cha miaka mitano ambacho nimekuwa nikiwatatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempongeza Waziri Peter M. Msolla lakini naomba pia kwa namna ya pekee niwapongeze wenzetu wa *TCRA*, hii Tume ya Mawasiliano, kwa kazi nzuri wanayoifanya chini ya Prof. Nkoma, wanafanya kazi ya kitaaluma na nzuri, Prof. Nkoma na timu yako hongereni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nina mambo mawili au matatu ya kuchangia katika hotuba hii. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Nishati na Madimi na nilikuwa nashughulikia mgogoro wa Mererani, tulipokwenda kule Mererani, Arusha moja ya shida tulizokuwa nazo ilikuwa ni matumizi ya mionzi kwenye *scanners* pale mgodini. Naomba kabisa kwa namna ya pekee kupitia Bunge hili niishukuru Tume ya Taifa ya Mionzi iliyopo Arusha, walitupa ushirikiano mzuri sana na ile kazi tumeifanya vizuri. Chini ya ushirikiano wao, wametu-guide vizuri na Bunge litaarifiwa juu ya *findings* zetu kuhusu matumizi yale kama yanaathari kwa binadamu au hayana kwa sababu wenzetu wa Tume ya Taifa ya Mionzi wakiongozwa na Prof. Idd walifika kwenye Kamati yangu na wakatupa ushauri mzuri wa kitaaluma na wametuandikia repoti nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati nawapongeza wenzetu wa Tume ya Mionzi, Arusha nilikuwa namuomba Prof. Peter M. Msolla, wakati tuko na ile Tume ya *Atomic Energy Arusha* walitunong'oneza mambo mengi mazuri. Lakini moja walilolisema, walitupa angalizo juu ya *Uranium* inayochimbwa katika Wilaya ya Bahi na Namtumbo chini ya makampuni ya Australia, kwamba walikuwa hawaridhiki na *safety standards* ambazo wachimbaji au watafutaji wa *Uranium* wanazifanya. Sasa ninamuomba Waziri kama itampendeza ile timu ya Prof. Idd ya *Atomic Energy Arusha* kabla ya Bunge hili kufungwa wapate fursa ya kuja kutueleza au walieleze Bunge masuala ya *Uranium*. Mambo ambayo yalitusisimua sana na moja walilolisema walisema kwamba hata maji tunayokunywa yanayotoka Makutupora/Mzakwe, yako kwenye eneo ambalo lina *Uranium* nydingi sana. Wataalamu hao na ni mabingwa kweli, *physician* wako pale, ninaomba sana kupitia kwako Prof. Msolla kabla ya Bunge hili bila shaka

hujaishiwa bado, una mabakibaki hebu ile timu ya Prof. Idd Mkilaha ambaye ni bingwa wa *Uranium* kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lakini sasa hivi ameazimwa na *Atomic Energy* waje watueleze masuala ya *Uranium*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalitusisimua sanasana sisi, tuliwaomba kwenye Kamati waje lakini Prof. Idd akawa amesafiri nje ya nchi kwa shughuli hizo hizo za kitaalamu maana yeye ni *member* pia wa *International Atomic Energy*. Kwa hiyo, ninaomba kupitia kwako Prof. Msolla hebu tumkaribishe huyu bingwa ili na Wabunge mnufaika mjue haya mambo ya *Uranium*, ni mambo ya msingi kweli na tusifanye mchezo kwa sababu ni Nishati nzuri sana lakini ni Nishati hatari kweli kweli ikiwa *mishandled* na baadhi ya watu ambao hawana mapenzi mema na Taifa letu.

Napenda kusema kwamba hawa watafutaji wa *uranium* wamekuwa wakiwapiga chenga hawa mabingwa wa *atomic energy* kila wanapowatembelea kwenye maeneo yao huko Bahi na huko Namtumbo. Nalizungumza hili kwa sababu *wali-appear* kwenye Kamati yangu. Kwa hiyo, naomba Profesa alizingatia. Hiyo Semina haiwezi kuwa na bei kubwa, Wabunge hawa hawana gharama siku hizi, mkiwapa pesa kidogo tu hawana shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa naomba tu kupitia kwako, najua haya makampuni ya simu ni wafanyabiashara *Zain, VodaCom, TTCL*. Lakini naomba kupitia Wizarani kwamba kule katika Jimbo langu la Kasulu kuna migogoro. Maeneo waliiyoweka minara katika Vijiji vya Makere, Mgombe na Nyumbigwa kuna migogoro ambayo nafikiri kupitia kwenu tunaweza kusaidiana nao kuweza kuiondoa. Najua ni wafanyabiashara, basi waweze kulipa pale ambapo wamewekeza minara yao.

Pia kwa namna ya pekee, sisi tuko mpakani, Mheshimiwa Prof. Msolla kupitia kwako tuangalie uwezekano pia katika maeneo yetu kuweza kusaidia baadhi ya maeneo kama vile Heruoshingo kwenye mpaka wetu na Burundi kule Kagera Ng'anda na Kitanga kuweza kupata mitandao hii. Mimi najua fika kama hawa ni wafanyabiashara, lakini kupitia kwako kama Wizara tunaweza pia tukatumia hizi simu kama nyenzo za usalama katika maeneo yaliyoko mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, habari ya Mkongo wa Taifa, Mheshimiwa Ngasongwa ameisema vizuri, għarama za simu kuwa ghali wenzangu wamelisema vizuri, sina haja ya kurudia. La mwisho, namwomba Profesa Msolla kitu kimoja, siku moja Profesa nimezungumza naye kama anakumbuka tukakubaliana kwamba Vyuo vingi hivi vya Sayansi na Teknolojia vimezagħaq katika Mji mikubwa tu. Kuna *DIT Dar es Salaam* pale, kuna *MIST Mbeya* sasa na Arusha na unakumbuka Prof. Msolla nikakunong'oneza, fikirieni namna ambayo mnawea mkatawanya hizi rasilimali za Vyuo vya Sayansi katika Mikoa mingine.

Tangu tumezungumza Mheshimiwa Prof. Msolla kule Kigoma tumekutengea hekta 2000 kwa ajili ya kuanzisha Chuo, fikiria. Anza kulifikiria hili kwa ajili ya kuanzisha Chuo cha Sayansi na Teknolojia katika Mkoħha wa Kigoma. Tumekutengea ardhi hiyo na utakapokuwa tayari. Kwa sababu najua utarudi Bungeni na mimi kuna kila

dalili za kurudi, tutashirikiana ili tuweze kuanzisha tawi lingine la Taasisi ya Sayansi na Teknolojia katika Mkoa wa Kigoma. Wewe mwenyewe unajua kwamba Mkoa wa Kigoma kihistoria una wanasayansi wengi, maana Mheshimiwa Prof. Msolla unajua hata yule mwanasayansi aliyepata tuzo ya *Nobel* alitokea Kasulu, yule Profesa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unamjua. Kwa hiyo, Kasulu ni eneo ambalo lina wanasayansi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na Profesa nakushukuru sana. (*Makofifi*)

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ilio mbele yetu. Awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Prof. Msolla na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya tangu wamepata Wizara hii. Kwa kweli hawa katika hotuba wametuonesha kwamba tunatoka kwenye ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya, tunakwenda sasa kwenye ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi, hongera sana. Vile vile nawatakia kila la heri kwa wapigakura wao waweze kurudi maana ni tunda adimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye hoja yenyewe nikianza kuwashukuru hawa Waziri na hasa Naibu Waziri kwa kazi nzuri aliyonisaidia kupata simu katika Jimbo langu la Bukene. Pale nilipokuwa nachukua Jimbo, simu zilikuwa za mkorogo, zile za kizamani kabisa. Lakini kutokana na ushirikiano tuliokuwanao na vile vile katika kusema ndani ya Bunge hili na kwa kwenda katika kampuni zile za *VodaCom* na wakati ule *Celtel* ambayo ni *Zain* sasa na *TIGO* ambayo wakati ule ilikuwa *Mobitel*, kwa hiyo, nimewenza kupata mitandao hii katika Jimbo la Bukene na sasa tumeondokana na ule mkorogo, tuko katika sayansi na tekinolojia, tuko kwenye simu za mkononi. Nawashukuru sana kwa ushirikiano wao, nawashukuru pia wananchi wa Bukene kwa kunisukuma ili niweze kuwasaidia kupata mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujikita zaidi kwenye simu kwa sababu ni kitu kinachotugusa zaidi wananchi wa Bukene. Nikizungumzia yale masuala ya sayansi na tekinolojam ile ya kama Mkongo wa Taifa, kule inakuwa juu zaidi kwa watu wangu wa Bukene. Maana tumetoka kwenye mkorogo, tunakuja kwenye simu za mkononi. Kwa hiyo, mimi naamini hata huo mkongo utatufikia tu, lakini kwa sasa hivi kwa lugha ya kikwetu na lugha ya Kiingereza tunasema *mashokoromageni*. Nawakoroga sio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye Jimbo la Bukene tumepeata mitandao kila mahali ila kuna sehemu tu ambayo imebaki ambayo nataka kusisitiza katika ngwe hii ya mwisho ndugu zangu hawa Waheshimiwa wanisaidie kusukuma makampuni hayo kwa kuleta mtandao huo kwa hizo sehemu. Nilizungumza ana kwa ana, nilizungumza na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari nikaambiwa niandike barua, nimeandika barua hiyo, nimeifikisha na nikaahidiwa katika maswali ya nyongeza hapa na pale kwamba watanisaidia kupata mtandao katika sehemu hizo.

Lakini mpaka nazungumza sasa hivi, mtandao huo bado, ndio maana nasema katika ngwe hii ya mwisho basi kwa kuwa tumemaliza ng'ombe mzima tumbakiza mkia, naomba basi tuhitimishe. Sehemu zenyewe ninazoziombea na kuzisisitizia maombi niliyotanguliza siku nyingi ni kwamba pale Semembela katika Kata ya Semembela mtandao haupatikani, kama walivyosema wenzangu, watu wanakwenda mlimani, wanakwenda kwenye visigi, wanakwenda kuongea na simu kutafuta mtandao ulivyo kwa mbali.

Kwa hiyo, pale katika Kata ya Mambali vile vile kuna sehemu inayoitwa Shilago na sehemu nyingine inaitwa Mbutu, pale vile vile hakuna mtandao unaoweza kupatikana. Halafu katika Kata ya Kahama ya Halanga kuna sehemu inaitwa Nabala na penyewe vile vile huwezi kupata mtandao kwa uzuri kwa ajili ya kuzungumza na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika Kata ya Karitu kuna sehemu inaitwa Bulunde na penyewe pana matatizo kama hayo. Kwa hiyo, kwa kutumia Bunge lako Tukufu ningeomba Wizara hii kuitia kwao wanisaidie kumaliza hivi visehemu vidogo vidogo ambavyo vimebaki, ni vidogo sana kuwasaidia wananchi wa sehemu hizo waweze kupata mtandao waweze kuzungumza na simu zao. Sehemu hizi ninazozizungumzia ni za biashara na mimi nilipokuwa nazunguka walipo kuwa wananiomba simu, niliwaambia tafadhali msiombe simu kwa ajili ya kuzungumza mambo ya kipuuzi, tafuteni simu kwa sababu ni ya ghali, tafuteni simu kwa ajili ya kufanya biashara na hii sehemu ni ya biashara.

Ukisema Semembela, maana yake ni wakulima, ukisema Semembela maana yake kuna mbao, ukisema Semembela maanake ni wafanyabiashara ndogo ndogo wanaoleta mazao kutoka shambani maporini kuleta katika Miji Mikuu kwa ajili ya kuuza mazao yao; ukisema Mbutu au Shilago maana yake tumbaku, ukisema Mbutu au Mambali maana yake asali (asali ya Tabora, *Honey*), inatoka katika Kata yangu iliyo nyingi ambayo ni Kata ya Mambali.

Kwa hiyo, ninavyozungumza, sehemu hizi maana yake nawaitia watu hawa walete biashara, halafu vile vile na wananchi wangu waweze ku-*communicate* biashara zao wanapopeleka asali zao, wanapopeleka mbao zao, wanapoleka mahindi yao au mpunga au tumbaku waweze kuuza kwa wakati na kupata siku hiyo hiyo wanapofikisha na kupata pesa zao. Naomba sana ndugu zangu hawa wanisaidie kuweza kupata hiyo na nimepeleka barua kweli na nimepata majibu kama watanisaidia. Kwa hiyo, ni hitimisho ili tuweze kumaliza ngwe hii na tufunge ukurasa wa mawasiliano na kwamba sitasema tena kuhusu mawasiliano na sisi twende juu zaidi tuzungumze na mambo mengine ya Kimataifa kuliko kuishia kwenye hii simu ya mkononi na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza kidogo, hivi inakuaje unapopiga simu siku hizi hasa simu za *TIGO* na simu za *Zain* kila dakika zinakatika, unapiga tena dakika mbili inakita? Unaona imeandika *hold* hamsikilizani, kunakuwa na kitu gani hapo? Utaalamu huo unakuaje?

Mimi naomba wataalamu wetu watuwekee mtiririko mzuri ili tunapozungumza hata kama kuna kurekodi, basi wamrekodi lakini bila kumvuruga mtu ambaye

anazungumza ili tuweze kwenda na mtiririko mzuri tunapozungumza na watu, hasa unapoangalia mtu anazungumza kwa ajili ya biashara na ametoa biashara unakata, anapiga tena, unaanza tena kum-*charge* unakata, kwa nini? Naomba Wizara hii iwaangalie wataalamu hawa na wenyewe wafanyakazi kwa kutimiza wajibu wao, wafanye kiutaalamu watimize majukumu yao ipasavyo. Kama ni kurekodi, warekodi bila kum-*disturb* yule anayezungumza ili wewe uende mtiririko sawa na gharama yote iende kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofî*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Lakini kwanza kabisa, nianze kwa kuipongeza sana Wizara, nimpongeze sana Waziri, Prof. Msolla na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya na hasa hii ya Mkongo wa Taifa. Tanzania itabadilika muda sio mrefu na ni imani yangu kwamba Watanzania pamoja na kwamba sio wengi wanaojua mkongo huu na mambo yake mazuri yanayokuja juu ya mkongo huu, lakini muda sio mrefu watashuhudia na mabadiliko ya nchi yatakuwa makubwa. Lakini nichukue nafasi hii pia kupongeza sana makampuni ya simu za mkononi ya *Zain* na *VodaCom* kwa kazi nzuri ambayo wamefanya katika Wilaya ya Mpwapwa na hususani Jimbo la Kibakwe kwa kutandaza katika baadhi ya maeneo minara ambayo inatoa huduma kwa karibu asilimia kubwa sasa katika Jimbo la Kibakwe.

Lakini niendeleze tu kilio changu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu nilishakwenda naye Jimboni kwangu kule Wota tulikokwenda hadi leo hii bado ule mnara uliojengwa haujaweza kusambazwa kwa kiasi kikubwa, sijui kuna tatizo gani la kitaalamu! Lakini mnara umejengwa na ni mkubwa, lakini mawasiliano yake hayafiki mbali, ni eneo dogo tu ambalo linaweza kuwa *covered* na *network* ya ule mnara. Sasa ningombwa kwa kutumia nafsi mliyokuwa mnafanya siku zote kwa kushawishi haya makampuni kwa kutusaidia kwa kutumia nafasi hiyo kuona namna gani wanawenza kufanya pale Wota kwa sababu ile Sekondari ambayo tunatarajia iwe *high school*, sasa bado *network* haifiki ambapo tulifika na Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri unakumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niombe sana kwamba Kata nytingine za Mbunga, Galigali na Ipera bado makampuni haya hayajaweza kufika na kuna uwanja mpana sana wa biashara na watu wenye uwezo wa kutumia mawasiliano haya, ningombwa sana mwone namna ya kuendelea kutusaidia kuyashawishi haya makampuni ili tuweze kupata mawasiliano katika maeneo hayo. Lakini liko tatizo la minara ambayo inatumia *satellite*, minara ile sasa ni karibu mwezi wa tatu imekufa kabisa.

Nadhani makampuni haya yanapata hasara kubwa kwa minara ile kwa sababu sielewi kwa nini hawaifanyii ukarabati ili iweze kufanya kazi kama minara mingine. Tulichoambiwa tu ni kwamba minara hii inatumia *satellite*. Kwa hiyo, teknolojia ile inasumbua na sina hakika kama wanawenza kubadilisha, lakini kikubwa tunachowaomba ni kwamba wajaribu kuona namna ya kuweza kufanya ili kuweza kurekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii pamoja na maeneo haya ya mawasiliano, lakini inayo eneo moja muhimu ambalo kwa hakika nataka kulizungumzia kwa nguvu kubwa. Eneo hili ni sayansi na tekinolojia na mimi nilitaka kuainisha namna sayansi na tekinolojia inavyochukua nafasi katika nchi yetu ya Tanzania na tuone kwa sababu Wizara hii ndio yenye dhamana: Je, Wizara hii imefanya jitihada zipi katika kusimamia maendeleo ya sayansi na tekinolojia? Kazi ya Wizara hii pamoja na kusimamia sera zilizopo, lakini kusimamia pia maendeleo ya sayansi na tekinolojia kwa maana ya vitu halisi. Kwa maana ya tafiti, kwa maana ya gunduzi mbalimbali na kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanatumia gunduzi hizi, wanatumia tafiti hizi kwa ajili ya kuongeza uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama nilivyowahi kusema hapa Bungeni ni kwamba mimi *background* yangu mimi ni fundi, lakini kwenye ufundi huko tumekimbia kwa sababu ya matatizo haya, ufundi unaonekana hauna *future* katika nchi ya Tanzania na kubwa kama kuna maeneo yanayokatisha tamaa ni eneo hili ambalo tafiti mbalimbali, gunduzi mbalimbali hazipewi nafasi, hazipewi fursa ya kuonekana hata katika soko la Tanzania, lakini pia hata soko la nje.

Ninakumbuka wakati nasoma ufundi wa magari nilitamani sana kufanya kazi kwenye kiwanda kile cha Mzinga cha Jeshi ambako walikuwa wameshaanza kutengeneza magari na yalikuwa yameanza kupita barabarani. Lakini leo hii yale magari waliyokuwa *wana-assemble* pale na tukafikiria namna ya kuanza kuyeyusha chuma, kutengeneza *block* na vitu vingine, usione chuma kilichopo Tanzania, usione *copper* iliyoko Tanzania, hakuna chochote kinachoyeyushwa na kutengenezwa kama *product*, vyote vinakwenda nje kama *raw material*. Je, nchi yetu tutaendelea?

Leo hii, China, India wako mbele, hivi sisi Tanzania ambao tuna kila kitu, tuna chuma, tuna shaba, tunafanyia nini hizi chuma na shaba? Kama viwanda hivi havitapewa nafasi kwa maana ya kuthamini tafiti na gunduzi mbalimbali kwa hakika nchi yetu hatutapiga hatua, tutabakia kusimamia sera. Eti mtu unajisifu kununua redio ya *transistor* moja kutoka China ya Sh. 2,500/= unasikiliza, unajisifu. Hivi si hata mwanafunzi wa Darasa la Saba Tanzania anaweza kutengeneza vitu mbalimbali! Lakini wako vijijini vijana ambao wanagundua vitu mbalimbali, wanaweza kurusha matangazo hata ya kilomita tano, nani anawashughulikia hawa? Hivi vipaji vyta Watanzania nani anayevishughulikia? Wanapelekwa wapi wakishagundua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma na mtu mmoja alikuwa anaitwa Mazuki. Mazuki aliletwa *Arusha Technical College* akiwa ametoka Iramba akiwa Mwalimu wa Shule ya Msingi, alikuwa amegundua *timing system* ya *engine* ya gari, leo hii anafundisha sijui Mwanza, sijui wapi ile habari aliyogundua imekwisha, hakuna anayeishughulikia, hakuna anayeithamini. Lakini naamini ziko gunduzi mbalimbali, wanakuja watu mbalimbali hapa Bungeni wanatuonesha vitu walivyogundua, wamekuja watu wanaotumia mashine zinazotumia *oil chafu*, nani anashughulika nao hawa? Je, kuna *budget implication* ya kuwashughulikia hawa? Tutabakia tunasindikiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata Korea walanza kwa kuamua. Ni lazima Serikali *i-invest* kwenye tafiti, ni lazima Serikali *i-invest* kwenye gunduzi hizi ndipo tutakapopata maendeleo. Hakuna mtu binafsi anayeweza *ku-invest* katika hizi gunduzi kwa sababu biashara yake ni ndefu na ni ngumu, lakini ni heshima kwa nchi kama tutagundua vitu. Hivi leo Tanzania hata balskeli hatuwezi kutengeneza, redio hatuwezi kutengeneza, sasa tunasema tuko kwenye safari ya duniani, sisi tuna sababu ya kuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kuna haja ya kufikiria upya na *ku-implement* sera itakayokuwa inasimamia na kuanzisha utaratibu mzima wa kuwasimamia watu wanaogundua vitu na tafiti mbalimbali. *Power tiller* ni teknolojia ndogo sana ambayo inaweza kutengenezeka. Mimi nilipokuwa nasoma *FTC* Arusha kule *college* nilifanya utafiti wa kutengeneza balskeli ya walemvu na tulitengeneza, lakini leo zinatengenezwa kwa kiasi kidogo sana na pengine hakuna hata soko la kufanyia hivyo, ile itakayotoka nje ndio ya maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepata fursa zaidi, lakini muda ni mchache, nizungumzie la mwisho, nalo ni suala zima la madini ya *uranium*. Kwenye ukurasa wa 54 imezungumzia Tume ya Mionzi, nguvu za *atomic*. Unapozungumzia *uranium*, unazungumzia bomu, unazungumzia *nuclear*. Hivi kweli Watanzania tuko tayari? Sio rahisi kwa mawazo yangu na hizi ni hisia zangu, mimi nadhani hatuko tayari na kama tunategemea, basi tunategemea hao wageni wanaokuja kuchimba kwa ajili ya kule kwao. Mimi ushauri wangu kwa Serikali, hebu tuwe makini na jambo hili tusikurupuke. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa George Simbachawene kwa mchango wako ambao unafukisha mwisho katika hatua hii, lakini tutaendelea jioni kama utaratibu wetu unavyoruhusu ili kumalizia masuala yanayohusu Wizara hii. Tutakaporudi saa kumi na moja, mchangiaji wetu aliyebakira hapa mezani ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Kiongozi wa Upinzani Bungeni, ndiye atakayekuwa mchangiaji pekee na nadhani kwa heshima yake tutampa robo saa ili Mheshimiwa Waziri apate kumsikiliza sawa sawa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mpangilio wa mezani hapa, inabidi nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni. Ahsanteni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tumbaki na mchangiaji mmoja ambaye ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa bahati mbaya bado simwoni hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunaendelea na ratiba.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla Waziri na timu yake, Naibu Waziri – Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu - Dr. Florens Martin Turuka, Naibu Katibu Mkuu - Dr. Patrick James Makungu, viongozi wote wanaongoza taasisi zilizo chini ya Wizara hii, *DITI, MIST, NM-AIST, TAEC, COSTECH, PPC, TTCL, TCRA na UCAF*. Bila kusahau, napenda kuwapongeza wanasayansi walio chini ya Wizara na Idara zake, taasisi na watoa huduma nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila Jemadari ambaye anaongoza na kuratibu mapigano, wanajeshi, wapiganaji, watasambaratishwa. Hivyo basi kwa moyo wa dhati na kwa niaba ya wananchi wa Rarya, natoa pongezi na shukrani nyingi kwa Rais wetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutambua umuhimu wa Sayansi na Technolojia kwa kuunda Wizara hii na kumteua Mwanasayansi, Prof. Peter Msolla na wasaidizi wake, madaktari na wakuu wa taasisi, maprofesa. Nasema hongera, Wizara imepata wachapakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi zangu hizo, napenda kutoa ushauri kama ifuatavyo:- Ukurasa wa nane kuhusu *Optic Febrer Cable* Mkongo wa Kitaifa, nashauri Mikoa 16 ya Tanzania Bara Ukurasa wa nane mpaka wa tisa wa kazi, taasisi, idara za Serikali na wananchi wapatiwe huduma inayostahili, vituo vya mawasiliano viongezwe katika Mikoa hiyo; ulinzi wa kutosha uimarishwe kwa lengo la kulinda mkongo na utafiti ufanyike ili kuhakiki gharama ya kuzungumza kwa kuwa wanaobebeshwa mzigo ni watumiaji ambao ni wananchi wenyewe mapato ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni 14 zinazotoa huduma za mawasiliano ya simu hivyo, nashauri wahamasishwe kupeleka huduma pembazoni mwa nchi yetu kama Rarya, Mpanda na Kasulu kwa kutaja Wilaya chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 28 wa hotuba ya Waziri kuhusu vituo vya mawasiliano Vijijini (*Telecentre*), napenda kumpongeza Prof. Mwenzangu, Mheshimiwa Msolla na timu yake kwa Wizara yake kuja kutupatia kituo cha mawasiliano vijijiji (*Telecentre*) katika Wilaya mpya Rarya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Rarya kiko pembezoni ya nchi yetu, wananchi wanaomba kituo hiki ambacho kitakuwa kitovu cha mawasiliano kwa Wolaya jirani kipewe kipaumbe kwa kuongezewa vyombo vya kisasa na kuongezewa wataalamu kwa kuwapatia mafunzo wasimamizi wa kituo hiki. Wananchi wanaomba Mungu Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wapate kurudi kuongoza Wizara hii, wamefanyakazi nzuri kwa kuendeleza Taifa katika nyanja ya mawasiliano na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu awabariki. Naunga mkono kwa asilimia mia moja na zaidi.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naandika mchango wangu wa mawazo kwa lengo la kuwapongeza Wizara husika hasa Mheshimiwa Waziri Prof. Msolla na Naibu Waziri wake Dr. Maua Daftari, kwa kuwasilisha hoja yao hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nataka iingie kwenye rekodi ya *Hansard* kwamba namshukuru na kumpongeza binafsi Mheshimiwa Dr. Maua Daftari - Naibu Waziri wa Wizara hii kwamba ametoa mchango mkubwa sana kufanikisha mtando wa simu vijijiini, kwenye Vijiji vyangu vyote kasoro kimoja cha Goziba na Kata zote 12. Ninamshukutru sana Mheshimiwa Dr. Maua Daftari kwani hata Kijiji kilichobakia tayari amewasilisha maombi yangu ya kuwafikishia mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Goziba, sasa kimepewa hadhi ya kuwa Kata. Kata hii yenye jina Goziba, inajitegemea kiuchumi. Ni Kata inayotoa mchango mkubwa kiuchumi katika Wilaya ya Muleba. Kwa maana hiyo, naendelea kuomba kwa kasi zaidi kwamba Goziba mpya ambayo ni Kata ipatiwe mtando. Naomba makampuni mbalimbali yaende yakaone namna nzuri ya kupeleka kule mtando. Naelewa pana mazingira magumu hasa kwa kuwa ni Kisiwa katikati ya *Ziwa Victoria*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara pia ituunge mkono hasa mimi kwani nimeanzisha Shule ya Wasichana ya Sekondari ambayo itakuwa na mchepuo wa sayansi na ufundi. Sekondari hii ipo katika hatua ya kuezeka vyumba vitano vya madarasa na jengo la utawala tayari limeezekwa. Kilichobaki ni kuweke milango, madirisha, kupiga plastika na kuweka samani. Tunakusudia pia kufanya *wiring* kwani tunataka iwe na umeme moja kwa moja. Kwa maelezo haya, naomba Wizara ituunge mkono ili tujenge kwa kasi, ituchangie angalau vifaa katika vyumba vitatu vya maabara za kemia, fikizia na biolojia. Pia, tukifungua (maana tunakusudia kuanza mwakani) tupatiwe vitabu vya kiada na ziada na kompyuta na walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa leo, nataka nielezee kidogo la gharama za simu. Wanajaribu kupunguza gharama za mazungumzo siku hadi siku. Lakini *SMS* bado ziko juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado naamini kuwa pamoja na punguzo hilo, bado gharama hizi ziko juu. Nawapongeza kwa kuwa *Tigo* kwa *Tigo* ni ndogo, na *Zain* kwa *Zain* kuanzia saa tano usiku hadi asubuhi ni ndogo sana. Lakini je, hawawezi kuacha malipo hayo madogo muda wote na kwa simu zote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri gharama za simu na meseji ziangaliwe upya kwa maana ya kuzipunguza zaidi. Hizi gharama za sasa bado mimi naona ni kubwa sana. Wafanye kuchaji kwa sekunde na isiwe zaidi ya shilingi moja kwa sekunde kwa saa zote na kwa simu zote. Aidha, gharama ya mtando mmoja kwenda mwingine wa kampuni tofauti, gharama zipunguzwe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa hotuba ya bajeti ya Wizara hiyo iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Baada ya kuipitia hotuba hiyo, ninaafiki moja kwa moja na kuunga mkono kwa asilimia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, ninapenda kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mtindo wa baadhi ya watu waishio kwa mashaka kutokana na wafanyayo, ambao wanawarubuni baadhi ya *operators* wa simu za mkononi kuwa wana-tape wanaowapigia simu kwa manufaa yao. Kiutaratibu ni vyombo vy'a dola vinavyoruhusiwa kufanya hivyo tofauti na sasa *operators* hao wanahongwa fedha na kufanya kazi hiyo.

Ninapendekeza Wizara isimamie zoezi la kuwapata watumishi waaminifu na weny'e sifa na kutoa agizo kwa weny'e makampuni kuwachukulia hatua ya kuwafukuza wale wote wanaobainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo zoezi la mkongo wa Taifa ambapo katika mpango, Kigoma naona haimo. Ninaomba Kigoma nayo na Wilaya zake iwemo katika zoezi hilo kwa sababu Kigoma inalo tatizo kubwa la mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara isimamie bei ya mazungumzo (*airtime*) kwa sababu ni mzigo kwa wananchi na hususani wale waishio Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma na Wilaya zake wanayo minara ya kila kampuni ya simu iliyoaamua kupeleka mawasiliano yake huko. Tatizo ni masafa yanayosababisha mawasiliano kutokuwa mazuri. Ninaishauri Wizara iwhahimize weny'e makampuni huko kusimamia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Murungu Wilayani Kibondo hawana mawasiliano kabisa hadi mtu apande juu ya mti. Ninaomba Wizara isimamie zoezi la kujengwa kwa mnara kwenye Kata hiyo ili wananchi hao waweze kuwa na mawasiliano. Hili ni ombi ambalo nilipewa na wananchi hao na kushughulika nalo kwa miaka mitano bila mafanikio. Naomba hili lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Posta wamekuwa na kiwanja walichopewa na Wilaya ya Kibondo kwa muda wa miaka mitano sasa bila kuendelezwa. Ni vyema kiwanja hicho sasa kijengwe ama tukubaliane wapaewe watu (kampuni nyingine iliyoonesha nia ya kukitaka na kukiendeleza).

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hii hasa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wa Wizara na Taasisi zake zote kwa kazi nzuri wanazofanya na kwa pekee, kwa ushirikiano mkubwa wanaotoa kwa Kamati ya Bunge ya miundombinu, Bunge na wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri, mapendekezo, na maombi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuundwa kwa Mamlaka ya Utafiti, Serikali iimarishe mfumo uliopo sasa ili Mamlaka kweli iwe ndio kiongozi kwa utendaji wa mfumo wa utafiti nchini na kuongoza mikakati na mafungu ya fedha za utafiti ambazo sasa zinaingizwa kama sehemu ya kasma katika Wizara mbalimbali na kusimamiwa na kutolewa maamuzi na Wizara ya Fedha bila kushirikisha Mamlaka ya Utafiti.

Pia nashauri Serikali itenge fedha za kutosha ili kujenga na kuimarisha maabara za kufanya utafiti, kuhifadhi na kuendeleza matokeo ya utafti katika sekta zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Taifa linaelekea katika mkakati na kuvuna madini ya kemikali, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, na Wizara ya Nishati na Madini zinapaswa kushirikiana kuandaa wataalamu watakaowezesha kuainisha matumizi bora ya madini hayo ya kemikali kuandaa wazawa (Watanzania) watakaowezwa kufanya kazi na kusimamia mfumo mzima wa matumizi ya madini hayo ya kemikali kwa usalama bila kuhatarisha maisha ya wafanyakazi, wananchi, na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga uwezo wa uchambuzi wa mikataba ili kulisaidia Taifa kuingia katika mikataba bora itakayonufaisha Taifa na nchini na sio kuacha mwanya kwa wawekezaji kujinufaisha kutohakana na kutokuwa na upeo na uelewa wa kazi na manufaa ya madini hayo ya kemikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionzi ina athari kubwa katika mfumo na maumbo ya binadamu. Matumizi ya simu za mkononi, mashine za ukaguzi wa usalama katika maeneo ya kazi, na njia za usafiri yameongezeka kwa kasi. Mamlaka/Bodi ya Utafiti iongeze nguvu ya kutathmini mifumo hii ili kutoa ushauri na njia bora ya kutumia vifaa hivyo ili kupunguza athari kwa wananchi wanaotumia vifaa hivyo.

Kuboresha mawasiliano Wilayani Muheza (Simu za Mkononi):-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya kampuni za *VodaCom*, *Zain* na *Tigo* bado siyo mazuri katika Tarafa ya Amani yenyewe Kata za Amani, Zirai, Mbomole, Misalai, Kisiwani. Hii inatokana pia na kuwepo kwa milima na mabonde mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wenyeji wa maeneo hayo wanafahamu maeneo mazuri ya kuweka minara ili kuunganisha mawasiliano kwa maeneo makubwa zaidi. Nashauri kampuni hizo za simu za mkononi ziwatumi wazee na wananchi hao kupata msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Kiwanda, Kata ya Kiwanda na Nkumba kipo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Zahanati, Shule tatu za Msisngi, Kiwanda, Mangubu na Tongwe. Mawasiliano ni ya shida sana licha ya idadi ya watu wenye uwezo wa kutumia simu za mkononi ni wengi. Tunaomba msaada kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mtendaji Mkuu wa *TCRA* na watendaji wote walio chini ya Wizara hii muhimu, kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kipindi chote cha miaka mitano ya Awamu ya Nne na pia kwa kuandaa bajeti yenye mwelekeo wenye kuleta matumaini kwa wananchi na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wimbi la watumiaji wa simu za mikononi, kuna baadhi yao wanazitumia vibaya kwa kutukana watu wengine, kutoa vitisho na uhalifu kama wizi na ujambazi na mipango mibaya ya kumdhuru mwanadamu. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuwa na teknolojia itakayoweza kuwabaini wale wahalifu wanaotumia simu za mikononi kuwadhuru wenzao kwa kuwatukana na kuwatisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano *TCRA*, iangalie uwezekano wa kuongeza muda wa kusajili simu maana kuna idadi kubwa ya wananchi hawajasajili simu zao kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ugonjwa, safari nje ya nchi na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kubwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano *TCRA*, kwa kazi nzuri, ilioleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Natoa pongezi nyingi kwa Wizara, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri. Naomba ufanuzi kuhusu mpango wa ujenzi wa Mkonga wa Taifa hauonyeshi programu za kufikisha Mkonga huo Mtwara kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa Wizara kuongeza muda wa kusajili simu lakini hapa Bungeni mwaka jana kampuni za simu ziliweka watu wa kusajili simu na sisi Wabunge tulisajili simu zetu leo tunaelezwa tuulize kama simu zetu zimesajilliwa kwani tuliosajili simu zetu hapa Bungeni ilikuwa danganya toto? Nani atabeba lawama ikiwa simu zetu zitafungwa wakati zilikuwa zimesajiliwa tayari? Kosa ni la nani? La mwenye simu au kampuni? Je, ikithibitika kuwa simu iliyo fungwa ilikuwa imesajiliwa kutakuwa na haki ya kudai fidia kwa usumbufu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba huduma za simu za mikononi Kongwa Vijijini kwa kampuni za *VODACOM, ZANTEL, TIGO, TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru ZAIN kwa mtandao mpana vijiji ni Kongwa. Hao wengine wahimizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadahiliwa katika Vyuo Vikuu nchini wa masomo ya Sayansi na Teknolojia ni wachache sana, hata Walimu katika Shule za Sekondari wa Masomo ya Sayansi ni kama hawapo. Wizara ina mkakati gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, TTCL inasuasua, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ambazo zinapitiwa na Mkonga wa Taifa kama Kongwa zinafaidikaje na Mkongo huo?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ambazo zinapitiwa na Mkongo wa Taifa kama Kongwa zinafaidikaje na mkongo huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahitimu waliosoma masomo ya sayansi, wakiajiriwa hawapati malipo mazuri kama Manesi, Madaktari, Wahandisi na kadhalika. *Encouragement* kwa vijana kusoma masomo magumu na ya miaka minge inakuwa ndogo.

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuendeleza shughuli za *fiber optic cables*. Nafurahi zaidi kwamba *SEACOM* na *EASSY* watashindana. Nafurahi zaidi kwamba Wilaya zote zitaunganishwa tayari kwa uendeshaji wa *E-government* na *E-commerce*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa Wilaya ya Rombo, ninapenda kutoa rai kwamba vituo vya mpakani Tarakea na Holili vifikiwe ili kuunganisha na Jamhuri ya Kenya katika Wilaya na Miji ya Loitoktok na Taveta. Tayari maeneo hayo yameunganishwa kwa barabara za lami za Afrika Mashariki, kuishia Makao Makuu tu ni kukosa fursa hizo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, bado Wilaya ya Rombo haina usikivu mzuri wa redio, wananchi wanategemea sana redio za Kenya za Serikali na watu binafsi. Ahadi za toka miaka ya 1990s kwamba tungepewa *boosters* hazijatekelezwa na hivyo kuwa kero hivi sasa. Naamini kuwa Wizara hii inaweza katuondolea kero hii kupitia *TEKNOHAMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Posta, ni lini wazo la kulishirikisha na Benki ya Posta litatekelezwa, hii ni kwa sababu Posta wana mtandao mpana sana kote nchini ambao hautumiki kikamilifu (*under capacity*). Huko nyuma Shirika lilifanya shughuli za akiba (*savings*). Vijiji bado wananchi hawana huduma hizi kwa karibu. Tuige pia shughuli za akina *Vodacom Shops/M-Pesa*. Nia iwe ni kupokea fedha, kulipa fedha na ikiwezekana kukopesha (*savings, payment, credit*) kibiashara na kwa gharama nafuu. Mpango huu pia utasaidia Kilimo Kwanza kwa wakulima wadogo wadogo, wenye viwanda vidogo vidogo na wafanyabiashara wadogo vijiji. Ni suala la Serikali hususani Wizara ya Fedha na Wizara ya Mawasiliano kujenga hoja ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MHE.PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi na shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii. Aidha, kwa kupitia Wizara yako, naomba niyashukuru makampuni ya simu ya viganjani kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Rufiji, tunashukuru kwa kupata minara ya mawasiliano, mathalani Miji ya Utete, Ikwiriri, Mohoro na Kibiti. Kampuni zote zina minara yake katika Miji hiyo na usikivu ni mzuri. *ZAIN*, *VODACOM*, *TIGO*, na *ZANTEL* tayari wapo na wanafanya biashara nzuri sana. Vijiji vingine vinavyopata huduma za mawasiliano ni Mloka, Kilimani, Mkongo, Nyamwage na Kijiji cha Mbwara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi binafsi natoa shukurani zangu za dhati kwenu, kwa kuchukuwa hatua za haraka ya kukazia maombi yangu ya kutupatia minara zaidi katika Jimbo langu, Mawaziri hawa huchukua hatua za haraka za kuyaandikia makampuni ya simu na kuwapa rai ili yafanye hivyo haraka kutuongzeza minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara izidi kuyaomba makampuni ya simu ya viganjani ili watujengee minara mingi katika Vijiji vya Jimboni kwangu navyo ni Vijiji vya Nyaminywili au Kipungira, Ruwe, Nambunju na Kijiji cha Chumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri. Mchango wangu utahusu mawasiliano ya simu za mkononi, hususani katika Jimbo langu la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara kwa msaada mkubwa walionipa katika kuwasiliana na makampuni mbalimbali ya simu hapa nchini. Hapa ninapenda nimpongeze Naibu Waziri, Daktari Maua Daftari, kwa msaada wake mpaka hivi leo katika Kata zangu 19, Kata 17 zina minara na mawasiliano ya simu. Naomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri anipe msaada zaidi kwa zile Kata mbili za Uchindile na Taweta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu barua za awali kwa makampuni hayo zilishaenda kuhusu Kata hizo mbili, lakini msukumo wa Wizara utanisaidia ili wananchi wale ambaeo eneo lao limefunguka kiuchumi kutokana na upandaji miti waweze kuwa na mawasiliano ya simu.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia muda huu ni mzima. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na wataalamu wake kwa hotuba yake iliyojaa ukweli. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri aliposhirikiana na Naibu wake kwa kuweza

kunipatia minara miwili ya ZANTEL katika Jimbo langu ambayo imetuwezesha kuwasiliana kwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Wizara inawasilisha bajeti yake, leo ni tarehe 30 Juni, 2010. Ni siku ya mwisho ambayo ilitangazwa kusajili simu. Hivi karibuni *TBC* (*TV*) wakati ikihojiana na Wakuu wa mitandao walisema simu milioni nne bado hazijasajiliwa. Napata wasiwasi wa kuwa leo itapita na bado kutakuwa na simu ambazo hazijasajiliwa, je, ni utaratibu gani utatumika kuzinusuru simu hizi na zoezi hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiwa na Kamati yangu ya Bunge, tulitembelea Tarime, nilifika maeneo ya Kata za Nyanungu, Muriba, nikakosa mawasiliano, je, ni mipango gani Wizara imejiandaa kuwasaidia wananchi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imefanikiwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa ambao ulianza tokea Julai, 2009, dhana kuu kwa Watanzania ni kupata mawasiliano. Leo kuna Mikoa kama vile Ruvuma, Mtwara, Rukwa, Lindi na Tabora mpaka leo haijaunganishwa na Mkongo wa Taifa. Je, ni lini Mikoa hiyo itapata huduma hii kwa kuunganishwa na Mkongo huo wa Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza mchango wangu, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Peter M. Msolla, pia Naibu wake Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kwa imani yao iliyotupelekea kuifanya Tanzania yetu kuwa kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia viongozi wetu hawa amba ni Wasemaji Wakuu wa Serikali juu ya Wizara hii, nawaomba wawasaidie Watanzania wenzao juu ya gharama za simu kutoka mtandao fulani kwenda mtandao mwingine. Jambo hili linatisha, gharama zake, ni kubwa mno, ukipiga simu kutoka *Zantel* kwenda *Tigo*, gharama ni kubwa mno. Naiomba Serikali iyaombe makampuni haya yaweze kuwasaidia wananchi wetu. Kwa kufanya hivyo ni kumwezesha Mtanzania kupata Maisha Bora kwa Kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwa maandishi. Nianze kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wakurugenzi mbalimbli wa vitengo/idara katika Wizara hii. Kazi ya miaka mitano imekuwa nzuri sana imeonekana katika idara mbalimbali na Wizara kwa ujumla. Ila naomba nitoe maoni yangu machache tu katika kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa mtandao wa huduma za simu za mezani na za viganjani hadi ngazi za vijijini, ukweli huduma hiyo imeshafika maeneo mengi ya vijijini, lakini pia bado kuna vijiji vingi hawajapata, naomba sana Wizara ijitahidi kuwashawishi wenyewe makampuni wafakishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo la huduma ya mtandao maeneo yasiyokaliwa na watu yaliyopo kwenye barabara kuu zitumiwazo na abiria wawapo safarini kwani hata ukipata tatizo, sio rahisi ukapata huduma, mtandao huwa haupo labda

Zantel ndio kidogo wamejitatihidi, mtandao wao una nguvu kiasi na porini unawenza ukabahatisha. Hivyo, ufanye utaratibu wa kuwepo kwa huduma hiyo, mfano barabara ya Nyakanazi – Kibondo – Kasulu – Kigoma ni misitu ya hatari sana lakini mtandao hakuna ama Nyakanazi hadi Ngara. Hiyo ni mfano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba nawapongeza *TCRA* kwa kazi nyingi nzuri wanazofanya mwaka hadi mwaka wanazidi kupanda. Ombi langu kwao kwa kuwa wao *TCRA* ndio wasimamizi wakuu wa vyombo vya habari, nawaomba wasaidie kuweka utaratibu wa kuwabana wamiliki wa *TV* na *Redio* waweze kulipa mirahaba ya kazi za wasanii wanazotumia katika *TV* zao na *Redio*. Naamini wakilipa nafasi na wakaliwekea utaratibu wa kuwabana hasa wanapokuja ku-renew leseni zao, wawaombe hati ya kulipia mirahaba toka *COSOTA*. Hati ya malipo hayo pia iwe ndio kigezo kimojawapo cha kufuzu kupata leseni mpya. Itakuwa imesaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha huduma ya posta, ni vyema kuwe na anuani za mitaa, vijiji na kadhalika kwa nchi nzima na hata mijini, kwani bila hivyo ni ngumu sana. Ni vyema kila nyumba iwe na *Post Code*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara inawatambua Watanzania waishio nje ya Tanzania ambao ni wabunifu? Je, ni kina nani na inawatumiaji? Je, hapa nchini kuna wabunifu wangapi waliosajiliwa na nchi imefaidikaje kwa ubunifu wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nashukuru, nawetakia baraka za Mungu wetu na tuombeane tena ili tukutane Novemba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ANIA SAID CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa maandishi hotubu ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2010/2011. Pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua kubwa imefikiwa kwa ajili ya mawasiliano, lakini naomba liangaliwe eneo kwa hizi kampuni za simu *Voda*, *Tigo*, *Zantel* na *Zain*. Hivi sasa watu wanazimika kubeba simu zaidi ya moja, ili kupata urahisi wa mawasiliano, ningependa utoe maelezo ya ziada ni sababu zipi kampuni hizi haziweki mazingira ya watu watumie simu moja, usumbufu wa mtandao uliopo kwenda mtandao mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mitandao inasajili simu nchi nzima, inaonekana hawakujiaadaa ipasavyo leo ni mwisho kujisajili, mazingira ya nchi yetu yalivyo magumu, hata taarifa kufika Makao Makuu ya Kampuni hizo, pia ukisajili na unapewa udhibitisho wa usajili ukipiga simu unaambiwa hujasajili namba yako hali hii ni vyema muda wa usajili uongezwe ili lengo lifikiwe, kama lilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa ya kusambaza mkongo (Optic Fibre) wa njia za kupitishia mawasiliano, serikali itoe taarifa juu ya utekekezaji wa mkongo wa Taifa.

MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri yenye kueleweka. Inafurahisha kwamba mkongo umekamilika na umeanza kutoa huduma hasa kwa nchi za majirani zetu ukiwa ni njia mojawapo ya kuendeleza uchumi hivyo nasisitiza na hizo sehemu zilizobaki ndani ya nchi yetu zikamilishwe ili huduma ziweze kupatikana kwa urahisi zaidi na wananchi tufaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pesa za utafiti kwa huo huo utafiti ufanyike kila sehemu Wizara, Mashirika na makundi maalum kama vile vijana, wazee na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu teknolojia naomba na watu wenye ulemavu nao wafikiriwe ili nao waweze kuzitumia ndani ya nchi yao, kama vile kompyuta, simu, ATM na kadhalika, wenzetu nje huduma hizi wanazifanya wenyewe bila ya msaada wa mtu ye yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia Wizara kila la kheri na mafanikio mema.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote natanguliza kwa kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara husika wakiongozwa na Katibu Mkuu, hakika kazi iliyofanyika ni kubwa na inatia matumaini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nipongeze Wizara kwa kukamilisha awamu ya kwanza ya mkongo wa Taifa na sehemu mojawapo ilipofika ni Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na baadhi ya wajasiriamali (*ISPs*) kuijandaa kuunganishwa kwenye mkongo, walikumbana na matatizo yafuatayo, kwanza hakuna kiunganisho (*interface*) sababu zinazotolewa ni kwamba hakuna kiunganisho cha *fibre* ya mjasiriamali na ile ya mkongo. Tatizo ni kwamba *specifications* lazima zitolewe na Mchina aliyejenga mkongo. Walipoomba *contacts* zao waliambiwa ni mpaka kiunganisho kitengenezwe kiwandani kwa ajili yao, kwa sababu vilivyopo ni vya *project lead time* kama wakitoa *order* ni miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wajasiriamali hawa waunganishwe mapema ili waweze kutoa huduma katika shule, vyuo, taasisi za utafiti, taasisi za umma, hospitali,

maktaba na sehemu zingine zinazotoa huduma kwa umma wapewe kipaumbele na pia wapewe *internet bandwidth* ya bei nafuu ili waweze kushusha gharama kwa taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau hao wako tayari kutoa ushirikiano wa kitaalamu kufanikisha jambo hili ili hatimaye mkongo uwe na manufaa ya kweli kwa wananchi wa kawaida na siyo kwa taasisi za Serikali tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmojawapo ni Dr. H. E. Kavishe, *Director – Kicheko Ltd.* Tel. 0715 – 210113, Emai:l info@kicheko.com. Skype [hkavishe](#), Msn kavishe@kicheko.com.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa leo Mjini Mbulu, *Vodacom* wanazindua *product* mpya kwa ajili ya watu wa vijijini lakini mtandao wao haufiki huko. *Vodacom* watawatumiwa wajasiriamali wadogo hamsini ambao wasasambazwa vijijini kuuza *airtime* bila kutumia vocha, kutoa huduma za kupiga simu, *sms* na huduma ya M-pesa, kwa kutumia simu ya jamii. Ombi letu kwa Wizara ni kuongeza sauti yake kwenye maombi yetu ya kuongezewa minara, siyo tu ya *Vodacom* bali pia *Zain* na *Tigo*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkongo wa Taifa, hivi kwa nini Makao Makuu ya Wilaya yanayofikiwa na mkongo wa *TANESCO* kwa sasa yasiunganishwe katika mkongo wa Taifa sambamba na mikoa? Je, ni kampuni gani itaziunganisha Tarafa, Kata na Vijiji na mkongo wa Taifa?

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri yeye, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari , Katibu Mkuu na wasaidizi wao kazi nzuri na hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa usimamizi mzuri wa mitandao ya simu hasa za viganjani, lakini simu za *TTCL* nyaya haziendi kwa kasi tulioitegemea. Napenda niwakumbushe kuwa *TTCL* waliahidi katika Wilaya ya Kisarawe kuweka vituo vya simu kwa umma (*public telephone kiosks*) katika maeneo ya Masaki, Maneromango, Mzenga, Msanga na Chale. Ahadi hii ilitolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwangu hata kabla ya Wizara mpya haijaundwa. Namshukuru sana. Lakini ahadi hii imebaki kuwa ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa kuna simu za viganjani, Wanakisarawe kule vijijini wamehamasika sana hasa kwa kuona minara mingi imefurika pale Makao Makuu ya Wilaya. Kwa bahati mbaya bado kuna maeneo mengi kule vijijini hakuna minara, hivyo mawasiliano ya simu katika maeneo hayo bado ni tatizo, ingawa kampuni ya *Zain* angalau imejitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisarawe ni Wilaya iliyopakana na Dar es Salaam. Haipendezi kuona kuwa Wilaya za mbali na Dar es Salaam ziwe na mawasiliano mazuri wakati Kisarawe ina shida. Watumiaji wa simu wapo wengi na simu wanazo tele, lakini

mitandao ni hafifu. Naomba Mheshimiwa Waziri, Wizara yako iwashamashe hasa *Voda, Tigo* na *Zantel* waongeze minara katika maeneo ya Kisarawe Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha huduma za *TEKNOHAMA* ni faraja kwa Watanzania hasa kwa kuboresha mitandao ya afya na elimu (*tele-medicine* na *E-learning*). Naona kwa Mkoa wa Pwani mmetoa umuhimu wa kuunganisha mkongo na Kibaha na Bagamoyo. Wenzetu hawa wana mawasiliano mazuri, barabara safi na huduma za umeme na kadhalika. Ningeshauri kwa hili basi na maeneo ya karibu na Dar es Salaam ambayo hayana huduma nyingine nzuri yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Kisarawe nayo ihusishwe mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Wizara hii. Aidha, natoa ushauri eneo la Mikumi hadi Ruaha Mbuyuni hadi Mahenge ni vyema kukawa na mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni wa kuuza *shares* za Mashirika ya simu kama *Voda/Celtel/Tigo*. Vyema *shares* zikawa *owned* na baadhi ya Watanzania (*public*) kama nchi zingine wanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za simu nchini bado ni kubwa sana, ombi langu ni kuwa gharama zipungue.

MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Peter MsoLla, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Maua Daftari pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa juhudni kubwa wanayoifanya hasa ya kutuingiza katika matumizi ya sayansi na teknolojia katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache niliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya uhakika hasa katika maeneo ya vijijini imekuwa ni tatizo hasa kwa vile watu wengi kwa sasa wamenunua simu za mikononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi za maeneo ya vijijini mawasiliano ni tatizo hasa katika maeneo yangu ya Kata ya Ilungu, Lwiji na hata Ilomba kila wakati akipiga simu utajibiwa mitambo ni mibovu. Naomba kuongeza nguvu ya mitambo katika sehemu ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu pia utahusu eneo la Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Misitu Mbeya. Kumekuwa na uvumi kwamba eneo lingine la misitu

litaongezwa na hali hiyo imeleta wasiiasi mkubwa kwa wananchi. Kama habari hii ni ya kweli basi ni vizuri utaratibu wa taarifa kwa wananchi uwe wa uhakika. Waelimishwe, wajulishwe na hatimaye zoezi la kupima eneo hilo lianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa eneo uende sambamba na malipo ya fidia kwa sababu baada ya kupima fidia inachukua muda mrefu na kuwaacha wananchi wakihangaika bila kuwa na mahali pa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili la wananchi wa eneo karibu na misitu na kata ya Igale lipewe suluhisho la kudumu na lijibiwe pia katika Bunge hili ili kuwaondolea wananchi wasiiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kutuletea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya simu yanasaidia sana kurahisisha shughuli za jamii na uchumi pia. Wananchi wa Wilaya ya Urambo hawapati kabisa mtandao wa *Tigo*. Maeneo yote kuanzia pale mjini Wilayani na Kata zake zote 24. Kampuni hii imekuwa inaahidi kuweka minara Wilayani Urambo tangu 2007 hadi leo bado Serikali itueleze ni lini mawasilino ya *Tigo* yatakuwepo Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa *Zain* pia minara ni michache sana. Iko mbali na *network* ni ya taabu sana, Kata zile za Uyowa, Kashishi, Ichomba na Mwongozo, Kata zile za Usoke Mlimani wananchi inabidi wapande kwenye miti ili wapate mawasiliano jambo ambalo ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madhara yatokanayo na kusikiliza simu kwenye sikio kwa muda mrefu. Madhara haya yanaongezeka kila siku, masikio yanauma pale ambapo unaweka simu kusikiliza.

Mimi mwenyewe nimepata madhara hayo. Nimekwenda kwa Daktari wa masikio wa Muhimbili akanieleza kweli wamekuwa wanapata kesi kama hii kutoka kwa watu wanaotumia sana simu. Jambo la ajabu aliniambia wao kama madaktari hawajajua nini haswa tatizo bado wanaendelea kufanya utafiti. Naomba Wizara hii itafute wataalam haraka waangalie suala hili ili kuepusha madhara kuendelea na baadaye isiwe *too late* hata kupata tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hata watoto wadogo miaka miwili na kuendelea wanaongea na simu, hii ni hatari sana, Serikali itoe tamko hapa Bungeni kuwa wazazi wasiwapo watoto simu inawezekana kwa kulifumbia macho tukawa na watu wasiokuwa na usikivu mzuri (viziwi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano inapotaka kutoa kibali cha ujenzi wa viwanja vya ndege iwasiliane kwanza na sekta inayohusiana na mambo ya ardhi ya eneo hilo. Mamlaka imetoa vibali vya kujenga kiwanja cha ndege Loliondo kwa Kampuni ya ABC ya uwindaji kwenye mapito ya wanyama, pia ndani ya eneo moja wametoa vibali vya kuweka viwanja vya ndege viwili kwa nini? Ni kwa nini Kampuni hizi mbili mpya, ya uwindaji na ile ya kupiga picha wasitumie kiwanja kimoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuharibu mapito ya wanyamapori lakini pia tuna wasiwasi viwanja hivi vinatumika kutorosha rasilimali za Watanzania kuna usiri mkubwa kuhusu mali zinazochukuliwa kupitia viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano ifanye marekebisho ya Sheria zake ili kuweka kifungu cha kutoa adhabu kwa watu wanaotumia simu kutukana viongozi pia kwenye *internet* wanaweka picha za ngono na picha zisizostahili.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Maua Daftari na Katibu Mkuu Dr. Turuka kwa kazi nzuri wanayofanya kwenye Wizara hii. Kwa ushirikiano na utii wa hali ya juu, viongozi hawa wamefanikisha kushawishi Kampuni za simu za viganjanai kupeleka mawasiliano ya simu hasa vijijni. Hivyo naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo ule ule wa matumaini namuomba sana Mheshimiwa Waziri ashawishike. Kampuni za simu kufikisha huduma maeneo yafuatayo, Segese Wilayani Kahama, Ngogwa Wilayani Kahama na Isaka – Jaana - Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii ambayo ina lengo la kuboresha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua uwezo na juhudi za Waziri Mheshimiwa Profesa Msolla na Naibu Waziri dada yangu Mheshimiwa Dr. Maua Daftari pengine ni vyema kuunga mkono hoja hii kabla sijatoa maoni yangu kwenye maeneo kadhaa na Mungu awape nguvu, afya na wapiga kura wao wawarudishe kwa kura za kishindo ili warudi kutekeleza mambo waloyandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maombi ya mawasiliano kwa simu za mikononi, napenda kuipongeza Serikali kwa kupeleka mawasiliano ya simu za mkononi za *Tigo, Zain, Vodacom, Zantel* na kadhalika mkoani Singida hadi vijijini kwa Wilaya

zote. Kwa kuwa kuna maeneo ambayo bado hayana mawasiliano mfano Tarafa ya Nkonko Kata za Heka, Nkonko, Iseke na Sanza.

Swali, je, lini mawasiliano ya simu za mkononi yatafika huko ili wananchi wanaoishi huko waweze kutumia simu za mkononi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo la mawasiliano Kata ya Rungwa ingawa mnara upo Rungwa wa *Vodacom* lakini kijiji cha Mwamagembe chenye wakazi wengi na uchumi wao uko juu kuitia mifugo na kilimo cha alizeti na pamba pamoja na vijiji vya Kintanula na Kalangali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mitundu ina mnara lakini kuna tatizo la mawasiliano vijiji vya Itagata, Lulanga na Kambi ya Mkaa naomba wawekezaji wahamasishwe kupeleka huduma hii. Vile vile mnara upo Itigi bali mawasiliano hayafiki vijiji vya Gurungu, Idodyandole, Ipande na Kashanga. Ninayo matumaini makubwa kuwa ataona umuhimu wa kupeleka mawasilinao kwani maombi ya Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa John Lwanji yako offisini kwako tukishirikiana na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudzi za Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu bado kuna tatizo la mawasilianokatika Tarafa ya Ihanja vijiji vya Muhintiri, Mnyange, Igilansoni na Kinyampembe. Vile vile Tarafa ya Sepuka vijiji vya Ighombwe, Msosa, Mgungira, Iyumbu na Mlandala wakati vijiji hivi uchumi wao uko juu kuitia ufugaji na kilimo cha alizeti na pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kuwa nitashukuru Waziri Mheshimiwa Profesa Peter Msolla akitambua juhudzi zetu na kutupa matumaini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano katika Wilaya ya Iramba, juhudzi za Wabunge wa Majimbo Mheshimiwa Mgana Msindai kwa Jimbo la Iramba Mashariki na Mheshimiwa Juma Killimbah nikishirikiana naye kuitia maswali na kuchangia Bajeti bado hatujafaulu kupata mawasiliano ya simu kupita simu za mkononi maeneo ya Kata ya Ntwike, Iramba ya Magharibi na Kata au vijiji vya Nkungi, Nkalakala na Mwangeza bado hakuna mawasiliano. Tunaomba Waziri atambue juhudzi zetu ili wapigakura wetu wasikie na tupate lugha yenye matumaini kwani wananchi wanauwezo wa kutumia kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kurudia tena kuwa naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

MHE. DR. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hoja ya Wizara yake pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na watumishi wote wa Wizara kwa utendaji kazi mzuri uliowezesha mafanikio makubwa katika sekta, pamoja na kulaza mkongo wa mawasiliano wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ya Wizara katika Jimbo la Bagamoyo, bado tuna changamoto kubwa ya mawasiliano ya mtandao wa simu za kiganjani. Mtandao wa *Zain* haapatikani katika maeneo mengi hasa katika Kata ya Kiromo (vijiji vya Kitopeni, Kiromo, Buma na Maraya). Pia katika Kata ya Yombo katika vijiji vya Yombo, Chasimba na Kongo na katika Kata ya Magomeni (Magomeni na Kitame). Tunaiomba Wizara ihamasishe makampuni ya simu yapanue mtandao wao wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujio wa mkongo wa mawasiliano lazima ulete maboresho ya mawasiliano na kupunguza gharama za mawasiliano. Wizara ifatilie kwa karibu gharama za simu zinazowekwa na makampuni ya simu ili faida za mkongo kigharama zimfikie mtumiaji huduma. Naunga mkono hoja.

MHE. ANNE S. MAKINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Wataalam wake katika kuongoza Wizara hii. Mafanikio makubwa yanaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tatizo dogo sana la mawasilinao kwenye Kata ya Lwungilo yenye vijiji vya Uliwa, Ngalanga, Lwungilo, Ulengule na Kata ya Matola, Vijiji vya Boimanda, Mamongolo na Kitulila na Kata ya Yakobi, Kijiji cha Yakobi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutashukuru kama utaalam utapatikana kuona sehemu hizo zina matatizo gani. Pia kama jibu litapatikana itakuwa faraja kubwa kwa wakazi wa maeneo hayo. Wao ni Wakulima wanaojishughulisha sana na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja. Naomba ufanuzi wa ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu ya maswali yangu hapa Bungeni kwamba angesaidia kufutilia *Commitments za Zain, Tigo, na Vodacom* kujenga Minara katika Kata za Malibwi, Mlola na Makanya, Wilaya ya Lushoto. Je, wakazi wa Kata hizo tatu watarajie kuunganishwa na mitandao hiyo lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia heri Wizara na naunga mkono hoja.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mungu kwa uzima. Pia naomba nimshukuru Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana. Sayansi na Teknolojia imejitahidi kwa uwezo wote na kuonyesha kuwa hawakukosea katika uteuzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) naipongeza kwa kupata tuzo ya Kimataifa kama taasisi bora zaidi ya usimamizi wa masuala ya mawasiliano Barani Afrika kwa mwaka 2009. Pamoja na kazi nzuri naiomba mamlaka

kuongeza muda wa kusajili simu zao kwa kuzingatia hali ya mawasiliano na ukubwa wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba minara katika maeneo ya Wilaya ya Nkasi katika Kata ya Ninde pamoja na Kata ya Wapembe. Kata hizo ziko kwenye Ziwa la Tanganyika, mawasiliano ni magumu sana, tunaomba juhudzi za Serikali kwani wananchi wako katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MANJU S. MSAMBYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za Posta, kuna haja ya Shirika kujipanua hadi vijijini kwa kuwa na mawakala wa kupokea, kusambaza na kusafirisha barua na vifurushi. Ni dhahiri uchumi wa Shirika hauruhusu kufungua ofisi maeneo mengi, lakini mawakala ni muhimu kwa sababu bado huduma za barua ni muhimu vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TTCL*, naiomba Wizara ilieleze Bunge hili ni kwa nini hadi sasa nafasi ya Afisa Mtendaji Mkuu haijajazwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu simu za mikononi. Gharama za simu za mikononi zinatia wasiwasi, unakuwepo ujanja wa promosheni na kuwaduwaza watumiaji eti lipo punguzo kuititia promosheni hizo, kwa nini mtandao wa *ZAIN* kila mara unabadi umiliki? Huu sio ujanja wa kukwepa kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilio cha kutokuwepo simu za mikononi Jimboni kwangu, eneo la Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Naomba Wizara itoe maelekezo kwa makampuni ya simu ili yawekeze huduma zao Jimbo la Kigoma Kusini, Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Eneo hili ambalo linahusisha Kata za Sunuka, Sigunga, Igalula, Buhingwa na Kaliwa ni maeneo ya wakulima na wavuvi ambao, wangependa kuwasiliana na maeneo mengine katika Mkoa wa Kigoma na Tanzania kwa ujumla kupanga na kufahamu bei ya mazao yao, wangependa kutumia mawasiliano kiulinzi hasa ukitilia maanani wavuvi wa mwambao wa Ziwa ni waathirika wa uvamizi wa maharamia toka nchi jirani ya DRC, kupora zana za uvuvi za wavuvi hawa duni. Mawasiliano ya kawaida baina ya wakazi wa maeneo tajwa na mengineo nchini na duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara inipe jibu kwa nini kampuni ya *Zain* imeweka mnara wa simu Kijiji cha Igalula lakini sasa tunafikia mwaka wa tatu mtambo huo haujazinduliwa, mnara umekaa pambo. Bahati mbaya zaidi watu wa eneo husika waliwapokea watumishi wa kampuni ya *Zain* kwa bashasha wakati walipopeleka vifaa vya mnara huo. Wanakijiji kwa kutambua umuhimu wa huduma ya simu waliwafanya takrima. Bahati mbaya ni kwamba kampuni imekuwa kama imepotea njia, naomba Wizara inipe majibu ni vipi wanawafikiria wakazi wa maeneo kuhusu mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje mnara unajengwa eneo fulani (Igalula) lakini hauwekwi katika matumizi na wala Serikali haipati maelezo toka kwa kampuni husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iwe inaomba taarifa ya utekelezaji na wapi minara imejengwa na ipi inafanya kazi.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa kazi nzuri na uwasilishaji wa hotuba ya bajeti, nawapongeza watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano na kufanikisha uendeshaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Posta, Serikali haijafanya chochote kuhusu ahadi zake kuhusu mtaji na kuliondoa Shirika katika mpango wa kubinafsisha, Serikali itekeleze ahadi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawasiliano ya simu katika Wilaya mpya ya Kalambo, mara nyingi nimeandika barua nikiomba makampuni ya *Zain*, *Celtel* na mengine wajenge na kusambaza mawasiliano katika Kata za Mambwe Kemya, Legezamwendo na Kalembe. Ipo Kata mpya ya Mnamba nayo inahitaji mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ijitahidi kufanya majadiliano na Makampuni ya Simu za Mkononi ili gharama ya muda wa maongezi ipunguzwe ili wananchi wapate huduma hii kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za utafiti nchini ziongezwe ili utafiti unaofanywa na wataalam wetu usikwame kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Utafiti wa kisayansi uunganishwe na uzalishaji ili iwe rahisi kuhuisha ubunifu na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa mawasiliano nao utiliwe mkazo ili usambazwe katika Mikoa na Wilaya zetu zote ili kuharakisha mawasiliano ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wote Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote katika Wizara hii na mashirika yaliyo chini yake kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanikisha katika nchi yetu. Aidha, hotuba yao ni nzuri inatia moyo. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kufikia uamuzi wa wateja wa simu za viganjani wasajili simu zao jambo ambalo litapunguza kama si kuondoa kabisa tabia mbaya na ya kihuni iliyokuwa imeanza kujeneka katika nchi yetu. Ombi

langu kuhusiana na jambo hili ni kupatiwa ufanuzi kinachosajiliwa hasa ni kipi *line au handset*. Iwapo mtu ataibiwa simu yake je, usajili wa simu huu utasaidiaje katika kuifutilia, kuzuia mwizi huyo asinufaikie na simu hiyo? Je, usajili huu utamzuiaje mwizi huyo kusaili simu hiyo, je, usajili huu utamzuiaje mwizi huyo kusaili simu aliyoiba kama simu yake? Je mitandao yote imeunganishwa ili kufutilia wizi wa simu na matumizi mabaya ya simu zinazoibowi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kuboresha mawasiliano ya njia ya simu za viganjani na za mezani (*TTCL*) katika jimbo langu hali illiyokuwa tofauti sana miaka mitano iliyopita hvi sasa ngudu katika jimbo langu kuna minara ya *TTCL*, *VODACOM*, *TIGO*, na *ZAIN*. Hungumalwa kuna minara ya *Vodacom*, *Zain* na *Tigo*, naishukuru sana Serikali na Makampuni hayo na Mheshimiwa Maua Daftari kwa juhudhi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masikitiko na maombi, Jimbo langu la Kwimba lina Tarafa tatu, Ngudu, Nyamilama na Mwamashimba, mawasiliano mazuri niliyoyasema hapo juu ni katika Tarafa mbili (Ngudu na Nyamilama), Tarafa ya Mwamashimba haina mnara hata mmoja na mawasiliano ni duni sana na sehemu zingine hazina kabisa maombi ya mara kwa mara, yamekuwa yakiwasilishwa Serikalini kuiomba iwasilishe maombi hayo kwa makampuni husika, juhudhi zote hizi kwa miaka sasa hazijapata majibu kwa kilio cha wananchi wa Kata zote tano za Tarafa ya Mwamashimba, hakijasikilizwa na makampuni ya simu haya.

Shukurani za pekee tunazipeleka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Maua Daftari kwa uvumilivu wake wa kuendelea kuyapokea maombi hayo na wakati mwingine yeye binafsi kuandika barua kwa makampuni hayo, cha kusikitisha baadhi ya makampuni hata kumjibu Naibu Waziri huyo hayakumjibu, tunamwomba radhi kwa kufedheheshwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na swalii, ni mambo gani hasa yanayosababisha iwe vigumu kufikisha mawasiliano hayo katika Tarafa hiyo? Je, ni sababu za kiuchumi, kiteknolojia au kijamii? Wananchi wangefurahi kujulishwa sababu, sababishi ili hata baada ya kusubiri kwa miaka mingi na juhudhi za kuomba huduma hizo kushindwa wajue kama kwa muda gani tena watasubiri kuboreshewa mifumo ya mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wanachoomba ili mradi waone kama itakuwa vigumu sana kujenga minara mipya katika maeneo hayo, wanaiomba sana Serikali iyasihi makampuni waweze kongeza juhudhi ya kuongeza nguvu ya minara iliyopo Hungumalwa ili nguvu ya mitandao hiyo iweze kwenda mbali zaidi. Nguvu ya minara iliyopo Hungumalwa, Mipa (Shinyanga) na iliyopo katika eneo la Kusini mwa Jimbo la Solwa na maeneo ya Kusini mwa Jimbo la Misungwi naamini kuwa itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana maombi haya yazingatiwe. Naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakupongeza kwa hotuba yako nzuri yenyе ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.
Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni minara ya simu. Jimbo la Mpwapwa linahitaji Mawasiliano ya simu za mkononi na kwa kuwa Minara iliyojengwa ni michache. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu katika Kata za Matomondo, Kimagai, Godegode, Mkanana, Berege na Mima ili kuboresha Mawasiliano ya simu Wilayani Mpwapwa?

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama za simu hizo ili wananchi wengi waweze kununua simu hizo na kuzitumia?

Je, Kampuni ya simu ya *TTCL* wana mpango gani wa kupeleka huduma hii vijiji na kwa gharama nafuu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, naanza kwa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii. Yako maendeleo yanayoonekana katika eneo hili hivyo wanafanya kazi njema.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu katika yafuatayo:-

- (1) Tuwe na Vijana wetu watakaofutilia maendeleo ya *science* na technolojia katika nchi mbalimbali ili kubaini maendeleo yanayofanywa na hivyo kushauri hatua za kuchukua hapa nchini.
- (2) Ushirikiano wa *Science* na Technolojia katika ngazi ya Vyuo vikuu yaimarishwe zaidi hasa katika nchi za Asia kama Korea, Japan, China na India.
- (3) Wizara ifanye na ipate taarifa za athari za technolojia mbalimbali kwa wananchi na kuwapa/kuwashauri wananchi ipasavyo.
- (4) Kuhusu Mbwiga.
 - (a) Zipo Kata hazina Mawasiliano ya simu kabisa kama Kata ya Ukata naomba, *Vodacom*, *Zain*, *Tigo* washauriwe kupeleka mitambo yao huko.
 - (b) Kata zilizobaki zina mawasilino ya simu lakini vijiji vyake havina mawasiliano kama vijiji vyote Kata ya Mpepai kama Kihungu, Rwuma Chini, Lahangai Kata ya Ngine pia vijiji vya Njombe na kadhalika.
 - (c) Wapo Vijana wabunifu wote Mbwiga, katika nyanja ya ufundii mbalimbali. Hawa wametambuliwaje na wasaidiweje. Yupo mmoja ame *assemble tractor* ndogo anaitwa Mkukute.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, Nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kufanya ukarabati mkubwa jengo la Posta la Mpwapwa. Je, kuna nini hadi sasa jengo hilo halijafanyiwa ukarabati?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Prof. Peter Msola, Mbunge na Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia - mwenye dhamana, nimpongeze pia Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mbunge na Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mkongo wa Taifa wa Mawasilinao tumeona utandazaji wa nyaya ardhini karibu maeneo mengi nchini eneo kubwa ni lile la barabara ya kat. Naomba Waziri atoe maelezo ya namna ipi maeneo yaliyopitiwa na mkongo huu yatafaidika na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, simu za viganjani – nashukuru mtando wa Makampuni mbali mbali yanayotoa huduma kwa wananchi kwa mawasiliano, nashukuru Kampuni za *Zain*, *Tigo*, *Vodacom* na *Zantel* na *TTCL* kuwepo maeneo mbalimbali Jimboni Iramba Magharibi. Nasikitika kwamba eneo la Kata ya Ntwike hakuna mnara wowote wa kutoa huduma na wala hakuna mawasilinao, pamoja na juhud zangu za kuwasiliana mara kwa mara na Makampuni yanayotoa huduma, bado juhud zangu hazijaza matunda. Naomba Waziri na Wizara ione umuhimu wa kuhimiza Makampuni ya simu za mkononi kuwekeza katika Kata ya Ntwike ili wananchi wapate mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Ving'amuvi (*Star time*). Napongeza uvumbuzi wa Teknolojia mpya ya ving'amuvi vya mawasiliano vya Star times, chini ya *TBC* pamoja na Teknolojia hii ambayo ina unafuu wa bei na rahisi lakini maelezo yanayotolewa na wasambazaji *Star times* ni ya jumla mno na mara nyingi yanasaababisha usumbufu kwa wateja, naomba Wizara kuwashauri wasambazaji kutoa maelezo ya kutosha ili kuondoa usumbufu kwa wateja. Kadhalika Teknolojia isambae kwa mikoa yote na isiwe kwa maeneo maalum.

Mheshimiwa Spika, utoaji leseni ya masafa (*Radio & TV*) naulizia juu ya Radio ya Halmashauri ya Iramba *RIKI FM* leseni yake itatolewa lini na vikwazo gani vinavyozuia utoaji wa leseni hii.

Mheshimiwa Spika, usajili wa simu, utaratibu ni mzuri hasa kwa sababu za kiusalama na utambuzi wa masuala mbalimbali na itasaidia kudhibiti matumizi mabaya ya simu. Tatizo lililopo ni hatua ya sasa juu ya utambuzi kuhusu usajili inawezekana simu nyingi zikafungiwa kimakosa kutokana na uzembe wa mawakala wa usajili kuzembea kuwasilisha taarifa za usajili kwa mamlaka (*TCRA*).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa jinsi wanavyotoa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza ilani ya Uchaguzi 2005 – 2010.

Mheshimiwa Spika, pamoja nao nawapongeza sana Watendaji wa Wizara, Katibu Mkuu, Wakuu wa Mashirika ndani ya Wizara hii ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa pamoja na Mashirika hayo kujishughulisha na masuala ya Mashirika yao pia wamechangia sana maendeleo ya Jamii kwa kuchangia miradi mbali mbali. Hoja ya msingi ni upatikanaji wa mawasiliano katika maeneo muhimu.

Mheshimiwa Spika, bado kuna kilio cha mawasiliano mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, eneo la Mkunda Muhukuru Wananchi wanaomba sana huduma hiyo, ili pia kuboresha ulinzi eneo hilo la mpakani.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni eneo la Mgazini nalo halina mawasiliano na umuhimu wa eneo hilo ni mkubwa kwani ndiyo ukanda maalum wa uzalishaji wa Chakula.

Mheshimiwa Spika, eneo la Vitalu vya Wawindaji la Iringa ni eneo muhimu sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Dr. Maua Daftari alionyesha moyo wa dhati wa kutembelea maeneo hayo, basi wananchi wanasubiri kauli ya Serikali yenye matumaini kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalize kwa kuwatakitia kila lenye kheri katika kutekeleza majukumu ya Wizara, cha muhimu tutumie sana kila mwanya unaopatikana kuona dhana ya Sayansi na Teknolojia inatumika kuleta maendeleo yakinifu katika nchi yetu, katika eneo la Sayansi, Teknolojia mbali mbali na kadhalika.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, hongera nydingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Makampuni ya simu yahakikishe simu zinasikika nchini kote, kuliko ilivyo sasa kwamba pakiwa na bonde simu inakatika na kupatikana maeneo kadhaa tu na hasa maeneo yenye mwinuko.

Mheshimiwa Spika, nawatakitia kazi njema.

MHE. DR. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia pamoja na Naibu Waziri wake, kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na ya hotuba nzuri. Aidha nawapongeza Watendaji wake wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kutayarisha hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu ni machache tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii itoe msukumo wa pekee kwa Kampuni za simu za mkononi ili wajenge minara ya mawasiliano katika maeneo yafuatayo:-

- Eneo la Kiloka. Hakuna mawasilinao kabisa.
- Eneo la Mkulabi – Tarafa ya Ngerengere ambako mtandao ni hafifu sana na hayo maeneo yote.
- Eneo la Kata ya Tagetero katika Wilaya ya Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yametengwa sana Kimawasiliano.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kama inawezekana muda wa usajili wa simu uongezwe kwa sababu maeneo mengi na hasa maeneo ya vijijini hawana habari na zoezi hili. Tafadhalni mawakala waende vijijini kuwapa wananchi taarifa pamoja na huduma za usajili.

Mheshimiwa Spika, nawatakia utekelezaji mzuri wa Bajeti ya 2010/2011 na Mungu awabariki kwa kuongeza muda wa usajili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia - Mheshimiwa Dr. Maua Daftari. Karibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uzima na afya njema na leo hii niko hapa kuchangia hoja ya Wizara yangu ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Kwa udhati kabisa namshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wangu kwa kunihamini na kunipa nafasi ya kumsaidia. Mola amlinde na azidishe kheri zake. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuniongoza vyema katika shughuli zangu hizi. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mola alinipa bahati kufanya kazi na Mawaziri saba. Mheshimiwa Kusila, Marehemu Mheshimiwa Nyanda, Mheshimiwa Prof. Mwandomsy, Mheshimiwa Mramba, Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Prof. Msolla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio mkamilifu, inawezekana nikawa pengine sikuwatendea mazuri. Naomba wanisamehe ila naomba niwashukuru sana ndani ya sakafu wa moyo wangu kwa kukubali kwao kuniruhusu nichote hazina ya busara zao ambazo zimenisaidia sana kuboresha kazi zangu. Kwa kipekee namshukuru Mheshimiwa Prof. Msolla - Waziri wangu na Katibu wangu Mkuu, Bwana Turuka kwa ushirikiano mzuri nilioupata kutoka kwao. Naamini ninapofanya kazi kwa kuamiana, kwa kusaidiana, kwa kushirikiana, kwa kutaarifiana, hakuna lisilowekana kutekelezeka, kwani sote tuko kutumikia wananchi wa Tanzania. Nasema ahsanteni sana Waheshimiwa Mawaziri wangu.

Pongezi kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wote kwa kazi nzuri mnazozifanya.

Lakini pongezi za pekee kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa *support* yote waliokuwa wananiwa wakati wote. Daima nilikuwa nawatumikia kwa yale yote ambayo waliona ni shida na kero za wananchi wao. Nasema Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana. Mwenyezi Mungu awajaze kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie machache kwa sababu ya muda. Nitachangia Sekta ya Mawasiliano na maeneo mengine. Ni jambo lisilofichika hata kidogo kuona hatua tuliyofikia katika Sekta hii, tumesahau sasa simu za kukoroga, sasa mawasiliano yameboreka sana. Hatushangai kuona bibi zetu vijijini nao sasa wanaona umuhimu wa kuwasiliana kwa kutumia simu za mikononi.

Wengi tunapotatembelea na wanapotembelea na wajukuu zao na kuulizwa wapelekewe zawadi gani, basi huomba simu ya mikononi. Nadhani sijasema uongo. Sasa ukimwuliza wewe bibi hiyo simu ni ya nini? Jibu ni kwamba mjukuu wangu napenda nami niwe nakujulia hali na kukeleza yanayoendelea huku nyumbani. Hayo nasema kwangu ni mafanikio. Sasa tuna uwepesi wa kuwasiliana hata tukiwa chooni, hayo ni maendeleo ya upashanaji habari.

Changamoto ambazo tunaendelea nazo ni kusisitiza makampuni husika yaendelee kusambaza mitandao yao mijini na vijijini ili wawarahisishie wananchi katika maisha yao wakulima wapate taarifa za bei na wafanyabiashara wafanye biashara zao na hali ya hewa itolewe, wananchi waweze kulima kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii. Niseme kidogo tu kwenye masuala ya mkongo wa Taifa na nitarudia, sekta ya mawasiliano, kwa sababu yote ni mawasiliano. Uniruhusu niandike, Mwenyekiti, kwani usipoandika hufutika.

Katika juhudi zangu za hapa na pale za kutaka kuboresha mawasiliano nikiwa kwenye mkutano mmoja wa mawasiliano wa kule Geneva, nilipata nafasi ya kuongea na kampuni inayoitwa *itv Worldtell* na *CICTCC* ya China kuomba kuona uwezekano wa kutusaidia Watanzania tuweze kujenga mkongo. Kwa pamoja walikubali kugharamia *feasibility study* kwa kufanya *study* hiyo. Kweli walifika Tanzania baada ya mawasiliano. Waliomba wapatiwe malazi na gari tu na wao wafanye kazi hiyo na kweli *study* hiyo ilifanyika na ndiyo iliyotupa nafasi ya kuanza harakati ya kutafuta fedha za ujenzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mwanzilishi wa mkongo huu wetu ni mimi. Naandika historia tu iwekwe katika daftari ambalo ni jina la babu yangu. Juhudi kubwa zinafanyika za ujenzi na sasa tumemaliza *phase one*, tuko *phase two* na pia tumefikisha mkongo wa mawasiliano mpakani mwa nchi jirani mwetu Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya. Zambia tuko njiani. Aidha, mradi huu ukikamilika utaifanya Tanzania kuchukua nafasi ya kuwa kitovu cha mawasiliano.

Ombi kubwa kwa Watendaji wenzangu ni kuharakisha kuunganisha na kujenga mkongo Zanzibar. Kwa sababu ndiyo ninakotaka na sadaka huanza nyumbani. Hasa kwa vile njia ya mawasiliano kupitia baharini, Pemba tayari imekamilika baada ya kuboresha

umeme. Changamoto kubwa mbele yetu ni kuunganisha mawasiliano ya mkongo kuwafikia walengwa vijiji walipo na kutumia nafasi zinayopatikana na matumizi ya *ICT* ili wengi wafaidike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamechangia juu ya mawasiliano, nao ni Mheshimiwa Margareth S. Sitta, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ndugai - wewe Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Manju S.O. Msambya, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia - Mwalimu wangu, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi - Mwalimu wangu, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Lodovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri. Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Martha M. Mlata na Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubwa wenzangu hawa waliyoyazungumzia yako katika maeneo kama manne. Kwanza usikivu siyo mzuri, inakatikakatika, wengine walitaka waongezewe minara, kuna maeneo ambayo hayajafikiwa. Wengine wanasema lazima wapande juu ya vichuguu au miti ndiyo wapate mawasiliano na mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba nilipata nafasi ya kutembea maeneo mengi tu katika nchi hii. Lengo kubwa ni kuwatoa wenzangu ambao wako juu ya meza kule Mikoani kuona kwamba makampuni ya simu huku ndiko kuliko na pesa na ndiyo nilikokwenda kuwaonyesha kwamba huko vijiji ndiyo pesa ziko. Kwa hiyo, wao waweke mawasiliano katika maeneo hayo. Kwa hiyo, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wale ambao hawakufikiwa kwa mara hii, Wizara bado itakuwepo na maeneo tulioandika bado yapo.

Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote ambao wana matatizo ya mawasiliano kwamba shughuli hizi za mawasiliano zitawafikia katika maeneo yao. Nawaomba subira tu, na namwomba sana Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Mheshimiwa Tatu Ntimizi wala sina lolote ndani ya moyo wangu, isipokuwa tu labda hajawahi kuniomba kwenda kwake. Lakini angaliniomba ningelikwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimwambie tu Mheshimiwa kwamba hatujasahau maeneo yake na tutawapa uzito unaofaa. Pili, naomba nichangie juu ya masuala ya *TCRA*. Kwa sababu ya wakati, mimi nisingependa kusema mengi sana. Niliona niya-*group* haya majibu yangu mbio mbio tu ili niweze kutoa maelezo machache. Yamezungumzwa mengi yanayohusu *regulations*. Kuna wengine waliozungumza kwamba huduma za *TV* na redio hazisikiki vizuri. Mheshimiwa Mramba alisema hivyo na Mheshimiwa Killimbah naye alitaka kujua kuna kikwazo gani kinachochewesha utoaji wa leseni ya redio na *TV*, Halmashauri ya Iramba. Tunasema Wizara tumeshalipokea hilo wala sidhani tena kuna tatizo.

Lakini alipongeza zoezi la usajili wa simu na kutoa angalizo kuwa baadhi ya wananchi wanaweza kuathirika kwa namna moja au nyingine kutokana na uzembe wa baadhi ya mawakala. Lakini tuseme leo tumetoa tena siku 14 kuanzia leo. Kwa hiyo, ni nafasi ya kutosha. Niombe makampuni kama wamefanya kukoroga koroga huko katika usajili waweke sawa, baada ya siku 14 tunarudia pale pale. Ni siku 14 tu tumeongeza, kwa sababu wengine wamekwenda kutazama majina yao hawakuyaona, wengine wameandikwa majina siyo! Kwa hiyo, tumetoa hizi siku 14 *at least* makampuni ya simu kujiweka sawa shughuli hizi ziende vizuri. Lakini suala la kusajili simu ni muhimu na haturudi nyuma katika hilo.

Mheshimiwa Anna Lupembe, ye ye alisema kutokana na wananchi wengi kutoweza kusajili kwa wakati na sababu mbalimbali, anashauri Wizara kushauriana na mamlaka watoe muda. Nasema muda tumetoa na leo Mheshimiwa Waziri amesema hapa. Kwa hilo, limepewa uzito wake. Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya ye ye anazungumzia ni lini yatapatikana mawasiliano ya simu katika maeneo ya Kiloka? Kama nilivyowajibu Waheshimiwa wenzangu kwamba hilo tutalishughulikia ipasavyo. Hata kama sisi hatupo, lakini tutawaandikia na watakaokuwepo watafanya *follow-up* kuanzia hapo tulipoacha sisi.

Kwanza niseme, jamani wote waliosimama walitushukuru sana kwa kazi nzuri tunazozifanya. Sisi tunasema ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge mmetupa nafasi ya kuwatumikieni na sisi tumewatumikia. Hii yote ni katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika sekta ya mawasiliano imetekelezwa, labda kwa asilimia 98.9. Ni asilimia ndogo sana iliyobakia ambayo nina hakika kwa muda huu uliobakia tunaweza tukafanya mambo mazito sana.

Mheshimiwa Killimbah, alishauri vile vile kuweko na mkakati mzuri kukabiliana na matumizi mabaya ya simu. Lakini nadhani Mheshimiwa Killimbah atakubaliana nami kwamba akiangalia ile Sheria ya Epoka inachukua mambo mengi sana na hayo matumizi mabaya ya simu ndiyo tuliyokuwa tunalenga. Ndiyo maana tukatengeneza Sheria ile na tukimaliza hizo siku 14, kwa sababu imeshapitishwa, imeshachapishwa na itaanza kufanya kazi yake.

Niwaombe tu Waheshimiwa wawasihi sana wenzetu huko vijijini, kuna wengine wanapenda sana mambo ya kutukanatukana kwenye simu. Hayo mambo wengine yanaweza yakawafikisha pabaya kwa sababu Sheria ikianza kazi ni kwa watu wote ambao hawafuati taratibu zinazotakiwa, lazima na wao washughulikiwe.

Mheshimiwa Anna Abdallah anasema: Je, kwa nini kuna haja ya kuhakiki na usajili? Tunasema kwamba Sheria mpya ya Mawasiliano ya Posta ya *electronic* ambayo imezingatia mapendekezo hayo. Pia namjibu Mheshimiwa Sakaya kwamba sheria hiyo ilishapitishwa Bungeni na kuridhiwa na sasa imeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 18

Juni, nakuombeni sana Waheshimiwa Wabunge tuwasih hawa wenzetu kama nilivyosema hapo awali wazingatie matakwa ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Sakila alitaka apewe ufanuzi juu ya zoezi la usajili. Nimeshalizungumza. Je, mitandao yote imeunganishwa ili kufuatilia wizi wa simu na matumizi mabaya? Nawaambia ni kweli tumefanya hivyo.

Kumekuwa na kilio cha muda mrefu wa kampuni ya simu kufikisha mawasiliano katika Tarafa walizozitaja za Mwacha. Kama nilivyosema kiujumla kwamba tutalishughulikia na mimi nilishawahi kumwandikia Mheshimiwa Sakila kumwambia kwamba nime-note maeneo mengine ambayo hayajafikiwa. Yeye pamoja na Mheshimiwa Ligallama kwamba tutalishughulikia masuala yao.

Mheshimiwa Msambya, yeye anasema gherama za simu zinatia wasiwasi kwa kuwalaghai wananchi kwa kuwa kuna pungozo kupitia promosheni. Lingine, anasema inakuwaje minara inajengwa eneo fulani kwa mfano, Igalula, lakini haiwekwi katika matumizi na wala Serikali haipati maelezo kutoka kwa Kampuni husika.

Sisi tuseme tu kwamba tutawasiliana na kampuni ya simu husika ili kuona uwezekano wa kufikisha huduma hizo kwenye Tarafa kwa kubaini sababu zilizokwamisha kwa sasa, kwanini? Minara ya kampuni haitumiki, kwani kampuni haiwezi kujenga mnara bila kuwa na sababu. Kujenga mnara mmoja ni zaidi ya dola laki tatu. Kwa hiyo, wana sababu za kiufundi, sababu za kimsingi. Sisi tutaendelea kuwasihii kuwaambia tu kwamba kule ambako mmeweka mali zile ni vizuri basi mzishughulikie.

Mheshimiwa Hemed Mohamed, yeye alitaka kama alivyofikiria mwanzo kwamba tarehe 30 ni siku ya mwisho kusajili simu. Sasa nadhani alitaka tuongeze muda na suala hili tumeshasema tunaliongezea mpaka tarehe 15. Kwa hiyo, hilo tumelizungumza vizuri. Mheshimiwa Mwananzila, Mheshimiwa Mramba, Mheshimiwa hasa Mramba anasema Wilaya ya Rombo bado haina usikivu wa *Radio Tanzania*.

Sisi tunasema kisheria Mamlaka ya Mawasiliano haina nguvu ya kuwalazimisha wamiliki wa vyombo vya utangazaji, na kuwalazimisha wamiliki wa vyombo vya utangazaji, kulipa mrahaba. Kuhusu wasanii katika utaratibu wa utoaji wa leseni, jukumu la kazi ya usanii na mrahaba zinashughulikiwa na mamlaka nyingine na hili suala la redio na usikivu, tutawaaambia wanaohusika, Wizara ya Habari na Utangazaji washirikiane na *TCRA* kuona wanatatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Sakila anasema upo mtindo wa baadhi ya watu kuwarubuni baadhi ya makampuni ya simu za mkononi waingilie mawasiliano. Sisi tunasema hiki ni kitu ambacho hakikubaliki na Sheria itachukua mkondo wake. Wenye dhamana ya kutoa habari hizo ni lazima wapate kibali kunakohusika.

Kuhusu masuala ya Taasisi na Vyuo, Taasisi ya *DIT* na *TAEC* yamezungumziwa sana. Wanataka wakati Taifa linaendelea katika mkakati wa kuvuna madini ya kemikali, Wizara hizi mbili, Wizara yangu na Wizara ya Nishati na Madini washirikiane kuandaa wataalam watakaowezesha kuainisha matumizi bora ya madini hayo ya kemikali.

Nasema shughuli hizi za ushirikiano tumeanza mapema na Tume ya Nguvu ya *Atomic* ilishaendesha mafunzo ya pamoja kati ya wataalam wa Wizara hizi mbili juu ya uchimbaji salama wa madini ya *uranium*. Lakini niwaambie tu hivi, sasa jamani *uranium* haijaanza kuchimbwa, walioko huko wanafanya utafiti tu. Kwa hiyo, wala msiwe na wasiwasi, ni utafiti tu kwa sababu uchimbaji wa *uranium* unahitaji zana kubwa tu. Nina hakika wachimbaji wadogo wadogo sio rahisi sana kuweza kufanya kazi kama hiyo.

Walitaka tushughulikie juu ya kujenga uwezo wa uchambuzi wa mikataba. Tunasema hili tumelichukua, na pia kulikuwa na suala la kuna ongezeko kubwa la matumizi ya vifaa vyta mionzi hapa nchini, mfano, simu za mikoni, *X-Ray machine* na wanaomba Serikali iongezee nguvu ili Tume iweze kutathmini mifumo hii kwa kutoa ushauri.

Serikali inatambua vyema ongezeko la matumizi ya vyanzo vyta mionzi na napenda niwahakikishie wananchi kwamba tunapima mionzi ya *X-Ray* katika hospitali zote za Bara na Visiwani na hata Visiwani wanajua hivyo hivyo na wanapewa ma-*batch* watu wa *X-Ray* na zinapimwa zile *batch* mionzi ni kiasi gani ambayo inatumika. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba tunachukua tahadhari za kutosha.

Juu ya Mkongo wa Taifa, nimezungumza vyta mionzi na napenda niwahakikishie wananchi kwamba tunapima mionzi ya *X-Ray* katika hospitali zote za Bara na Visiwani na hata Visiwani wanajua hivyo hivyo na wanapewa ma-*batch* watu wa *X-Ray* na zinapimwa zile *batch* mionzi ni kiasi gani ambayo inatumika. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba tunachukua tahadhari za kutosha.

Nasema, mpango wa kufikisha mkongo wa Taifa Mkoani na Wilayani, Mkoa wa Mtwara upo. Kazi hii inafanyika kama nilivyosema awali kwa awamu mbili au tatu za mradi.

Mradi umeshaanza kutekelezwa na fedha kwa ajili ya kazi hii zimetengwa katika mwaka 2010/2011. Mkongo wa Taifa utaanzia Dar es Salaam, Mkuranga, Somanga, Lindi, Mtwara, Tandahimba, Masasi, Tunduru, Namtumbo, Songea, Njombe na Makambako.

Aidha, maeneo mengine ni yale yaliyomo katika njia ya kuanzia Biharamulo, Kibondo, Kasulu, Kigoma, Urambo, Tabora, Mpanda, Sumbawanga, Tunduma na Unguja na Pemba. Kwa hiyo, mkongo utafikia maeneo yote. Tunafikisha maeneo ya Mikoa baadaye tutafikisha maeneo ya Wilaya na hatimaye wanaofika *last mile connection* wata-connect katika vijiji.

Kuhusu kuunganisha vituo vya Tarakea na Holili na Mkongo wa Taifa wa mawasiliano ili kuunganisha na Jamhuri ya Kenya na kuunganisha mkongo miji ya Loitokitoki na Taveta. Haya yalizungumzwa na Mheshimiwa Mramba. Niseme tumeyasikia, Wizara inaendelea na utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, dakika 15 huwezi kusoma yote ukamaliza. Lakini nikiri tu kusema kwamba Wizara hii imefanya mengi sana na yote sio ya kujificha, yanaonekana.

Waheshimiwa, kwa heshima na taadhima tunawaombeni mtupe pesa hizo ili tufanye hizo kazi zilizobakia ambazo bado hazijafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Naibu Waziri, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Sasa naomba kumwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Profesa Peter Msolla, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Karibu. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa mara nyingine tena kwa kuniwezesha kusimama mbele yenu na kutoa mchango wangu katika hoja hii. (*Makofî*)

Aidha, kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kilolo, kwa imani kubwa waliyonayo kwangu. Ninawashukuru kwa njia ya kipekee kwa ushirikiano waliouonesha katika ujenzi wa zahanati, shule za sekondari, chini ya uongozi imara wa Halmashauri ya Wilaya na hatimaye kudahili 100% ya wanafunzi waliofaulu darasa la saba na hatimaye kuijunga na kidato cha kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na Wenyejiti wengine wa Bunge kwa umahiri mkubwa mnaouonesha katika kuliendesha Bunge letu. Pia nichukue nafasi hii, kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa umakini wake wa kusimamia Shughuli za Serikali hapa Bungeni. (*Makofî*)

Aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyoasilisha hapa Bungeni leo asubuhi, tarehe hii 30 Juni, 2010 kwa michango yao mizuri na ya kina. Kumetolewa changamoto nyingi na hii ni dalili ya dhati ya mwamko mkubwa kwa upande wa kuendeleza maeneo ya mawasiliano, sayansi, teknolojia na ubunifu. Aidha, katika michango hiyo imedhihirika wazi juu ya mahitaji makubwa ya mawasiliano ya simu, kama ilivyo huduma za usafiri wa reli, barabara na bandari kuwa ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za kiuchumi za mawasiliano katika mwaka wa 2009, zilikua kwa kiwango cha juu zaidi ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi. Kiwango cha ukuaji cha shughuli hizi ilikuwa ni 21.9% mwaka 2009 ikilinganishwa na 20.5% mwaka 2008. Ukuaji huu ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya mawasiliano, kuongezeka kwa wateja wa simu za mkononi na mauzo ya vocha za simu. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa ni 2.1% kwa mwaka 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena kama alivyosema Naibu Waziri, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kwamba siku ya Alhamisi tarehe 15 Julai, 2010 ifikapo saa sita ya usiku, itakuwa ndio siku ya mwisho ya kuandikisha simu na *sim cards* na baada ya hapo zile ambazo zitakuwa bado hazijasajiliwa zitazimwa. Hivyo tufanye bidii kuandikisha ili kukwepa usumbu unaoweza kujitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Wabunge 49 wamechangia katika sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia. Wapo Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja mbalimbali kuhusu sekta ya mawasiliano, sayansi na teknolojia kwa kuzungumza hapa Bungeni na wengine kwa maandishi. Naomba sasa niwatambue waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale ambaao walichangia kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambaao walichangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Tatou Ntimizi, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na Mheshimiwa George Simbachawene. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Anna Makinda, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Athuman Janguo na Mheshimiwa Pindi Chana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Waheshimiwa Wabunge niliowataja ilikuwa ni mizuri sana. Aidha, sio rahisi kujibu kwa kina na kutosheleza hoja zote za

Waheshimiwa Wabunge kwa muda huu mfupi nilionao. Ninaahidi kwamba hoja zote tutazijibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote waliopo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, umezingatiwa na maoni ya Kambi ya Upinzani, vilevile yamezingatiwa. Hata hivyo, ningependa nitumie muda mfupi nilionao nijaribu kutoa ufanuzi katika baadhi ya maswali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kutokana na Kamati ya Miundombinu, kumekuwa na maswali mwengi lakini moja lilikuwa ni tutizame namna ya kutumia matokeo ya utafiti katika kutoa maamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba Serikali kwa kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia na Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia, ina mikakati ya kuanzisha atamizi yaani *incubators* na kongano ama *clusters*, ili kuweza kuhawilisha matokeo mazuri ya utafiti yaweze kuwafikia wajasiriamali walengwa na wananchi kwa ujumla. Mkakati huu unategemea kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wake ili iweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri nililitaja jina la Mheshimiwa Simbachawene, inaonekana kwamba nililiruka. Naomba kumtamka kwamba vilevile alichangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalí lingine ambalo lilijitokeza ambalo ni la kisera lakini hili lilikuwa ni agizo la Mheshimiwa Rais kwamba utafiti na maendeleo upewe angalau 1% ya Pato ghafi la Taifa kwa kila mwaka. Hii imetokana na maamuzi yaliyofanywa na viongozi wa Serikali wa nchi za Kiafrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ninayoyatoa ni kwamba mwaka jana tulipewa shilingi milioni 900 kwa ajili ya utafiti ambazo kwa kweli hazitoshi na kwa mwaka huu kama nilivyosema katika hotuba yangu, tumepewa kiasi cha shilingi bilioni 30 kwa ajili ya utafiti na maendeleo na kwamba hii ni historia katika nchi yetu kwa kutengewa kiasi kikubwa namna hiyo na nilieleza vilevile kwamba fedha hizi zitaelekezwa zaidi katika kujenga uwezo na vile vite kuimarisha vituo ikiwa ni pamoja na kulenga utafiti ambao utaenda sambamba na tamko la Serikali la mwaka jana la Kilimo Kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo lingine lilikuwa ni mgogoro wa ardhi wa Karangai, mahali ambapo taasisi ya Nelson Mandela itajengwa. Ni kweli kuna tatizo hilo, lakini Waziri Mkuu alitiisha mkutano mwaka jana tarehe 01 Agosti, ambao ulihusisha Wizara zinazohusika, Mkuu wa Mkoa wa Arusha na taasisi mbalimbali na ikaagizwa kwamba suala hili lishughulikiwe na Mkuu wa Mkoa wa Arusha pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru. Nimeambiwa keshokutwa tarehe 02 Julai, watakuwa na kikao kwa ajili ya kutatua tatizo hilo na Mkuu wa Mkoa wa Arusha aliniambia kwamba anavyoona mambo yalivyokaa, bila ya shaka tatizo hili linaweza kutatuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kulikuwa na agizo lingine kwamba Serikali ijenge barabara zile ziendazo kwenye Taasisi ya Nelson Mandela kwa kiwango cha lami,

ukizingatia hadhi ya jina ambalo tunalitumia kwa sasa. Kamati ya Kitaifa iliyoundwa kusaidia na kufuatilia uwekezaji wa miundombinu imehamasisha Wizara, Idara na Asasi mbalimbali kusaidia uwekaji wa miundombinu hiyo ikiwa ni pamoja na barabara ziendazo kwenye *campus* hiyo; na kwa kupitia *TANROADS*, TAMISEMI na Halmashauri za Meru na Arusha ambazo zimeitikia wito huu, inategemewa kwamba uboreshaji wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Moshono hadi kijiji cha Nambala ilipo *campus* ya Taasisi ya Tengeru utafanywa na *TANROADS*. Kwa hiyo, kuna maendeleo katika maagizo haya ambayo aliyatoa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Kwa kuwa taasisi hii ni mpya, ipewe upendeleo katika kupewa fedha za matumizi mengine. Hili limepokelewa na kwa mwaka huu kiasi cha shilingi bilioni mbili zimetengwa ili kusudi kutekeleza majukumu hayo. Lakini vilevile ningependa kuwaarifu kwamba Serikali kama nilivyosema asubuhi imewezesha kwa Taasisi hii kupata fedha kiasi cha shilingi bilioni 38.7 kwa ajili ya ukarabati wa Chuo kilichokuwa kinaitwa *CAMARTEC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo lingine lilikuwa ni kulipatia Shirika Posta mtaji. Ninasema kwamba Serikali inaendelea kurekebisha mizania ya Shirika na kufanya tathmini ya mtaji kwa ajili ya shirika hilo kwa nia ya kuboresha mtaji na kuweka mazingira mazuri ya kuliwezesha shirika kupata mikopo kutoka taasisi za fedha kwa ajili ya mpango wa maendeleo ikiwa ni pamoja na kuongeza vituo vyta kutolea huduma ya tovuti. (*Makofi*)

Pili, iliagiza kwamba marejesho ya shilingi bilioni mbili za Posta; Posta imetumia shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya kuwalipa wastaafu na baada ya kufanya mkutano tarehe 07 Desemba, 2009 na Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Uchumi, tulikubaliana kwamba watazame uwezekano wa kuweza kulipa fedha hizi. Zipo fedha ambazo zinatakiwa kwenda kwenye mfuko wa Bima shilingi bilioni 19.54, fedha za wastaafu wengine ambazo ni shilingi bilioni 8.2 na hizi ambazo Shirika limezitumia kwa kuwalipa wastaafu jumla inakuja shilingi bilioni 29.84. Kwa mwaka huu wa fedha na kutokana na ufinyu wa Bajeti, Wizara ya Fedha na Uchumi imeahidi kuilipa Posta shilingi bilioni mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ilikuwa ni kuimarissha uwezo wa *TTCL*. Ni kweli *TTCL* kifedha ina hali mbaya; inadai Idara za Serikali na Wizara mbalimbali jumla ya shilingi bilioni 9.2. Na hizi zimehakikiwa lakini zilipopelekwa Hazina tumeambiwa kwamba zile ambazo zimethibitishwa ni shilingi bilioni 6.3 kwa hiyo bado zilizobakia zinafanyiwa uhakiki lakini Wizara tumesema kwa zile ambazo zimeshapata uhakiki ni vyema zikalipwa ili kusudi Shirika hili liweze kujiendesha lenyewe. Lakini wakati huo huo waraka kwenda Serikalini umeandikwa ili kusudi Shirika liweze kupata *guarantee* ya kuweza kukopa na kuweza kujiendesha lenyewe. Waraka huo upo katika ngazi ya juu Serikalini, ili kuweza kuidhamini *TTCL* iweze kupata mkopo kwa jili ya hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lilikuwa ni mambo ya *ICT* kuhusu kutekeleza maagizo ya Kamati. Kamati ilitoa maagizo 25 na yote yametekelezwa na ndio maana Mwenyekiti wa Kamati alikuwa anapongeza kwa kazi nzuri ambayo imefanyika.

Lakini akazungumzia juu ya ufinyu wa fedha. Ni kweli tunasema kwamba kuna ufinyu wa fedha hasa za miradi. Kutokana na kwamba Bajeti ya Wizara imeshuka kwa 17.5% na kulikuwa na miradi mahususi ambayo tulitegemea kwamba itekelezwe ambayo kutokana na ufinyu huo miradi hiyo kwa sasa haiwezi kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiit, miradi hiyo ilikuwa ni ya anuani za makazi na *symbol* za Posta, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Saalam hasa *campus* ya Mwanza pamoja na mradi wa *super computer*. Tume ya Nguvu za *Atomic*, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela; kutokana na ufinyu huu wa Bajeti, shughuli zilizokuwa zimepangwa haziwezi kutekelezwa kikamilifu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na maagizo mengine ambayo yalikuwa yanazungumza juu ya umuhimu wa kuendeleza TEKNOHAMA nchini. Tunasema Serikali imepokea ushauri huu na tayari umetekelozwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis tangu mwaka 2004 kwa kuliweka somo la TEKNOHAMA katika mitaala ya kufundishia katika ngazi za chekechea, shule za msingi, sekondari na stashahada mpaka vyuo vikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo lilizungumzwa liliikuwa ni lile linalohusu kukamilisha Kanuni za *EPOCA*; sheria ile ya mawasiliano ya *ki-electronic* na Posta. Nasema kwamba *EPOCA* kama alivyozungumza Naibu Waziri, imeanza kutumika rasmi tarehe 18 Juni. Kanuni za sheria husika huanza kutengenezwa mara baada ya sheria kuanza kutumika. Hata hivyo, mchakato wa kutengeneza Kanuni hizi umekwishaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuyapa kipaumbele masomo ya sayansi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, ipo katika mchakato wa kuandaa Kamati ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia itakayo jumuisha Wajumbe kutoka Wizara yangu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis na TAMISEMI; lengo ni kuimrisha elimu ya msingi pamoja na sekondari. Kupitia Kamati hii, Serikali itashughulikia pia suala la ujenzi wa maabara. Aidha, Serikali imeongeza vyuo vya walimu na kutoa mkopo kwa 100% kwa wale wanaochukua masomo ya ualimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo lilitolewa maamuzi ilikuwa juu ya usajili wa namba za simu, hili naona limeshatolewa majibu na kwamba muda umekwishaongezwa ni imani yangu kwamba baada ya muda huu ambao umetolewa tutatumia vizuri zaidi ili kusudi tuweze kukamilisha usajili wa simu zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kumtambua Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale ambaye amechangia kwa maandishi. Kwa upande wa Kambi ya Upinzani ushauri ulitolewa kwamba Wizara iweze kuweka mkakati, itaweka mkakati gani? Wa utekelezaji wa sera zake kwa kuzingatia ufinyu wa Bajeti maana yake sasa hivi tuna sera tunazozishughulikia tano. Maelezo ni kwamba Serikali kwa kuzingatia ufinyu wa Bajeti uliopo imeainisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji wa sera ambazo zimepitishwa, kwani sera zote muhimu kwa kuwa uanzishaji wake ultokana na

mahitaji yaliyoibuliwa katika jamii ili iweze kutoa muongozo katika nyanja husika. Aidha, dhamira ya Serikali ni kutekeleza sera zote hata hivyo kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali itatekeleza sera kulingana na vipaumbele iliyojiwekea. (*Makofi*)

Vilevile kulitolewa hoja kwamba kutotekelezwa kwa agizo la Rais la tarehe 17 Februari kuhusu utengaji wa asilimia moja hili nimekwishalitolea maelezo na kwamba safari huanza na hatua moja, mwaka huu tumetengewa hiyo shilingi bilioni 30 ni imani yangu kwamba tutazidi kutengewa fedha zaidi kwa ajili ya utafiti na maendeleo. (*Makofi*)

Kuhusu Mfuko wa Maendeleo nasema fedha zilizotengwa na Serikali shilingi milioni 419 ni kwa ajili ya nini? Tunasema shughuli za mfuko wa mawasiliano zilianza rasmi mwezi Julai, 2009 toka kuanza shughuli hizo mshauri mwelekezi ameweka mipango ambayo itaanza kutekelezwa mwaka 2010/2011 mara baada ya kupitishwa na bodi ya mfuko. Kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote vyanzo vinne vya mapato vimebainishwa kwanza ni Serikali yenyewe ambayo kwa mwaka huu imetenga kiasi cha shilingi milioni 419, Mamlaka ya Mawasiliano imetenga shilingi milioni 300 na tuna mategemeo ya mchango kutoka watu wa huduma wa mawasiliano ambao wanakadiriwa kuwa shilingi bilioni tatu na shilingi milioni 26 washirika wa maendeleo Benki ya Dunia imeweka ahadi ya kufadhili miradi kwa kiasi cha dola za Marekani milioni mbili kwa mwaka huu wa fedha. Hivyo tunategemea kuwa kuanzia shughuli za mfuko zitafanyika kwa ufanisi zaidi, aidha, hizo fedha zilitolewa na Serikali japokuwa ni kidogo zimetengwa kwa ajili ya kununulia vifaa vya matumizi ya Mfuko wa Mawasiliano kama vile magari, samani za offisi na *software* kwa ajili ya kuzifanyia kazi na mfuko ili ziende vilevile katika sekta binafsi.

Eneo lingine lilikuwa kuongeza muda wa usajili, hili tayari tumeshalitolea maelezo, kuhusu Mkongo wa Taifa kwenda katika mikoa ya pembezoni Naibu Waziri ameshalitolea maelezo na kwamba hii ilikuwa ni awamu ya kwanza, awamu ya pili itafika maeneo mengi ikiwa ni pamoja na Makao Makuu yote ya Mikoa na Wilaya Tanzania Bara na Visiwani. (*Makofi*)

Vilevile kwa kuwa Tanzania inazungukwa na nchi nane na kati ya hizo nane nchi sita hazina hazipakani na bahari basi wote hao wanataka kutumia njia hii na ndiyo maana tunazungumzia juu ya Dar es Salaam au Tanzania kuwa *ICT harbour for service and infrastructure* ambako tayari mikongo ya baharini miwili ya *SEACOM* na *Easy* tayari imeunganishwa. Kwa hiyo, mkongo huu unafaida nyingine ikiwa ni pamoja na biashara kwa sababu hii inaitwa *ACT information highway*. (*Makofi*)

Kuhusu mkataba kati ya *TTCL* na *ZAIN* mkataba huo ulitiwa saini tarehe 5 Agosti, 2005 na kwamba Serikali ingekuwa na hisa za kiasi cha asilimia 25 na *ZAIN* ingekuwa na hisa za kiasi cha asilimia 35. Lakini *TTCL* imepitia katika mikono mingi ya kiuendeshaji ikiwa pamoja na kampuni ya Canada ambayo inayoitwa *SASCATEL* baada ya hapo *SASCATEL* iliondoka Julai, 2009 na ikaona kwamba kuna ulazima wa kuweka menejimenti ya kwetu sisi wenyewe na menejimenti hiyo imeanza kufanya kazi lakini ilikuwa ni menejimenti ya mpito na sasa hivi juhudhi zinafanywa ili kupata menejimenti

ya kudumu na tunaamini ifika mwezi Agosti, 2010 tatizo hili litakuwa limekwisha. (*Makofi*)

Lakini vilevile kulikuwa jambo ambalo limezungumzwa kwamba ile kubadilisha jina kutoka *CELTEL* kwenda *ZAIN* kwamba inaonekana kwamba kulifanyika biashara pale, hili ni jambo ambalo itabidi pengine tuendelee kufuatilia zaidi kwa sababu tulipowafuutilia wao walisema hawakuza walibadilisha jina tu ili liendane na mazingira na sehemu zingine wanazofanya biashara. Lakini la hivi karibuni ni hili la *ZAIN Africa* kuuzwa kwa *BAT AIRTEL* na hizi nchi 15 za Afrika ambako *ZAIN* ina *operate*, lakini nchi ambayo ina hisa ni sisi Tanzania ambao tuna hisa za asilimia 40. (*Makofi*)

Sasa kwa kawaida kwa kuwa tuna hisa tunalipwa mgawanyo wa mapato (*dividends*) katika kipindi toka kuingia ushirika huu ubia Tanzania imeshalipwa dola za Kimarekani bilioni 11.2, kwa hiyo tumeypata *shares* kutoka hapo. Lakini sasa wanapouza kwa kampuni nyingine sisi vilevile tuko mle ndani na hiyo asilimia 40 kwa sababu vinavyouzwa ni *asset* sasa katika mazungumzo tumezungumza nao Jumatatu, tarehe 21 tukawaambiwa kwamba haiwezekani katika fedha mnazopata ambazo mnauza *assets* ambazo ni *jointly owned*, ni lazima Serikali ya Tanzania ipate. Kwa hiyo, ndiyo ambalo linafuutiliwa wakokotoe mahesabu ili kusudi Tanzania nayo iweze kunufaika na mauzo hayo ya hiyo kampuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo yamezungumzwa ni pamoja na *Tele Centres* kwamba kuna mkakati gani wa kuharakisha utekelezaji wa vituo vya mawasiliano hususan kituo cha Mpanda ambacho hakijaanza kufanya kazi? Nasema Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano tayari imeainisha na kukagua maeneo ya kuanzisha vituo vya mawasiliano ikiwepo kile cha Wilaya ya Mpanda. Ufungaji wa vifaa vya mawasiliano katika vituo hivyo utakamilika ifikapo Agosti, 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulizungumzwa juu ya mradi wa *super computer* kwamba kumekuwa na kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huu, maeleo ni kwamba utekelezaji wa mradi huu umefikia katika hatua ya kuridhisha kama ifuatavyo, ukarabati wa vituo saba kati ya kumi vya habari ya jamii yaani *Commit Information Centre* vya Mara. Usimikaji wa vifaa vya ukarabati wa ofisi za madarasa katika taasisi zimeshafanyiwa majaribio na vinafanya kazi. *Super computer* hiyo imeshajaribiwa pia inafanya kazi vizuri na mawasiliano kati ya taasisi, kituo kikuu na vituo hivyo vidogo saba vilivyokamilika katika huduma ya tiba, mtandao navyo vimekamilika na yanafanya elimu ya mtandao nayo inafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko katika mchakato wa kuzindua mradi huu mwezi Agosti, 2010. Vifaa na samani kwa ajili ya vituo hivi vitatu vilivyobaki vimeshanunuliwa na kupelekwa katika vituo husika na ukarabati wa vituo hivi utakamilika katika mwaka wa fedha 2010/2011.

Eneo lingine ilihusu udahili wa wanafunzi katika taasisi zetu kwamba inaelekea tunaendelea kupanua lakini hatuweki mazingira kuwa mazuri kwa mfano miundombinu, kama vile mabweni, karakana, mashine zake pamoja na maabara, ninachosema ni kweli

hali hii ipo lakini Serikali inajitahidi mtakumbuka nilipoeleza juu ya shilingi bilioni 30 tumesema kazi moja ya kwanza ni kuongeza uwezo kwa maana ya rasilimali watu, miundombinu pamoja na karakana na maabara mbalimbali ili kusudi wanafunzi waweze kupata elimu bora. (*Makofi*)

Vilevile ilizungumzwa kwamba wanafunzi wa kike ni wachache katika fani za sayansi na teknolojia hili ni kweli lakini lilijulikana kwa muda mrefu Serikali imeanzisha katika vyuo vyake mipango mbalimbali ikiwa na *pre-entry program for female students*, vilevile wasichana wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi kila mwaka wanapewa zawadi na vilevile hao wanaochukua masomo ya sayansi wanapata mkopo asilimia 100 na hivi vyote ni vivutio kusudi wasichana wengi wajiunge katika masomo ya sayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali maeneo ambayo yamezungumziwa ni mengi na kwa muda huu ambao nimepewa si rahisi kuyamaliza yote na kama nilivyoahidi, kwa mfano maswali ya watu wengi ambayo wameuliza Wabunge wengi mengi hatukuyajibu kwa mmoja mmoja, lakini tumetoa maelezo ya kijumla lakini napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba haya tutayafanya kwa maandishi ili kusudi Wabunge wote waweze kupata haya maelezo ambayo nimeyatoa na kule ambako tumeshindwa kutoa maelezo kamili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nichukue nafasi hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika hoja, kuna maswali mengi lakini kama nilivyosema tutajitahidi kwa uwezo wetu wote kuweza kutoa majibu haya kwa maandishi kabla ya Bunge hili halijaisha kwa sababu hatuna uhakika nani anayerudi hapa lakini tuombeane kwamba sote tulipo hapa wenye nia njema tatarudi tena katika Bunge hili ili kuendelea kusukuma gurudumu la maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwa*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Peter Msolwa, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kuzipitia hoja zote zilizo nyingi kuhusiana na hoja yetu ya leo. (*Makofi*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 68 - Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia

Kifungu 1001 – Administration and General Sh. 1,586,290,000

MWENYEKITI: Mheshimiwa Said Amour Arfi baada ya kuwa peke yako nilidhani unakaa chini! Endelea. (*Kicheko*)

MHE: SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa sababu ya nia njema tu ndiyo maana nimekataa kukaa chini, wala sina tatizo niko kwenye programu 10, *sub vote 1001 Administration General*, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maoni ambayo nimeyawasilisha asubuhi ya Kambi ya Upinzani na ambayo yamepata majibu ya kuridhisha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, lakini Kambi ya Upinzani kwa niaba ya wananchi iliomba muda uongezwe wa kusajili simu na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu imeongeza wiki mbili. Lakini hali ilivyo mjini leo ukienda ukaangalia misururu ya watu iliyopo na pia kwamba mfumo mzima wa kuhifadhi namba zilizosajiliwa bado si mzuri tumeambiwa tupige namba 106 ili tuhakiki simu zetu kama zimesajiliwa lakini wengi wanaofanya hivyo wanaambiwa simu zao hazijasajiliwa wakati wameshazisajili. Kwa hiyo, hata mfumo wenyewe hauko sawasawa wa kuhakikisha kwamba wale wote ambao wamesajili simu zao wamesajiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nataka kuiomba Serikali kwa niaba ya wananchi kwamba muda wa wiki mbili zilizoongezwa hautoshi. Maadam ni Serikali sikivu isikilize kilio cha wananchi iongeze muda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara yangu na Waziri Kivuli, Mbunge wa Mpanda Kati kupitia CHADEMA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la kusajili simu lilianza mwaka jana mwezi Machi mwanzoni kwa kuanza kusema kwamba zile simu ambazo zilikuwa hazioneishi namba zile zimefutwa na watu wakatayarishwa *mentally* kwamba ifikapo tarehe 01 Julai, 2009 itabidi waanze kuandikisha ama kusajili simu zao. Tumekwenda mpaka Desemba tarehe 31, 2009 ikaonekana kwamba uandikishaji wa *sim-cards* na simu zenyewe ulikuwa bado. Zilikuwa karibu *sim-cards* milioni nne hivi.

Sasa baada ya pale ndiyo tukajadiliana na kusema tuongeze muda wa miezi sita na ikatangazwa na wameendelea kutangaza hawa *operators* wenyewe na *TCRA* imetangaza sana mpaka kufikia tarehe hii ya leo 30 Juni, 2010 lakini bado inaonekana kwamba kuna baadhi ya watu. Sasa hii misururu inayooonekana ni kwamba watu ukishaongeza muda basi wanapumzika kabisa, ndiyo maana kumekuwa na misururu mingi watu wanakimbizana huku na kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna wengine wanassema walishajiandikisha lakini wakitafuta hiso takwimu kwenye *computer* hazipatikani. Kinachotokea kwa hao *operators* ambao wanaandikisha ni kwamba wanapokea hiso *forms* kutoka kwa ma-agent

wao lakini hawaingizi kwenye *database* hicho ndicho ambacho wanakuwa wamechelewesha na baada ya kugundua hilo na TCRA kuzungumza na *operators* muda uliongezwa wa majuma mawili inaonekana kwamba unaweza kutosha. Kwa hiyo, hii ya kusema kuongeza tena baada ya hapo kidogo itakuwa ngumu pengine kuwe na mazingira mengine, napenda kuwasilisha. (*Makofî*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Sh.395,332,000
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh.937,875,000
Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.112,680,000
Kifungu 1005 - <i>Legal Unit</i>	Sh.55,215,000
Kifungu 1006 - <i>Information Education and Communication Unit</i>	Sh.223,697,000
Kifungu 1007 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 221,792,000
Kifungu 1008 - <i>Management Information System</i>	Sh.121,381,000
Kifungu 2001 - <i>Communication Division</i>	Sh.547,466,000
Kifungu 2002 - <i>Information, Communication and Technology</i>	Sh.732,710,000
Kifungu 3003 - <i>Science and Technology</i>	Sh.21,656,252,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO NA MAENDELEO

Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i>	Sh.115,833,333
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh.100,000,000
Kifungu 1008 - <i>Management information system</i>	Sh.1,295,000,000
Kifungu 2001 - <i>Communication Division</i>	Sh.3,109,586,000
Kifungu 3003 - <i>Science and Technology</i>	Sh.39,806,490,667

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)
(*Bunge lilirudia*)

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi ya kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2010/2011 kifungu hadi kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu likubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa Fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Na kwa jinsi hiyo basi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2010/2011 kwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia yameshaptishwa rasmi na Bunge kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote ningependa kuwatakia kila la heri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii katika utekelezaji wa Bajeti iliyoko mbele yetu kwa mwaka ujao wa fedha. Tunatumaini tutakapokutana kwenye Bajeti ijayo mwakani kwa vile Wabunge wote tunarudi Bungeni kutakuwa na maisha bora zaidi kwa kila Mtanzania. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zilizopangwa katika *Order Paper* zimekamilika zote naomba kuchukua fursa hii sasa kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 12.10 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 1 Julai, 2010 saa tatu asubuhi*)